31 SEPTEMBA, 2026

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Nne – Tarehe 31 Agosti, 2026

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Cecilia D. Paresso) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa karibuni katika Mkutano wetu wa Nne, Kikao cha Nne.

Katibu.

NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA:

Maelezo ya Waziri wa Fedha kuhusu Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali zinazohamishika wa Mwaka 2026.

MHE. KAKULU B. KAKULU K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali zinazohamishika wa Mwaka 2026.

MWENYEKITI: Katibu.

NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaanza na maswali. Swali la kwanza litaelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu.

Sasa ninamwita Mheshimiwa Yumna Mmanga Omar, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 37

Mkakati wa Serikali Katika Kukuza Vipaji na Ujuzi kwa Vijana Wenye Ulemavu

MHE. YUMNA MMANGA OMAR aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani mahsusi wa kukuza vipaji na ujuzi kwa vijana wenye ulemavu, ili kuongeza ajira na ushiriki wao katika uchumi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Yumna Mmanga Omar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya CCM ya mwaka 2025 - 2030 Kifungu cha 95, imelenga kuwashirikisha na kuwawezesha watu wenye ulemavu kupata ajira zenye staha na kuwajengea uwezo wa kushiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imeweka mkakati wa Kitaifa wa kukuza na kuendeleza vipaji na ujuzi kwa vijana unaoongozwa na Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007, Toleo la mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, katika Dira ya Taifa ya mwaka 2050, Serikali imeweka mkakati wa kukuza Elimu Jumuishi na ujumuishwaji wa vijana wenye ulemavu katika elimu, mafunzo ya ufundi, ajira na shughuli za kiuchumi kwa kutambua kuwa, ulemavu haupaswi kuwa kikwazo cha mtu kutumia kipaji chake na uwezo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza mikakati hiyo, jumla ya vijana wenye ulemavu 643 walijiunga na kuhitimu mafunzo ya ufundi stadi kwenye vyuo vitano vya ufundi, ikiwemo *VETA*, kwenye maeneo mbalimbali nchini kuanzia mwaka 2023 hadi 2025. Vijana hao, waliwezeshwa kupata ujuzi katika fani mbalimbali za umeme wa majumbani, useremala, uungaji vyuma, ushonaji wa nguo na viatu, kilimo na ufugaji na ujenzi na uashi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Serikali imeendelea kuwawezesha vijana wenye ulemavu kwa kutenga 30% ya zabuni za umma, ambapo kufikia mwaka 2024/2025 jumla ya vikundi 703 vimesajiliwa kwenye mfumo wa *NEST,* ili kuhakikisha ujuzi wanaopata uweze kutumika kuwapatia ajira na kujikwamua kiuchumi kupitia shughuli za ujasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali imeendelea kutenga 10% ya makusanyo ya halmashauri, kwa ajili ya kutoa mikopo kwa makundi maalum, ambapo asilimia mbili hutengwa, kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Katika kipindi cha mwaka 2021 hadi kufikia mwaka 2026 jumla ya kiasi cha fedha shilingi bilioni 26.87 kimetolewa, kwa ajili ya kuwawezesha watu wenye ulemavu. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yumna Mmanga Omar, swali la nyongeza.

MHE. YUMNA MMANGA OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na majibu mazuri ya Serikali, ningependa kujua. Je, Serikali ina mfumo gani madhubuti wa kutambua vijana hawa ambao wamepata mafunzo haya, ni wangapi ambao wamepata ajira, wamejiajiri na kuanzisha biashara endelevu? Iwapo mfumo huo upo, Serikali inaweza kutueleza matokeo halisi yaliyopatikana hadi sasa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza naanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Yumna kwa kuwasemea watu wenye ulemavu. Amefanya hivyo hata katika Bunge la Bajeti lililopita, ameendelea kuwasemea walemavu, ili waweze kunufaika na fursa katika nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanzisha mfumo rasmi wa kupata taarifa kutoka katika halmashauri zetu kote nchini, lakini pia, tunaendelea kutumia wakurugenzi wetu na maafisa maendeleo ya jamii katika halmashauri zote nchini kuwafikia vijana wenye ulemavu, kutoa elimu na kuhakikisha na wao wananufaika na ile

mikopo ya 10%, zile asilimia mbili na pia, katika yale manunuzi ya umma *(PPRA)* nao wanaingia katika mifumo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tumepata takwimu hii ya zaidi ya vikundi 703 na mwanzoni vilikuwa vikundi 45 tu, lakini mpaka sasa kuna vikundi 703 na tunaona matokeo. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Yumna, pamoja na walemavu wengine nchi hii ni yao na wao lazima tuwajumuishe katika kukuza uchumi wao binafsi. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Faraji Nandala, swali la nyongeza.

MHE. FARAJI B. NANDALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi. Ili tuweze kuandaa vijana bora walemavu waingie kwenye soko la ushindani la ajira tunahitaji kuwandaa kuanzia ngazi ya shule ya msingi, lakini mazingira ya shule nyingi za msingi, hasa zile zinazo wa-*occupy* hawa vijana wenye ulemavu, siyo rafiki kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwenye Jimbo la Ndanda tuna Shule ya Msingi Lukuledi Maalum, shule hii haina uzio wala jenereta. Je, ni lini Serikali itakwenda kuboresha mazingira yale, ili tuweze kuandaa vijana bora wenye ulemavu watakaoingia kwenye soko la ushindani la ajira?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Faraji, ndugu yangu, kijana mwenzangu. Mara zote tumekuwa tunawasiliana katika masuala mbalimbali, hasa katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Faraji, sisi Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEM, tunaendelea kufuatilia masuala haya na mara nyingi tunaongozwa na Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo.

Tunapokwenda ziara kukagua miundombinu, huwa tunakagua masuala yote na tunachukua taarifa. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Faraji, tunaendelea kufanyia kazi masuala haya ya watu wenye ulemavu, ili na wao wanufaike katika miundombinu pamoja na elimu. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nyamizi Mhoja, swali la nyongeza.

MHE. NYAMIZI S. MHOJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Majibu ya Serikali ni mazuri na yameelekeza kwamba, kuna vyuo vya ufundi vya watu wenye ulemavu, ambavyo ndio vinazalisha ujuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hivi vyuo vingi bado mazingira yake yanahitaji kuboreshwa. Mfano, wakalimani hawapo na mambo mengi, vinapitia changamoto. Je, ni nini mkakati wa Serikali kuboresha, ili wanafunzi hawa wa *VETA* waweze kupata ujuzi unaostahili?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba kujibu swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kuratibu maeneo yenye upungufu, yenye uhitaji na tunachukua hatua. Nampongeza sana Mheshimiwa Ummy Nderiananga, anaendelea kufanya kazi hii kwa dhati na pale ambapo pana mapungufu anayaleta moja kwa moja Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na tunachukua hatua kuhakikisha kwamba, maeneo yote yenye uhitaji tunapeleka wataalam, ili waweze kufundishwa na wao waweze kutoa mchango katika Serikali yao. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asha Juma Feruz, sasa aulize swali lake.

Na. 38

Kuwaunganisha Wahitimu wa Kada Zinazoendana na Miradi ya Kimkakati

MHE. YUMNA MMANGA OMAR K.n.y. MHE. ASHA J. FERUZ aliuliza:-

Je, Serikali imewaunganishaje wahitimu wa kada zinazoendana na utekelezaji wa miradi ya kimkakati nchini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu wali la Mheshimiwa Asha Juma Feruz, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa inatumia miradi mikubwa ya kimkakati kuwaunganisha wahitimu wa kada mbalimbali na fursa za miradi hiyo, kama sehemu ya kuzalisha ajira na kuwapa uzoefu wahitimu hao. Takribani ajira 35,000 zimezalishwa katika ujenzi wa Mradi wa *SGR*, 10,000 katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi *(EACOP)*, 10,000 katika ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere, ajira 1,500 katika ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, ajira 1,500 katika ujenzi wa Daraja la Kigongo – Busisi na 3,000 katika upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine ni kuhusisha na kuimarisha programu za mafunzo ya uzoefu wa kazi *(internship),* ili wahitimu waweze kupata uzoefu unaoendana na mahitaji ya waajiri. Hadi Aprili, 2026 jumla ya wahitimu 29,902 walikuwa wamepata mafunzo hayo. Aidha, Serikali imeandaa Mwongozo wa Taifa wa Mafunzo kwa Vitendo kwa Wahitimu wa mwaka 2017 unaotumika katika sekta ya umma na binafsi. Vilevile, kuwajengea uwezo vijana na wafanyakazi katika maeneo yenye mahitaji

makubwa ya kitaaluma na kiufundi. Hadi kufikia Aprili, 2026 Watanzania 168,657 walikuwa wamenufaika na programu hiyo. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yumna Mmanga, maswali ya nyongeza.

MHE. YUMNA MMANGA OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sambamba na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujua, miradi hii ya kimkakati inazalisha sana fursa mpya za ajira na ujuzi. Je, Serikali inahakikisha vipi wanafunzi wahitimu wenye ulemavu wanafaidika na fursa hizi za ajira mpya na ujuzi? Ni kwa namna gani inawafuatilia wao kuweza kunufaika na ajira hizo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Kwanza nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge, amekuwa mahiri sana katika kupigania suala la watu wenye ulemavu katika sekta hii ya ajira na muda si mrefu ametoka kuuliza swali la aina hiyohiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua kwamba, miradi ya kimkakati katika dhana ya *local contexts* inasisitiza ajira kwa wazawa na pia, inahusisha ajira kwa watu wenye ulemavu. Kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, katika Kitengo cha Kamishna wa Kazi, tunafanya kaguzi mbalimbali kuhakikisha uzingatiaji wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu, Sura 183, ambayo inasisitiza kwamba, kila mwajiri katika mradi huu anatakiwa kutenga nafasi, kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tunaendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara

kuhakikisha watu wenye ulemavu, wakiwa ni wadau muhimu kabisa katika kutekeleza miradi hii ya kimkakati, wanapata fursa ya ajira.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri Deus Sangu, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Sasa namwita Mheshimiwa Said Ali Mbarouk.

MHE. RASHID HABIB ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa...

MWENYEKITI: Sijakuita.

Mheshimiwa Rashid, kwa niaba.

Na. 39

Kuondoa Utaratibu wa Sasa wa Kikokotoo kwa Watastaafu wa Jeshi La Polisi

MHE. RASHID HABIB ALI K.n.y. MHE. SAID ALI MBAROUK aliuliza:-

Mpango gani wa kuondoa utaratibu wa sasa wa kikokotoo kwa Wastaafu wa Jeshi la Polisi, ili kuboresha maslahi kwa Wastaafu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Ali Mbarouk, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ni kuendelea kuboresha mafao ya wastaafu wote, ikiwemo wa Jeshi la Polisi, kadiri mifuko ya pensheni inavyoimarika na si kuondoa utaratibu uliopo sasa unaotumika kulipa mafao. Mifuko ya pensheni inatumia kanuni

maalum au kikokotoo katika kulipa mafao kwa wanachama wanaochangia katika mifuko hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni hii hutumika kwa wafanyakazi wote walioajiriwa katika sekta ya umma na binafsi, ikiwemo Jeshi la Polisi. Aidha, Kanuni hii hairuhusu kuwa na ukokotoaji tofauti katika mfuko wa pensheni kwa wanachama wenye sifa zinazofanana. Nninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rashid, maswali ya nyongeza.

MHE. RASHID HABIB ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Said Ali Mbarouk, ninaomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, taasisi nyingine za ulinzi na usalama hazikuwekwa katika mfumo huu. Je, ni vigezo gani vilivyotumika kuwekwa Jeshi la Polisi katika mfumo huo wa kikokotoo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali namba mbili. Je, Serikali haioni haja sasa, kwa sababu ya malalamiko ya muda mrefu ya mfumo huu, kuwaondolea Jeshi la Polisi mfumo wa kikokotoo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. Nampongeza Mheshimiwa Rashid, kwa niaba ya kuuliza swali hili, juu ya masuala ya kikokotoo kuhusu ni kwa nini, Jeshi la Polisi limeingia katika kundi hili, lisiwe kama taasisi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwanza niweke sawa; siyo Jeshi la Polisi pekee katika taasisi hizi za ulinzi na usalama ambazo zinahusika katika ulipaji wa mafao kwa njia hii. Pia, kuna taasisi kama Jeshi la Magereza na nyingine kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa

Mbunge si kwamba, Jeshi la Polisi kuwepo katika mfumo huu wanabaguliwa, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amefanya jitihada kubwa kuhakikisha mifuko hii inazidi kuimarika. Mwaka 2018 mifuko hii iliunganishwa kwa sababu moja tu, ilikuwa haipo himilivu katika kulipa mafao. Katika kipindi hicho, kwa Mfuko wetu wa *PSSF,* kulikuwa na deni maarufu la *pre-1999,* la zaidi ya shilingi trilioni 4.6. Mpaka ninavyozungumza sasa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amelipa deni la shilingi trilioni 4.2 na kiasi kilichobaki kipo katika uhakiki, ndani ya muda mfupi deni hilo lote la shilingi 4.6 litakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mfuko wetu wa *NSSF* pia, nako Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amelipa shilingi 4,483,000,000,000. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni kuimarisha uhimilivu wa mifuko hii kulipa mafao; kufuatia hivyo, mifuko hii imeweza kulipa. Kwa mfano, *PSSF* tuna kauli inayosema, "tunalipa kama jana"; mstaafu, anapostaafu leo, anaenda nyumbani jana, mafao yake yanakuwa yamelipwa. Nakuhakikishia kwa kadiri tunavyoendelea kuimarisha uhimilivu wa mifuko hii, hata mafao au kikokotoo kitaboreshwa kwa watumishi wote wa sekta binafsi na umma. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, Mheshimiwa Rais ameonesha dhamira safi ya kulipa madeni yaliyokuwepo *PSSF* pamoja na *NSSF*. Je, Serikali haioni sasa, kuna umuhimu wa kukaa na wadau, wakiwepo wawakilishi wa vyama vya wafanyakazi na wawakilishi wa waajiri, ili kuboresha mafao ya watumishi hasa katika suala zima la kikokotoo?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, NA MAHUSIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika maelezo yangu ya awali; nia ya Serikali ya kuboresha mafao kwa wastaafu iko Dhahiri. Ndio maana nimesema jitihada ya kwanza ilikuwa ni kulipa madeni haya, ambayo ndiyo yalikuwa mzigo mkubwa kufanya mifuko hii isiwe himilivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, nia hii ya Serikali itaendelea na ndiyo maana hata kima cha chini cha mafao kwenye sekta ya umma kimeongezeka. Mheshimiwa Rais amekuta kima cha chini cha mtumishi aliyeko kwenye sekta ya umma kwenye mafao yake ilikuwa ni shilingi 100,000 lakini sasa analipwa shilingi 250,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakuhakikishia pamoja na mambo mengine haya, Serikali inaendelea kufanya tathmini na mwaka huu katika mifuko yetu tunaenda kufanya *actuarial evaluation*. Lengo ni kuona uhimilivu wa mifuko hii na kama uhimilivu utakuwa unatosheleza Serikali itaona sasa, namna gani ya kuboresha mafao haya. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwanahamisi Munkunda, swali la nyongeza.

MHE. MWANAHAMISI A. MUNKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninaomba kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada kubwa, ambayo Serikali inafanya, hasa kwa waajiri binafsi, bado kuna changamoto kubwa sana kwa waajiri binafsi kupeleka mafao ya wafanyakazi. Ni nini sasa mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba, waajiri binafsi nao wanawajibika kisheria kuhakikisha kwamba, wanapeleka mafao ya wafanyakazi? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, NA MAHUSIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuuliza swali muhimu sana, hasa kuhusu waajiri kutoka sekta binafsi. Kupitia mfuko wetu wa *NSSF* tumekuwa tunachukua hatua mbalimbali; kwanza ni kuunda timu maalum, *taskforce,* ambayo ilikutana na waajiri kuhakikisha kwamba, zoezi la kupeleka madeni yao, ambayo walikuwa hawajaleta michango ya wafanyakazi wanafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naliarifu Bunge lako Tukufu, ndani ya muda wa miezi nane tumeweza kukusanya zaidi ya shilingi bilioni 378 kwa waajiri ambao walikuwa hawajaleta michango yao. Isitoshe, tarehe 4 Juni, nimetoa unafuu kwa waajiri wale ambao wameshindwa kuleta michango yao na wanadaiwa *penalty,* kwa kufuta *penalty* kwa miezi sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa nafuu ya kwamba, wale watakaoweza kupeleka michango ya waajiri wao mpaka tarehe 31, *August* watasamehewa *penalty* zote kwa 100%. Wale ambao wataweza kuleta mafao yao kuanzia *August* mpaka *November* watasamehewa *penalties* kwa *75%* na wale ambao watachelewesha kuanzia mwezi *November* mpaka 31 *Disember* wao watasamehewa kwa 50%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hili limewavutia waajiri wengi na wanaleta michango ya wafanyakazi wao. Sasa tunaona mwelekeo kwamba, ifikapo Januari tutakuwa tumepunguza tatizo hili kwa kiasi kikubwa cha waajiri kutoleta michango kwa wafanyakazi ambao wamechangia katika Mfuko huu wa *NSSF*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Deus Sangu, Waziri wa Kazi, Ajira na Mahusiano tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea. Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI. Sasa ninamwita Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mbunge wa Ikungi Magharibi, aulize swali lake.

Na. 40

Ujenzi wa Vituo vya Afya, Ikungi Magharibi

MHE. ELIBARIKI I. KINGU aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga vituo vya afya katika Kata za Minyughe, Igombwe, Muhintiri na Mwaru katika Jimbo la Ikungi Magharibi?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri - TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mbunge wa Jimbo la Ikungi Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ina jumla ya kata 28, ambapo kata 09 zina vituo vya afya na kata 19 hazina vituo vya afya, hivyo wakazi wake wanapata huduma za msingi kwenye zahanati na huduma za dharura na rufaa katika vituo vya afya vya karibu, pamoja na hospitali ya wilaya. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 hadi mwaka 2025/2026, Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 2.3, kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya vya Ntuntu, Iyumbu, Irisya, Iglanson na Kingwi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali imetoa jumla ya shilingi milioni 250, kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya cha kimkakati katika Kata ya Misughaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu, kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya katika kata zitakazokidhi vigezo; zikiwemo Kata za Minyughe, Igombwe, Muhintiri na Mwaru katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Elibariki Kingu, swali la nyongeza.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali kutoka kwa kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Jafar, Naibu Waziri mchapakazi kabisa, nataka tu nijue. Je, sasa Waziri ananipa *commitment* gani, hasa kwa Kituo cha Afya cha Minyughe, Igombwe, Mwaru pamoja na Muhintiri ukizingatia kwamba, haya maeneo ni ya uzalishaji mkubwa, ambao ndio unafanya *base* ya kusimama kwa Halmashauri ya Ikungi kwa mapato kutoka kwa wananchi, lakini hawana vituo vya afya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Nataka nijue sasa, Naibu Waziri yuko tayari tukimaliza Bunge hili niongozanenaye jimboni, akajionee umbali wanaoupata wananchi wangu katika kutafuta matibabu kwenye kata ambazo zina vituo vya afya hapo jimboni? Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba kujibu maswali madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Immanuel Kingu, mpakwa mafuta, lakini mwakilishi wetu kule *IPU. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutenga fedha. Tathmini ambayo tumeifanya, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, zaidi ya vituo 364 tumevitengea fedha kuanzia katika mwaka huu wa fedha 2026/2027. Tunaanza na vile vituo 111, ndani ya vituo hivyo, vimo na vile ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja. Aidha, naipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, imetenga zaidi ya shilingi milioni 150 kukamilisha miundombinu katika vituo vya afya na zahanati. Namwelekeza mkurugenzi ampe ushirikiano wa dhati Mheshimiwa Mbunge, ili kuhakikisha kwamba, fedha zile walizotenga halmashauri zinaleta tija katika maeneo ambayo ameyataja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Mheshimiwa Kingu ni rafiki yangu sana na yupo njiani tu, nikiwa ninaelekea Mkoani Geita huwa ninapita pale. Juzi nimepita nikakumbuka ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tuliyofanya pale, alitupokea kwa msafara mkubwa sana wa bodaboda, maafisa usafirishaji; wanampenda sana Mheshimiwa Kingu pale Ikungi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge usiwe na wasiwasi, ondoa shaka, tutapanga kadiri muda unavyoruhusu mimi na wewe twende tukawaone Wanaikungi na kuchagiza hatua mbalimbali za maendeleo katika halmashauri hii. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, swali la nyongeza.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kata ya Mashewa ina kituo cha afya cha kimkakati kinachohudumia Kata ya Kalalani, Kata ya Kizara, Kata ya Foroforo, pamoja na Kata ya Mashewa yenyewe, lakini Serikali imetoa shilingi milioni 250 tu, kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kata ya Mashewa na miundombinu ya awali imekamilika. Ni lini Serikali itatoa fedha nyingine, kwa ajili ya ujenzi wa majengo mengine, ili kituo hiki kikamilike, kiweze kutoa huduma kwa ukamilifu wake, kama kituo cha afya? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mnzava kwa kuuliza swali dogo la nyongeza. Ni kweli, tumetenga fedha hizi za kujenga vituo vya afya vya kimkakati, vile 120, katika majimbo 120. Shilingi milioni 250 haitoshi kukamilisha miundombinu yote katika ujenzi wa vituo vya afya, lakini wazo la awali ilikuwa ni kuhakikisha kwamba, vituo hivi vinaanza kutoa huduma zile za *OPD* na za misingi, ambazo wananchi wetu wanaweza kuzipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Wabunge wengine katika Bunge lako la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tutaendelea kutenga fedha kuhakikisha kwamba, tunakamilisha vituo hivi pamoja na yale majimbo mengine, ambayo bado kabisa hatujatengea fedha. Tayari tumewasilisha maombi Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba, tunakamilisha kujenga katika majimbo yale 94, pamoja na kuongeza miundombinu katika vituo vile vya afya vya kimkakati, ambavyo vilitengewa shilingi milioni 250.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ziko halmashauri ambazo zina *muscles,* wao tayari wameanza kukamilisha baadhi ya miundombinu katika vituo vyao vya afya. Waendelee kufanya hivyo, ili kuhakikisha kwamba, tunavyoendelea kuleta fedha huku chini zile halmashauri ambazo zinajikongoja tunaendelea kuziongezea fedha, tuweze kukamilisha miundombinu hii. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Jafar Rajab, Naibu Waziri – TAMISEMI, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba twende kwenye Swali Namba 47. Sasa ninamwita Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 47

Kuwepo Somo la Historia ya Nchi Yetu
Kuanzia Elimu ya Msingi

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha somo la historia ya nchi yetu kuanzia elimu ya msingi, ili kizazi kijacho kiwe na uzalendo?

MWENYEKITI: Majibu, Naibu Waziri Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Wanu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ninaomba kujibu swali namba 47 la Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kuwa, Serikali imefanya maboresho ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, pamoja na Mitaala, ili kuhakikisha Taifa linazalisha rasilimali watu wenye maarifa, ujuzi, weledi na maadili yanayohitajika kwa maendeleo ya Taifa. Hivyo, maudhui ya historia ya nchi yetu yamewekwa katika Somo la Historia ya Tanzania na Maadili, linalofundishwa kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha sita, pamoja na vyuo vya ualimu. Maudhui ya somo hili yamelenga kumjengea mwanafunzi uelewa kuhusu historia, utamaduni, mila, desturi na maadili ya Taifa na hivyo, kumkuza kuwa Mtanzania mwenye uzalendo, uwajibikaji na utayari wa kulitumikia Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, somo hilo linafundishwa kwa lugha ya kiswahili kwa kuzingatia nafasi na historia ya lugha hii katika Taifa letu. Aidha, pamoja na hatua hizo masuala ya uzalendo, maadili, uwajibikaji na utambulisho wa Taifa yamejumuishwa pia, katika masomo mengine katika ngazi mbalimbali za elimu, ikiwemo kiswahili, kingereza na sayansi. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, swali la nyongeza.

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa ninaishukuru na kuipongeza Serikali yetu kupitia Wizara ya Elimu kwa namna ambavyo wanaendelea kuboresha mfumo wa elimu Tanzania. Hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile wanafunzi wa vyuo vikuu vyote nchini, ukiacha mbali wale wa vyuo vya ualimu, ndio

wanaenda kujenga mustakabali wa vijana, ambao wanaenda kutoa maamuzi yenye mustakabali mzima wa Taifa letu. Je, Serikali haioni umuhimu kwamba, hata hivyo vyuo vingine ambavyo siyo vya ualimu, somo hili liende huko likasomeshwe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Huwezi kutaja historia ya Tanzania bila kuutaja Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, pamoja na Waasisi wake. Je, Serikali ama Wizara ya Elimu imejipangaje kuhakikisha kwamba, somo la Muungano wa Tanganyika na Zanzibar linawafikia watoto wote kuanzia shule ya msingi mpaka vijana walioko vyuo vikuu? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimjibu Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, maswali yake mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza kwa kusimamia masuala ya maadili, lakini pia, kuona kwamba, muungano wetu unazidi kuimarika katika nchi yetu. Swali lake namba moja, kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi kwamba, Serikali imefanya maboresho ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 na Mitaala yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Serikali imeendelea kusimamia mageuzi hayo na kuhakikisha kwamba, elimu inayotolewa inawanufaisha wanafunzi wetu na kuwajenga katika maarifa, ujuzi, weledi na kuhakikisha kwamba, elimu inayotolewa inakuwa ni ya kiwango kile ambacho ameshauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake kwamba hatuoni umuhimu wa ku-*extend* programu hii ya kusomesha historia ya nchi yetu katika vyuo vingine, ninamwambia Mheshimiwa Mbunge, Serikali inaendelea kuliangalia. Ninamhakikishia kwamba, ushauri ambao ameutoa tumeuchukua na tutaangalia ni namna gani bora,

ambayo tutaweza kufundisha programu hizi katika vyuo mbalimbali, ili kuwafikia wanafunzi wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kwamba, hatuwezi kuzungumzia historia ya nchi hii bila kuzungumzia Muungano, ninakubaliana naye. Ni kweli, hatuwezi kuzungumza historia ya nchi yetu hii bila kuzungumzia suala la Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwamba tunawezaje…! *Sorry,* ninaomba a-*repeat* swali la (b).

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu imejipangaje kuhakikisha kwamba, elimu ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar inapatikana kwa vijana wetu kuanzia wadogo mpaka vijana wa vyuo vikuu?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, Wizara ya Elimu pamoja na Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano zinaendeleza programu maalum inayoitwa Muungono *Caravan,* ambayo inafundishwa ama inatolewa katika nchi nzima katika kada tofauti tofauti, ikiwemo kada ya vyuo na shule. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Najma kwamba, Serikali iko imara katika suala la muungano na itaendelea kuhakikisha kwamba, kila mwananchi anafikiwa na anafahamu nini maana ya muungano na wapi nchi yetu imetoka na wapi tunataka kuelekea. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Wanu Hafidh, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, sasa ni Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ninamwita Mheshimiwa Mdowe Haji Kombo, Mbunge wa Nungwi, aulize swali lake.

Na. 41

Ushirikishwaji wa Vijana Katika Upangaji wa Miji ya Kisasa

MHE. MDOWE HAJI KOMBO aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha vijana wanashirikishwa na kuwa sehemu ya upangaji miji ya kisasa?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mdowe Haji Kombo, Mbunge wa Nungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua vijana ni kundi muhimu katika ujenzi wa miji ya kisasa, miji jumuishi na endelevu. Serikali imeweka misingi ya kisera na kisheria, kupitia Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, Toleo la 2023, Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000 na Sheria ya Mipango Miji, Sura ya 355, inayosisitiza upangaji shirikishi, matumizi endelevu ya ardhi na ushirikishwaji wa wadau wote katika maendeleo ya miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia matakwa hayo ya kisera na kisheria Serikali itaendelea kushirikisha makundi yote ya wadau wa uendelezaji wa miji, ikiwa ni pamoja na kundi la vijana ambalo ni muhimu katika kuchangia usanifu wa miji nchini. Ushiriki wa vijana ambao ni takribani asilimia 35 ya idadi ya watu nchini umekuwa ni nguzo muhimu katika upangaji miji ya kisasa na hivyo, kuwa na miji stahimilivu, jumuishi, salama na endelevu, ikiwa ni utekelezaji wa Lengo la Maendeleo Endelevu Na. 11 na Ajenda Mpya ya Miji ya Mwaka 2016 – 2036. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mdowe Haji Kombo, swali la nyongeza.

MHE. MDOWE HAJI KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninaendelea kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri, ambayo ametupatia hapa, lakini pia, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujua, Serikali ina mpango gani mahususi wa kuhakikisha mipango ya miji inatenga na kulinda maeneo yatakayowezesha vijana kupata fursa za biashara, kilimo na uwekezaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali namba mbili; je, Serikali iko tayari kufanya tathmini maalum ya ushiriki wa vijana katika upangaji wa miji na kuweka utaratibu wa kuhakikisha maoni yao yanaingizwa kwenye mipango ya maendeleo ya miji? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninakushukuru sana Mheshimiwa Mdowe na kukupongeza kwa sababu, umekuwa na vijana, unawawakilisha vijana na kuwatetea na kuangalia hatima yao katika uwekezaji ambao kimsingi ndiyo dira ilivyosema ya mwaka 2050. Kuwa, vijana ni kundi ambalo linalochochea uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejipanga na inaendelea kutekeleza mpango wake wa kuwahusisha vijana katika sekta zote. Kama tunavyofahamu, sekta yetu ya ardhi ni wezeshi, tunashirikiana na sekta zote za uzalishaji, ikiwemo viwanda na biashara, kilimo na sekta nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu nikuhakikishie, Wizara ya Viwanda na Biashara na pia, Wizara ya Uwekezaji pamoja na Mipango, imeweka mipango mikakati kwa kushirikiana na Wizara ya

Ardhi kwa kutenga maeneo maalum katika ngazi ya Kitaifa, ambayo ni *special economic zone*. Pia, katika kila halmashauri tuna kongani, ambapo katika kongani hizo tumewaangalia vijana nao waweze kupata fursa, ili waweze kuwekeza. Hivyo natoa wito kwa vijana tutumie fursa hii kutembelea kongani hizo na kushirikiana na halmashauri kutumia fursa katika uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu tathmini. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, si tathmini tu, sisi tunaendelea na utekelezaji kwa sababu, mipango yetu imejionesha wazi kabisa. Takribani 35% ya wananchi wote Tanzania hapa ni vijana kwa hiyo, tathmini ya kwanza ni kujua umuhimu wa vijana kwa sababu, wako wengi katika maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, katika ushirikishwaji wa upangaji. Tayari tumeanza kuwahusisha kisera na kisheria ndiyomaana tumeweza hata kutenga maeneo haya. Leo hii hata ukimuuliza Waziri wa Mifugo atakuambia kuna mpango wa ekari zaidi ya milioni sita ifikapo 2030 ambapo vijana hao watakuwa wanahusishwa katika kutumia fursa hizo. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Ninaomba niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe ambao ni wa Kamati ya Uongozi, mnatakiwa kwenye kikao, Ofisi ya Spika, sasa hivi.

Tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele, Mbunge wa Mafinga, aweze kuuliza swali lake.

Na. 42

Kupima Ardhi kwa Bei Nafuu

MHE. DICKSON N. LUTEVELE aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanzisha utaratibu wa kupima ardhi kwa bei nafuu kwa wananchi wa Kata za Isalavanu, Bumilayinga, Rungemba na *Sao Hill?*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele, Mbunge wa Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za upimaji ardhi kwa maeneo ambayo yameendelezwa hutozwa kwa kuzingatia Mwongozo wa Urasimishaji wa Mwaka 2021. Kwa mujibu wa mwongozo huo, gharama za kupanga na kupima kiwanja kimoja ni shilingi 130,000. Kabla ya hatua za Serikali kupunguza gharama hizi, wananchi walikuwa wanalipa kati ya shilingi 250,000 hadi shilingi 400,000, kwa ajili ya upangaji na upimaji wa kiwanja kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa upimaji wa kawaida usiohusisha urasimishaji, gharama za upimaji zinatozwa kupitia Mwongozo wa Ukadiriaji wa Bei za Viwanja wa Mwaka 2016, ambao umeweka vigezo vya gharama za upimaji kwa kutegemea umbali eneo lilipo, ukubwa wa eneo linalopimwa, umbali kutoka alama za msingi, idadi ya vifaa vya kufanyia kazi na gharama za alama za mipaka *(beacons)* ambazo zinazohitajika. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele, swali la nyongeza.

MHE. DICKSON N. LUTEVELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa ninaipongeza Serikali kwa mpango huu ambao jimboni kwangu Mafinga umeanza. Kusema ukweli, umewavutia sana wananchi wengi kwa sababu, kabla ya Serikali kuachia upimaji huu kwa gharama ndogo wananchi walikuwa wanapata shida sana kupata gharama za upimaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu. Kwa kuwa, mpango huu umeivutia sana jamii na wananchi wengi wamehamasika, hasa wananchi wa maeneo ambayo upimaji haujafika, kwenye Kata zangu za Isalavanu, Bumilayinga, Rungemba, *Sao Hill* na Changalawe. Je, Serikali haioni kuwa, ipo haja ya kuongeza kasi ya upimaji kwa sababu, sasahivi kasi ni ndogo sana, ili wananchi wa kata hizi nilizozitaja waweze kufikiwa kupata huduma hii na upimaji ufanyike? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Dickson Lutevele, Mbunge wa Mafinga Mjini. Ninaomba kwanza kukiri kuwa, vijiji ambavyo wamevitaja vya Salavanu, Bumilayinga, Rungemba na *Sao Hill* mimi ninavifahamu na nimeshawahi kuvitembelea katika nafasi mbalimbali. Ni vijiji ambavyo viko pembezoni mwa Mji wa Mafinga na hili hitaji la kupimwa kweli, bado lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, ninaomba nimhakikishie tutaendelea kuongea na Mkurugenzi wa Mafinga, ili tuweze kupanga muda na jinsi ya kwenda kutekeleza upimaji wa vijiji hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, mahitaji haya ya upimaji mara nyingi yanatolewa na Mkurugenzi katika eneo husika na sisi tunashirikiana naye, ili kuweza kufikia maeneo ambayo yana uhitaji wa haraka. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Boniphace Getere, swali la nyongeza.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Hivi karibuni tumekuwa na mgogoro mkubwa kati ya wafugaji na wakulima katika Jimbo la Bunda, Kijiji cha Sarakwa, ambacho kina wafugaji karibu 90%; wameamua kutengeneza

blocks zao kwenye maeneo yao ya kuchungia. Sasa ni lini Serikali itaenda kwenye eneo hilo kuwapimia wale wafugaji maeneo yao, ili kupunguza mgogoro wa wafugaji na wakulima?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakiri kufanya mazungumzo na Mheshimiwa Boniphace kuhusu maeneo aliyoyataja katika eneo lake la Bunda. Ni ukweli ambao haupingiki kuwa, Bunge hili limefanya kazi kubwa ya kuiwezesha Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kutenga fedha zaidi ya shilingi bilioni 35, ambayo kimsingi, fedha hizi zitaenda kumalizia maeneo yote ya vijijini, ambayo hayajapangwa na kupimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upimaji huu tunashirikisha sana wananchi wa maeneo husika, ili waweze kutambua shughuli za kiuchumi ambazo zinafanyika katika maeneo yao, ili waweze kutenga maeneo. Hivyo, ninamwomba Mheshimiwa Boniphace kwa ushirikiano na Mkurugenzi na wenyeviti wa vijiji wawe tayari kuonesha maeneo ya mifugo, ili tukienda kupanga iwe rahisi kujua ni kiwango gani cha ardhi kitatengwa katika maeneo yao kulingana na idadi ya mifugo, ambayo ipo katika eneo hilo. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kaspar Muya, Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Sasa ninamwita Mheshimiwa Patrick Mwalunenge, Mbunge wa Mbeya Mjini, aulize swali lake; kwa niaba, Mheshimiwa Baraka Mwamengo.

Na. 43

Ujenzi wa Baraara ya Tanzam Kutoka Igawa – Mbeya Mjini – Tunduma

MHE. BARAKA A. U. MWAMENGO K.n.y. MHE. PATRICK A. MWALUNENGE aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya *TANZAM* kutoka Igawa hadi Mbeya Mjini kuunganisha Mbeya Mjini hadi Tunduma, pamoja na *Bypass* utaanza?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Patrick Adkin Mwalunenge, Mbunge wa Mbeya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Barabara ya Igawa – Songwe – Tunduma, yenye urefu wa kilometa 218, pamoja na njia ya mchepuko ya Uyole – Songwe, yenye urefu wa kilometa 48.9 unatekelezwa kwa utaratibu wa ubia wa Serikali na Sekta Binafsi *(PPP)*. Kwa sasa, mwekezaji wa mradi huo anaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu ambao unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Novemba, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za ujenzi wa barabara hii zitaanza baada ya kukamilika majadiliano kati ya Serikali na mwekezaji. Aidha, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* inaendelea na ujenzi wa barabara ya njia nne kuanzia Nsalanga – Ifisi, yenye urefu wa kilometa 29, ambayo ni sehemu ya barabara hiyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Baraka Mwamwengo, swali la nyongeza.

MHE. BARAKA A. U. MWAMENGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri. Ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kwa niaba ya Mbunge wa Mbeya Mjini. Eneo la *bypass* ile ya pale Mbeya Mjini ni muhimu kwa bandari yetu na kwa maendeleo ya nchi yetu kwa sababu, inaongeza ubebaji wa mizigo. Ni lini sasa barabara ile itakamilika kwa kile kipande cha *bypass*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa Iringa alitoa tamko la kuwa, mikataba mipya haitaanzishwa, badala yake ataendeleza ile ambayo iko tayari, ambayo hatua za manunuzi zimekamilika; Barabara ya Ibanda – Kajunjumele hatua ya manunuzi imekamilika. Ni lini sasa mkataba ule utasainiwa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya *Bypass* ya Mbeya ni sehemu ya hiyo barabara kuu ya kutoka Igawa – Mbeya – Songwe hadi Tunduma na ndiyo inayofanya ziwe hizo kilometa 218. Kwa hiyo, itajengwa wakati huo baada ya huyo mbia kuwa amekamilisha tathmini na Serikali kukubaliananaye; kwa hiyo, ni sehemu ya hiyo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, hata fidia ya hicho kipande ambacho ni barabara tayari tumewalipa wananchi, ikiwa inasubiri tu kukamilika. Hata hivyo, tumemwelekeza Meneja wa Mkoa pale anapopata hela kidogo aendelee kuifungua, ili wale watakaohitaji kuitumia waitumie, lakini tukiwa tunasubiri kuijenga kwa njia nne. Kwa hiyo, mpango huo upo na unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Barabara ya Ibanda – Kajunjumele, tulikuwa tumepata mkandarasi, lakini akasimama, tunavyoongea hivi tumempata mkandarasi mwingine, tunachosubiri ni kupata siku ya kusaini na, kama tulivyosema, ni moja ya barabara ambazo tumeanza kupokea fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, itakuwa ni moja ya barabara ambazo tutasaini muda si mrefu, hasa baada ya kupata fedha kwa sababu, ni barabara ambayo kimsingi ilitakiwa iwe inaendelea, lakini tukashindwana na mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni barabara ambayo inapewa kipaumbele kikubwa sana katika kipindi hiki cha utekelezaji, hasa wa mwaka huu wa fedha. Tuna hakika tutaanza kuijenga kwa kiwango cha lami.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba turuhusu swali la maliasili, halafu utarejea kumaliza maswali. Tafadhali ukae.

Sasa ni Wizara ya Maliasili na Utalii. Ninamwita Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly, Mbunge wa Lindi, aulize swali lake.

Na. 54

Kuendeleza Vivutio vya Utalii Lindi Mjini

MHE. MOHAMED M. UTALY aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza vivutio vya utalii vilivyopo Lindi Mjini, ili kuongeza mapato na ajira kwa wananchi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Mussa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea kusimamia na kutekeleza Sera ya Taifa ya Utalii ya Mwaka 1999, ambayo imetilia mkazo suala la kutanua wigo wa mazao ya utalii nchini kwa

kubainisha vivutio na mazao ya utalii, kuyaweka katika mpango wa uendelezaji na utangazaji, ambapo katika mwaka wa fedha 2024/2025 lilifanyika zoezi la kubaini vivutio vya utalii katika mikoa 10 ikiwemo Lindi. Kwa upande wa Mkoa wa Lindi, mazao na vivutio vya utalii vilivyobainishwa ni pamoja na maeneo ya kihistoria, malikale, utamaduni na fukwe za bahari zenye fursa za kukuza utalii kupitia uwekezaji wa huduma na shughuli mbalimbali za utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kutoka sekta za umma na binafsi, ikiwa ni pamoja na mamlaka zilizopo Lindi kuhakikisha vivutio vilivyopo mkoani humo vinaendelezwa. Aidha, Wizara kupitia Bodi ya Utalii Tanzania itaendelea kuimarisha mikakati ya kutangaza na kuvifikisha sokoni vivutio vya Lindi kwa kutumia majukwaa ya kidijitali, mitandao ya kijamii, maonesho ya utalii na kampeni mbalimbali za masoko ndani na nje ya nchi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly, swali la nyongeza.

MHE. MOHAMED M. UTALY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri na ninaipongeza Serikali kwa kazi kubwa iliyoifanya ya kubainisha mazao ya utalii katika Mji wa Lindi. Maswali yangu ya nyongeza mawili ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kuwa, kwa kitendo cha kubainisha vivutio hivyo vya utalii tangu mwaka wa fedha 2024/2025 na mwaka wa fedha uliofuata 2025/2026, kutofanyika chochote katika uendelezaji wa vivutio hivyo ni kuwanyima Vijana wa Lindi fursa ya ajira na kuikosesha Serikali mapato, ambayo yangeweza kupatikana kutokana na utalii katika vivutio hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, katika mwaka huu wa fedha 2026/2027 ni vivutio vipi hasa vya utalii, katika Manispaa ya Lindi, vipo katika mpango huu wa kuendelezwa? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mohamed Mussa, lakini kabla ya kujibu ninaomba nimpongeze sana kwa maswali yake mazuri yenye kujenga. Ninaomba uniruhusu nianze kujibu swali la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivutio ambavyo vimebainishwa kule Mkoani Lindi ni pamoja na fukwe za Lindi Mjini, Kilwa, pamoja na sehemu za kihistoria. Maeneo ya kihistoria ya Vita vya Majimaji, kama kule Nandete pamoja na Tendaguru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili. Serikali imefanya jitihada mbalimbali baada ya kubaini vivutio hivyo, ikiwa ni pamoja na kuviweka kwenye mpango wa mwaka huu 2026/2027. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na mamlaka mbalimbali za Serikali za Mitaa, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kule Lindi, pamoja na wadau wengine, ili kuendeleza vivutio hivyo kwa pamoja. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hamad Chande, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa, tunarejea kwenye mtiririko wa maswali yetu; tulikuwa Wizara ya Ujenzi. Sasa ninamwita Mheshimiwa Bazilio Kapunda Mbwilo, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, aulize swali lake.

Na. 44

Ujenzi wa Barabara ya Namanyere – Kipili

MHE. BAZILIO K. MBWILO aliuliza:-

Je, lini Barabara ya Namanyere – Kipili, Nkasi Kaskazini, itajengwa kwa kiwango cha lami?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Bazilio Mbwilo Kapunda, Mbunge wa Nkasi kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Namanyere – Kipili ni sehemu ya Barabara ya Msangama – Namanyere – Katongoro – *New Kipili Port,* yenye urefu wa kilometa 64.8. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mradi huu umeingizwa katika mpango wa bajeti, kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami kwa kuanza na sehemu ya Namanyere – *Mfili II Bridge* yenye urefu wa kilometa 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa, Serikali inaendelea kutafuta fedha, kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bazilio Kapunda Mbwilo, swali la nyongeza.

MHE. BAZILIO K. MBWILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaishukuru Serikali kwamba, sasa barabara hii imefikia hatua nzuri. Kwa kuwa, barabara hii ni muhimu sana, hasa kwa mapato ya Serikali, kutokana na mizigo mingi inayokwenda nje ya nchi inapitia Bandari ya Kipili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kitu kimoja katika hizo kilometa 20 au hata ikibidi, pungufu ya hizo zianzie bandarini kwenyewe kwa ajili ya yale malori yanapokuja na mizigo; kwa sasahivi yanahangaika sana kuingia pale bandarini, lakini lami

ikianzia bandarini hata kilometa mbili tunaweza kuwa tumevutia wasafirishaji wengi kuendelea kuitumia Bandari hiyo ya Kipili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kama Bandari ya Kipili ilivyo muhimu kwa uchumi wa nchi hii, Bandari ya Kabwe nayo ni hivyohivyo. Ninamuomba Mheshimiwa Waziri, walau kilometa moja tu tuijenge, ianzie bandarini, ili kuwezesha magari baada ya mihangaiko huko mbugani kwenye matope mengi yanapoingia kwenye gati yaweze kupita kirahisi. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninaomba nijibu maswali mawili ya nyongeza, kwa pamoja, ya Mheshimiwa Mbunge wa Nkasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakiri kupokea ombi lake, lakini pia, namweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba, pamoja na kupokea huo ushauri, lakini lengo letu hasa ni kuhakikisha zile barabara zinapitika na tunajua barabara zinazotoka bandarini zinakuwa ni zenye uzito mkubwa. Kwa hiyo, pamoja na kupokea ushauri, lakini tutakachoshauriana na wataalamu ni hasa yale maeneo ambayo yanaweza kuwa ni kikwazo kwa magari kupita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linaweza likatoka bandarini, lakini kama litakwama Katikati, hata kama tutakuwa tumeweka lami mwanzoni itakuwa haina maana. Cha msingi ninadhani tutaangalia yale maeneo korofi, ambayo yanaweza yakafanya barabara isipitike tufanye hasa kwa maombi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Kabwe tumeanza kufanya hivyo, maeneo yenye madaraja membamba na kwa maeneo korofi, tumetoa maelekezo yatengenezwe, ili magari yaweze kupita. Kwa hiyo, tutashauriana, lakini pia, wataalamu watashauri nini cha kufanya, hasa kulingana na ombi lako. Ahsante sana.

SMWENYEKITI: Mheshimiwa Arif Premji, swali la nyongeza.

MHE. ARIF S. PREMJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuzingatia Kanuni ya 56(1) ya Kanuni zetu za Bunge, kwa kuzingatia Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi ya 2025 – 2030, ujenzi wa barabara ya Ziwani kwenda Kilambo na kwa kuzingatia ripoti ya *BOT* ya mwezi Julai ambayo inaonesha makusanyo ya fedha yamevuka malengo. Je, lini ujenzi wa barabara ya Ziwani kwenda Kilambo utaanza? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba moja, sisi kama Wizara tayari tumeshatenga hata fedha ya kuanzia kufanya upembuzi yakinifu na usanifu kwa lile daraja la Kilambo. Pia, ni mpango kwamba hiyo barabara tumeitengea fedha ya kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tulivyosema katika bajeti, kipaumbele kwanza kwa sasa ni ile miradi ambayo imesimama lakini pamoja na hiyo miradi ambayo tumeipangia fedha, tuna hakika kwamba ndiyo tunaanza utekelezaji wa bajeti na hasa kwa Ilani yetu ya miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika kwa umuhimu wa barabara hiyo, nayo itakuwa ni kati ya barabara ambazo katika kipindi hiki zitaanza kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaipongeza Serikali kwamba Makete tuliomba barabara mbili zipandishwe hadhi, barabara ya Ikuwo – Nkenja mmeipandisha hadhi kwenda *TANROADS* na inaendelea kujengwa. Pia kuna barabara kutoka Lupila – Kipengere ni barabara ambayo inawasumbua sana wananchi wa eneo la Lupila na eneo la Ipepo.

Ni lini Serikali itatoa fedha ili barabara hii ianze kujengwa kwa kiwango cha changarawe, kwa sababu tayari iko kwenye mikono ya *TANROADS* kutoka mwaka 2024?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba barabara hiyo ya Lupila – Kipengere imeshapandishwa hadhi tangu 2024 na mara tu baada ya kupandishwa hadhi, *TANROADS* cha kwanza ilianza kuiweka katika hadhi ya barabara za *TANROADS* kwa sababu viwango vya barabara za *TARURA* na *TANROADS* vinatofautiana pakubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachofanya sasa hivi ni kuhakikisha inapitika na hata katika mwaka huu wa fedha, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, hiyo barabara tutaendelea kuikarabati na imetengewa fedha ili iweze kukarabatiwa, kwa sababu ndiyo kwanza ilikuwa katika hadhi ya *TARURA*, Meneja ameelekezwa kwanza ahakikishe kwamba maeneo yale ambayo ni korofi ndiyo hasa yanatengenezwa kuhakikisha kwamba inapitika wakati sasa anaiweka katika viwango vya barabara ya *TANROADS*, hiyo barabara ambayo ina takribani kilometa 50. Kwa hiyo ninamhakikishia, tayari tunayo na tumeshaanza kupata bajeti yake, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, swali la nyongeza.

MHE. JACQUELINE K. N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Ninaomba niulize swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilometa 124 kwa kiwango cha lami kutoka Songea Mjini eneo la Likuyufusi kwenda Mkenda, mpakani mwa Tanzania na Mozambique? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Songea hasa kutokea Likuyufusi kwenda Daraja la Mkenda mpakani na Msumbiji tutaanza kuijenga kwa awamu. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tuna mkandarasi, huyu mkandarasi anasubiri alipwe *advance* na ndiyo barabara ambazo tulikuwa tunasema tutaanza kuzijenga ikiwa ni pamoja na hiyo barabara. Kwa hiyo, tutaanza Likuyufusi hadi eneo linaloitwa Muhukuru kwa kilometa 60. Kwa hiyo, sasa hivi muda siyo mrefu sana tumeshaanza kupokea fedha, tutamlipa fedha ya awali ili mkandarasi aende *site* kwa sababu tayari yupo. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naomy Mwaipopo, swali la nyongeza.

MHE. NAOMY D. MWAIPOPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Uvinza – Lukoma yenye kilometa 38 kuelekea lango la *Mahale National Park* ni mbovu sana. Ni nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba barabara hii inajengwa ili kuchochea watalii kwenda kwenye *National Park ya* Mahale*?* Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba arudie. Nimemsikia tu kuanzia Uvinza, sijasikia kwenda wapi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naomi.

MHE. NAOMY D. MWAIPOPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Uvinza – Lukoma mpaka kwenye lango la Mahale *National Park* yenye kilometa 38 ni mbovu na haipitiki hasa kipindi cha mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nini mpango wa Serikali kuhakikisha barabara hii inajengwa ili kuchochea uchumi wa utalii pale Uvinza? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue swali la Mheshimiwa Mbunge na tutasaidiana na wenzetu wa *TARURA* kuhakikisha kwamba hii barabara kwa kweli kwa sababu inaenda kwenye mbuga muhimu ya utalii inakarabatiwa na inapitika kipindi chote cha mwaka, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, sasa namwita Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka, Mbunge wa Nachingwea, aulize swali lake.

Na. 45

Huduma za Fedha Kupitia Mitandao ya Simu – Nachingwea

MHE. FADHILI A. LIWAKA aliuliza:-

Je, lini huduma za fedha kupitia mitandao ya simu zitapelekwa kwa wananchi Kilimarondo na Kiegei ambao hufuata huduma hiyo umbali wa kilometa 120?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka, Mbunge wa Nachingwea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtandao wa simu za mkononi ni muhimu kupatikana kabla ya kupata huduma za pesa mtandao ili

kuwezesha mawasiliano kati ya simu ya mtumiaji na mfumo wa huduma za kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia miradi ya *UCSAF* tayari imejenga minara miwili ya *TTCL* inayotoa huduma za mawasiliano. Mnara mmoja unatoa huduma katika Kijiji cha Nanjihi, Kata ya Kilimarondo na mwingine upo katika Kijiji cha Kiegei, Kata ya Kiegei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa *TTCL* inayo huduma ya pesa mtandao kupitia T-PESA, nimemuelekeza Mkurugenzi Mkuu wa *TTCL* kuhakikisha mawakala wa pesa mtandao wa T-PESA wanakuwepo katika vijiji vya Kilimarondo na Kiegei ili waweze kutoa huduma za kifedha kupitia mtandao wa simu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote itafanya tathmini ya hali ya mawasiliano katika maeneo hayo ili kuona changamoto zilizopo ikiwemo upatikanaji wa kampuni nyingine za watoa huduma za mawasiliano katika maeneo hayo. Hii itawezesha kuchukua hatua stahiki ikiwemo kuhamasisha kampuni nyingine za mawasiliano ya simu kutumia minara iliyowekwa kusimika mitambo yao ili kuwezesha wananchi kupata mawasiliano ya simu na huduma za fedha kutoka mitandao hiyo pia.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka, swali la nyongeza.

MHE. FADHILI A. LIWAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na majibu mazuri na ya kutia moyo ya Serikali, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Kwa kuwa maeneo ya Kiegei na Kilimarondo yamekuwa na mwamko mkubwa wa uzalishaji wa madini, hususan madini ya dhahabu na kumekuwa na mwingiliano mkubwa wa watu na uhitaji wa huduma za kifedha na kufanya miamala mbalimbali ya simu. Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kushawishi na kusukuma kampuni mbalimbali za simu

za mkononi ili ziweze kwenda kujenga minara na kuwezesha huduma hizi muhimu za upatikanaji wa fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa majibu na jitihada hizi za kuhakikisha kwamba tunapata mawasiliano yenye huduma za kifedha ni za muda mrefu. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ana utayari wa kuongozana na mimi japo kwenda kutembelea kwa siku nzima ili ajionee mazingira ya mawasiliano na masuala ya miamala katika maeneo ya Kilimarondo na Kiegei? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninaanza kwa kumpongeza, Mheshimiwa Liwaka amekuwa mfuatiliaji mzuri wa huduma hizi za kidijitali katika Jimbo lake na ni msumbufu kwelikweli. Amekuja Wizarani zaidi ya mara kumi, kwenye simu yangu nina meseji zake zaidi ya 30 na watu wasiomfahamu kama ni Mheshimiwa Mbunge wanaweza kudhani kwamba ni mtumishi wa Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninampongeza sana kwa kuwapigania wananchi wake. Hakika wananchi wa Nachingwea wamepata Mbunge jembe, jembe ulaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kujibu swali la pili kuhusu kutembelea Jimbo la Mheshimiwa Liwaka. Ninamhakikishia Mheshimiwa Liwaka kwamba niko tayari, baada ya Bunge hili, tutapanga mimi na yeye ni lini nitakwenda kutembelea ili nikajionee hali halisi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la kwanza, Wizara yetu inaendelea na mazungumzo na watoa huduma mbalimbali ili kuhakikisha kwamba wanafikisha huduma katika eneo hilo kwa sababu amesema ni eneo la uzalishaji na lina mwingiliano mkubwa wa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa eneo hili, ninamwelekeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano kupitia taasisi zake kuratibu haya mashauriano yanayoendelea na watoa huduma ili kuhakikisha kwamba wanapeleka huduma za minara katika eneo alilolitaja Mheshimiwa Liwaka la Kiegei mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kwamba Dira yetu ya 2050 inaitaka sekta binafsi iwe mstari wa mbele katika kuleta maendeleo ya nchi yetu na sisi hilo tumelizingatia, tunawasiliana na watoa huduma wetu ili kutekeleza pia dira yetu hii. Ninakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Dunia iko kiganjani, huwezi ukapata fursa mbalimbali kama hauna mawasiliano, huwezi ukafanya huduma za kipesa kama hauna mawasiliano. Mheshimiwa Naibu Waziri ulikuja Bunda, hukuamini kama Jimbo la Bunda Mjini kuna maeneo hakuna mawasiliano, nikakupeleka Kabasa, nikakupeleka Guta, nikakupeleka Wariku, nikakupeleka Sazira, nikakupeleka Mcharo, nikakupeleka Bunda Stoo, Mgaya Ngogo hakuna mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini sasa ahadi yako uliyosema utatujengea minara ili wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini wapate mawasiliano na waweze kufanya huduma mbalimbali za kifedha kupitia mawasiliano itatimia? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Bunda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nilikuwa Jimboni kwake, ni Mbunge imara kabisa, alinipokea vizuri, tulitembelea maeneo yote

aliyoyataja. Hakika Bunda wana Mbunge imara, Mbunge mchapazi, bado kijana, wanaweza kumuongeza miaka mingine 10. Hata hivyo, ninamhakikishia kwamba tutajenga minara katika Jimbo lake mwaka huu wa fedha ulioanza. Kwa hiyo, awe na amani, akawaambie wapigakura wake kwamba minara inakuja katika mwaka huu wa fedha. *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Switbert Mkama, Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Sasa namwita Mheshimiwa Lucy Simirya Kombani, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 46

Ulinzi wa Watoto Dhidi ya Ukatili wa Mtandaoni

MHE. LUCY D. S. KOMBANI aliuliza:-

Je, hatua gani zinachukuliwa kuwalinda watoto dhidi ya ukatili mitandaoni kutokana na ongezeko la matumizi ya mitandao ya kijamii.?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuchukua hatua za kuhakikisha watoto wananufaika na teknolojia huku wakilindwa dhidi ya ukatili, unyanyasaji, unyonyaji na madhara mengine ya kidijitali ambapo, miongoni mwa hatua hizo zinazotekelezwa ni kampeni ya kitaifa ya ulinzi na usalama wa mtoto mtandaoni, iliyofanyika katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara na iliyolenga kutoa elimu kwa wazazi, watoto, walezi na jamii kuhusu matumizi

salama na yenye uwajibikaji na yanayolinda haki za watoto mtandaoni. Kupitia kampeni hiyo, zaidi ya watoto 1,811,212 wamefikiwa na elimu kuhusu usalama wa mtoto mtandaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imeunda Kamati ya Kitaifa ya Ushauri kuhusu Ulinzi na Usalama wa Mtoto Mtandaoni yenye jukumu la kutoa ushauri wa kitaalamu na kusaidia kuweka mikakati na afua madhubuti za kuzuia na kukabiliana na vitendo vya ukatili na madhara yanayoweza kuwakabili watoto wanapotumia mifumo ya kidijitali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lucy Kombani, swali la nyongeza.

MHE. LUCY D. S. KOMBANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Wizara na nitauliza maswali mawili ya nyongeza. Kumekuwa na matumizi makubwa sana nchini ya akili mnemba. Je, Wizara ina utaratibu upi wa kujiridhisha kwamba teknolojia hii haitokuwa kisababishi cha ukatili wa mitandaoni kwa watoto wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kumekuwa na uingizwaji wa vifaa vya kielektroniki kama simu na *tablet* za watoto. Je, Wizara ina utaratibu upi wa kujihakikishia kwamba vifaa hivi havitaruhusu watoto hawa kupakua maudhui ambayo yatasababisha wao kupitia ukatili mtandaoni? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda sana kumpongeza Mheshimiwa Lucy Kombani kwa ufuatiliaji wake wa karibu sana na kuona kwamba Kamati anayoifanyia kazi anaitendea haki, amekuwa akiuliza maswali mengi na ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi makubwa ya akili mnemba na teknolojia yasije yakasababisha madhara kwa watoto. Awali ya

yote, ninapenda kusema kwanza maswali yake yote mawili moja kwa moja yanaingia kwenye Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Hivyo, ninapenda kusema nimeyapokea lakini sisi kama Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum tunafanya kazi na wizara nyingine ikiwemo Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jibu langu la msingi hapa kwenye *paragraph* ya mwisho nimesema kamati ya kitaifa imeshaundwa na katika kamati hii tuna wajumbe wanaotoka kwenye Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Hivyo, masuala mazima ya matumizi makubwa ya akili mnemba tayari tunaendelea kuyajadili kuona namna njema kwa umoja wetu kudhibiti; tusikimbie teknolojia, dunia tuliyopo lazima watoto waishi ndani ya teknolojia na wanafahamu zaidi hata ya sisi wazazi. Kwa hiyo, hatuwezi kuwaondoa huko zaidi ya kuona kwamba kamati hii iende kufanya zaidi na kuhakikisha watoto wetu wanabaki salama huku wakiwa wazuri katika teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninapenda kutoa wito wa malezi chanya kwa jamii, kila mzazi achukue jukumu la kuhakikisha anakuwa karibu na mtoto wake. Kifaa anachotumia mtoto wako umekinunua wewe, kama ni simu, kama ni *tablet*, umeinunua wewe, kwa hiyo pale unaponunua hakikisha *programs* ambazo mtoto anakwenda kuziangalia, kuzisoma, wewe mzazi uzifahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haijalishi umri, hata akiwa zaidi ya miaka 18 mpaka miaka 25 hivi, tujitahidi kama wazazi na walezi, kuwaangalia kwa karibu, wakati mwingine kuwafanyia *control*. Unamvamia tu mtoto unamwambia hebu lete hiyo simu, fungua *password,* angalia anacheza na maeneo gani. Unaweza ukakuta wewe mwenyewe kiongozi mtoto wako huko mitandaoni anashiriki katika kujidhulumu yeye mwenyewe, anatuma picha mbaya ambazo kesho hata akipewa uteuzi wowote zinakwenda kumpa shida. Kwa hiyo, tuendelee kufanya malezi ya pamoja kuhakikisha kwamba teknolojia haitupeleki pabaya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, sasa ninamwita Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo, aulize swali lake.

Na. 48

Ujenzi wa Jengo Jipya la Mahakama ya Mwanzo Urambo

MHE. MARGARET S. SITTA aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga jengo jipya la Mahakama ya Mwanzo Urambo kutokana na hali mbaya ya jengo lililopo sasa hasa kipindi cha mvua?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na Mahakama ya Tanzania imeendelea kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama kwa lengo la kuimarisha miundombinu ya utoaji haki katika ngazi mbalimbali. Mpango huu unahusisha ujenzi wa majengo mapya na ukarabati wa majengo yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ujenzi wa jengo la Mahakama ya Mwanzo Urambo umepangwa kutekelezwa kwa bajeti ya mwaka 2027/2028.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali la nyongeza.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaipongeza Serikali kwa majibu mazuri yaliyotolewa hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hali ya Mahakama ya Mwanzo Wilayani Urambo ni mbaya sana, kwanza ni kutokana na kujengwa wakati wa mkoloni, majengo yale au jengo lile limeezekwa kwa *asbestos*, sasa si rahisi sasa hivi kukuta majengo yaliyoezekwa kwa *asbestos* kwa sababu ni *material* iliyokuwa inatumika enzi za ukoloni zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya na hasa kipindi cha mvua jengo zima huwa linazungukwa na maji na nilishachukua picha zake kiasi ambacho wafanyakazi ndani ya jengo lile la Mahakama ya Mwanzo, wanapata shida hata kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali iko tayari na hasa Mheshimiwa aliyesimama na kujibu maswali, anaweza kupata nafasi ya kuja kujionea mwenyewe hali ngumu iliyoko katika Mahakama ya Mwanzo Wilayani Urambo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwanza kumpongeza Mheshimiwa Margaret Sitta kwa swali lake zuri, kwa sababu lengo hapa anataka kuona upatikanaji wa haki katika Jimbo lake unaendelea kuimarika kwa kuwa na miundombinu bora ya Mahakama ya Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kabisa Serikali ya Awamu ya Sita imefanya uwekezaji mkubwa kabisa wa kipekee na wa kimageuzi wa jumla ya shilingi bilioni 524.9 katika kipindi hiki tu cha miaka mitano, kwa ajili ya kuboresha miundombinu hii ya mahakama. Pia kufanya mapinduzi makubwa ya matumizi ya TEHAMA katika Muhimili wa Mahakama kwa ajili ya kuboresha huduma hizi za upatikanaji wa haki, kwa hakika hii ni *legacy* ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Margaret Sitta, kwamba katika mkakati huu, katika huu mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama, lengo ni kufika katika maeneo mbalimbali ya nchi, kuboresha miundombinu ya Mahakama ikiwemo Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie, kama nilivyojibu katika jibu la msingi kwamba katika mwaka wa fedha 2027/2028, jengo la Mahakama hii ya Mwanzo litajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipo tayari nikitoka hapa tutakaa na yeye, tutazungumza, tutapanga ratiba ili niweze kufika kama alivyotaka yeye Mheshimiwa Mbunge, kwenda kujionea hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali na Muhimili wa Mahakama unafahamu uhitaji, ndiyo maana tayari unaendelea kufikia maeneo mbalimbali kwa awamu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba miundombinu hii ya mahakama inajengwa kwenye maeneo ambayo yanahitaji ujenzi na inakarabatiwa kwenye maeneo ambayo ni chakavu. Kwa hiyo, kwa awamu tutakuja kufika pia katika Mahakama hii ya Mwanzo ya Urambo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inajengwa na inakuwa na ubora ambao utaboresha upatikanaji wa haki kwa wananchi. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zainab Katimba, Naibu Waziri, Katiba na Sheria tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, sasa ninamwita Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 49

Kuwapatia Maji ya Ziwa Victoria wananchi Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA aliuliza:-

Je, upi mpango wa kuwapatia maji ya Ziwa Victoria wananchi wa Kata za Lyamidati Ilola, Puni, Nyida, Itwangi na Usanda – Shinyanga?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kuwa inafikisha huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wote kwa kutumia vyanzo vya maji vya uhakika, vikijumuisha maziwa, mito na mabwawa. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali kupitia mradi wa maji ya Ziwa Victoria imekamilisha sehemu ya mradi unaolenga kuhudumia Kata Tisa Wilayani Shinyanga kwa kujenga matanki matatu yenye jumla ya ujazo wa lita 1,300,000; sanjari na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilometa 60 ambapo unanufaisha zaidi ya wakazi 15,198 waishio kwenye vijiji saba vya Kata za Didia, Tinde na Nsalala zilizopo Wilaya na Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na mpango wa kuongeza mtandao wa maji ili kuhakikisha kuwa maji ya mradi wa Ziwa Victoria yanafika kwenye vijiji 34 vinavyopatikana kwenye Kata Tisa za Lyamidati, Ilola, Puni, Nyida, Itwangi, Usanda, Tinde, Nsalala na Didia.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa majibu ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Jimbo la Solwa, lina Kata 12. Katika Kata 12 ni Kata moja tu ambayo haina maji, ambayo ni Kata ya Lyamidati, bomba kuu la Ziwa Victoria linapita katikati ya nyumba za watu. Je, Serikali ina mpango upi wa kuhakikisha kwamba inasambaza maji katika Kata ya Lyamidati ili wananchi wale waweze kunufaika na maji ya Ziwa Victoria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, Serikali yetu imeweza kujenga tenki kubwa katika Kata ya Tinde Kijiji cha Mchama, lakini ninavyoongea mpaka sasa hivi kijiji kile hakina mtandao wa maji. Tenki lipo lakini wananchi wa kile kijiji hawajaweza kusambaziwa maji. Je, Serikali ina mpango upi wa kuhakikisha kwamba wananchi wale ambao wametoa eneo lao kwa ajili ya ujenzi wa tenki wananufaika na mtandao wa maji?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa harakati kubwa za kuhakikisha akina mama wa Mkoa wa Shinyanga wanatuliwa ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa kwa kuwa Serikali imefanya uwekezaji mkubwa wa miundombinu chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, nimwelekeze Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji kwa eneo la hiyo Kata ambalo halijapata huduma ya maji pamoja na hivi vijiji ambavyo havijaunganishiwa maji, kwa sababu sera ya maji inatutaka linapopita bomba kuu kilometa 12 mwa bomba kuu kulia na kushoto vinatakiwa viunganishiwe maji.

Nimwelekeze atoe kibali mara moja na kazi ianze kuhakikisha wananchi hao wanapata huduma ya maji safi na salama.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jumaa Aweso, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, sasa ninamwita Mheshimiwa Alan Thomas Mvano, Mbunge wa Kakonko, aulize swali lake.

Na. 50

Kupeleka Mbegu za Ruzuku kwa Wakulima wa Kakonko kwa Msimu 2026

MHE. ALAN T. MVANO alijibu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka mbegu za ruzuku kwa wakulima wa Kakonko kwa mazao ya mahindi, maharage na mtama kwa msimu wa 2026?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara majibu kwa niaba ya Wizara ya Kilimo.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo ninaomba nijibu swali Namba 50 kutoka kwa Mheshimiwa Alan Thomas Mvano kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kupunguza gharama za upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima, ikiwa ni pamoja na utoaji wa ruzuku ili kuongeza matumizi ya mbegu bora za mazao mbalimbali kulingana na gharama za pembejeo hizo katika soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa mikakati hiyo, upatikanaji wa mbegu bora nchini umeongezeka kutoka tani 64,152 mwaka 2022/2023 hadi tani 72,031.85 mwaka 2025/2026. Aidha, kuongezeka kwa matumizi ya mbegu bora kumewezesha kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya nafaka kutoka tani 11,448,757 mwaka 2022/2023 hadi tani 14,924,582 mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kufanya tathmini ya utekelezaji wa mpango wa utoaji wa ruzuku ya mbegu bora ili kubaini njia mbadala ambayo itawezesha wakulima kupata mbegu bora kwa bei nafuu bila kuathiri uzalishaji wa mazao ya kilimo, pamoja na kupunguza gharama zitokanazo na ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa Serikali. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Alan Thomas Mvano, swali la nyongeza.

MHE. ALAN T. MVANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali yanayoonyesha jitihada katika kuhakikisha wakulima wetu wanapata mbegu bora, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza, ni kwamba katika Wilaya ya Kakonko tumekwisha tenga ekari 257 na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo *(TARI)* tayari iko pale kwa ajili ya kuzalisha mbegu na kufanya utafiti. Kwa kuwa, tayari taasisi hiyo ipo ndani ya Wilaya ya Kakonko. Je, Serikali ina mkakati upi wa kuhakikisha kwamba wananchi wa Kakonko pamoja na maeneo ya jirani wananufaika na mbegu bora kwa gharama nafuu ili kuwapunguzia gharama katika uzalishaji wa kilimo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, katika Wilaya ya Kakonko tumekuwa na changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa mbolea za ruzuku, wananchi wa Kakonko wamekuwa wakitoka Kakonko na kwenda maeneo ya Wilaya za jirani kutafuta mbolea za ruzuku. Je, Serikali ina kauli ipi kuhakikisha kwamba katika msimu huu

wa kilimo tunaouendea, wakulima wetu wanafikiwa na mbolea za ruzuku ili waweze kuongeza tija katika kilimo chao?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Alan Thomas Mvano, Mbunge wa Kakonko kwa jitihada zao na *commitments* zao za kutenga eneo ambalo wameliweka kwa ajili ya *TARI* kuzalisha mbegu, na kufanya utafiti wa mbegu bora katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii kumwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Mbegu Tanzania *(ASA)* akishirikiana na *TARI* kwenda Kigoma, hususani Wilaya ya Kakonko kuangalia eneo hilo ili watoe ushirikiano na mamlaka za Mkoa wa Kigoma, hususani hapo Kakonko, kuona ubora wa eneo hilo kwa ajili ya matumizi ambayo wamepangia kufanya utafiti wa mbegu na uzalishaji wa mbegu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la mbolea ya ruzuku mbolea ya ruzuku inatolewa kupitia, ama inasambazwa kupitia mawakala. Ninaomba nikiri kwamba ni kweli kuna maeneo mengine ambayo hayana mawakala, ama wananchi wanapaswa kwenda mbali kufuata mawakala walipo lakini hiyo pia ni fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe rai kwa Mheshimiwa Mbunge na wadau wote wa sekta ya kilimo kuichangamkia fursa hiyo kuomba uwakala kupitia Mamlaka ya Kudhibiti Mbolea *(TFRA)* ili wajisajili kwa ajili ya kutoa huduma za mbolea kwa karibu kwa wakulima wa Jimbo la Kakonko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba nitoe maelekezo kwa Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Mbolea Tanzania *(TFC)* akishirikiana na *TFRA* kuangalia *gap* lililopo, ama pengo la usambazaji wa mbolea kwa wananchi wa Kakonko ili watumie *gap*

hilo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata mbolea kwa karibu na kwa wakati. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dennis Londo, Naibu Waziri, Viwanda na Biashara tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, sasa ninamwita Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, Mbunge wa Musoma Mjini, aulize swali lake.

Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko kwa niaba yake.

Na. 51

Kuboresha Bandari ya Musoma Mjini

MHE. ESTHER N. MATIKO K.n.y. MGORE M. KIGERA aliuliza:-

Je, lini Serikali itaiboresha Bandari ya Musoma Mjini ili ianze kufanya kazi na kufungua fursa za kiuchumi kwa wananchi kupitia Ziwa Victoria?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kubaini mahitaji halisi na uwezekano kuendeleza bandari za Maziwa Makuu, ikiwemo Bandari ya Musoma, Serikali kupitia *TPA* imetenga kiasi cha shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuratibu upembuzi yakinifu ambao unatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha wa 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilika kwa upembuzi huo, Serikali itakuwa kwenye nafasi nzuri ya kuelewa namna bora na lini Bandari ya Musoma itaendelezwa kutokana na matarajio ya shehena na abiria watakaovutia safari za meli kama *MV Mwanza* kuanza kufanya safari kutoka na kuelekea katika bandari hiyo. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwanza kabisa nipende kuishukuru Serikali na kuipongeza kwa kukamilisha uwanja wa ndege wa Musoma ambao unaboresha usafirishaji na sasa wananchi wa Mkoa wa Mara wataanza kupata safari za ndege kutoka Dar es Salaam, Musoma, Mwanza siku ya Alhamisi na Jumamosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yangu mawili ya nyongeza, kwa kuwa bandari ya Musoma ni lango kuu la kimkakati linalounganisha Mkoa wa Mara na masoko ya nchi Jirani, na kwa kuwa kupitia bandari ya Musoma kunaweza kuzalisha fursa za kibiashara, usafirishaji wa mizigo na ajira. Je, Serikali iko tayari kutuambia ni lini wananchi wa Mkoa wa Mara wataanza kuona utekelezaji wa mradi huu kwa vitendo baada ya upembuzi yakinifu kukamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa reli ya Tanga – Arusha – Musoma bila uwepo wa bandari yenye uwezo wa kupokea na kusafirisha mizigo haiwezi kukamilisha thamani ya *corridor* hii. Na kwa kutambua dhamira ya dhati ya Serikali ya kuendeleza bandari ya Musoma. Na kwa kuzingatia pia kuchelewa kwa bandari hii kuendelezwa kunaweza kuchelewesha mfumo mzima wa thamani kwenye *corridor* hii. Je, Serikali iko tayari kuipa kipaumbele bandari ya Musoma ili utekelezaji wake uweze kuendana na maendeleo ya ujenzi wa reli ya Tanga – Arusha – Musoma?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi kumpongeza sana Mheshimiwa Mgore Miraji, Mbunge wa Musoma Mjini kwa jinsi ambavyo anapaza sauti akiungana na Mheshimiwa Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini, ambaye kimsingi ameleta hapa pongezi Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza pongezi za kukamilisha uwanja wa ndege wa Musoma lakini pili kwa kulipokea tangazo la ndege yetu, kampuni yetu ya Ndege ya *ATCL* ambayo inaanza rasmi safari zake kwenda Musoma kupitia Mwanza kila Alhamisi na Jumamosi. Hili ni jambo jema ambalo Waheshimiwa Wabunge wamethibitisha jinsi walivyo na moyo wa shukrani, na wanavyofuatilia masuala makubwa katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa namna anavyofuatilia miradi ya Mkoani Mara kwa ujumla, kuanzia uwanja wa Serengeti ambao Serikali imeshatangaza tenda, tunakwenda kupata mkandarasi, pamoja na sasa anazungumzia bandari. Bandari hii kwanza imetajwa katika Ilani ya CCM. Ukienda Ibara 42 na 43 utakuta CCM ilivyojipanga na ilivyoona umuhimu wa kujenga Bandari ya Musoma ili kufungamanisha na reli inayotoka Tanga kwenda Musoma na matawi ya Dutwa kwenye madini ya *Nickel*, pamoja na Engaruka kwenye madini ya *Potash* kwa maana ya kwenye madini ya magadi soda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa swali lake la nyongeza ambalo ameliuliza kuhusiana na umuhimu na lini hasa, kwa sasa Serikali pamoja na kuona umuhimu kwenye Ilani ya CCM imeshaanza upembuzi yakinifu kwa kutambua umuhimu huo, tumetenga bilioni moja yaani milioni 1000 kwa kazi hiyo moja tu ili kuweza kujua, je, bandari hii ina nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya upembuzi yakinifu, kwanza ndiyo inatoa ramani kamili ya mradi husika ndiyo inatupatia gharama zitakazotumika na ndiyo inatuambia muda utakaotumika,

ndiyo inatupa namna bora ya kutekeleza, ndiyo inatuambia kwamba kuna *risk* zipi kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Tarime Mjini ambaye ameuliza swali kwa niaba ya Mheshimiwa Mbunge wa Musoma Mjini kwamba, Serikali inatambua na imekwishaanza, katika mwaka wa fedha huu inakwenda kuanza kufanya upembuzi yakinifu mara baada ya kukamilisha tunakwenda kuanza mchakato kwa ajili ya kujenga bandari hiyo. Kwa hiyo nimtoe mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo maana ya hoja yake kwamba ni kipaumbele, ni kweli Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameliona jambo hilo ni kipaumbele na anawahakikishieni wananchi wa Musoma na Kanda ya Ziwa kwamba ni mpango wa Serikali kwenda kuboresha bandari hii ya Musoma. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa David Kihenzile, Naibu Waziri wa Uchukuzi, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Madini, sasa namwita Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum aweze kuuliza swali lake.

Na. 52

Mchango wa Wachimbaji wa Madini

MHE. AZIZA S. ALLY aliuliza:-

Je, upi mchango wa wachimbaji wakubwa na wadogo wa madini kitakwimu ndani ya miaka mitano?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, kwa niaba ya Wizara ya Madini.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI K.n.y. WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile ni mara yangu ya kwanza kusimama baada ya kuteuliwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, nitumie fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuiona Wizara yetu ya Nishati na kumteua Mheshimiwa Ndejembi aweze kumsaidia, tunamtakia kila la kheri katika majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Madini ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa sekta ya madini kwa ujumla ndani ya kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2020 hadi 2025, mchango wa sekta hii katika pato la Taifa umeongezeka kwa asilimia saba nukta moja mwaka 2020 hadi 10.3% mwaka 2025. Mchango huu umeiwezesha sekta ya madini kuvuka lengo la kuchangia 10% ya pato la Taifa ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maduhuli ya Serikali yatokanayo na shughuli za madini yameongezeka kwa kiasi kikubwa kutoka shilingi bilioni 624.61 mwaka 2021/2022 hadi shilingi trilioni 1.39 mwaka 2025/2026. Ongezeko hili limechangiwa na shughuli za wachimbaji wakubwa na wadogo, ambapo kwa wastani katika kipindi hicho wachimbaji wakubwa wamechangia takribani 60% ya makusanyo hayo, huku wachimbaji wadogo wakichangia takribani 40%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa pande zote mbili, ikiwemo kuboresha upatikanaji wa maeneo ya uchimbaji, huduma za kitaalamu na kifedha, masoko ya madini, teknolojia ya uchimbaji na uchenjuaji pamoja na mifumo ya udhibiti na ufuatiliaji wa biashara ya madini ili kuongeza mchango wa wachimbaji wakubwa na wadogo katika uchumi wa Taifa. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, swali la nyongeza.

MHE. AZIZA S. ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri. Pia, ninaomba nitoe pongezi kwa wachimbaji wadogo kwa kufikia 40% hawakuwa na mikopo wala hawakuwa na vitendea kazi vilivyo imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mkakati gani wa kuweza kuwawezesha wachimbaji wadogo waweze kupata mikopo ili waweze kuongeza pato la Taifa kuliko kwenye 40% waliyopo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mkakati gani kwa hawa wachimbaji wa kati waweze ili nao kupata msamaha wa kodi kama wanavyopata msamaha wa kodi wachimbaji wakubwa ili tuwe na wachimbaji wakubwa wengi katika nchi yetu na waongeze Pato la Taifa? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI K.n.y. WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kumpongeza Mheshimiwa Aziza kwa uwakilishi wake makini kwa wananchi wa Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aziza, ameuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza ni kuhusiana na mikopo kwa wachimbaji wadogo. Serikali kwanza kwa ajili ya kuwasaidia wachimbaji wadogo tulibadilisha Sheria ya Madini na tukaweka kipengele ambacho kwa wamiliki wa leseni ambao hawana fedha kwa ajili ya kuendeleza leseni zao wanaweza kutafuta msaada wa kiufundi kwa wataalamu wa ndani na nje ya nchi ili waweze kufanya uzalishaji wenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Serikali kupitia Wizara ya Madini na Shirika la Madini Tanzania *STAMICO* wameingia mkataba na Benki za *CRDB, NMB, KCB* na Azania kwa ajili ya kuwatengenezea mazingira maalum ya kuwapatia mikopo wachimbaji wadogo. Mheshimiwa Mbunge utakubaliana na mimi, tumeona mabadiliko

makubwa ya wachimbaji. Hata hili jambo unaloliona la Katoro, ni matokeo ya kazi kubwa iliyowekezwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu wachimbaji sasa wanapata msaada wa kitaalamu, wanapata msaada wa kifedha na wanawezeshwa na Shirika letu la *STAMICO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na msamaha wa kikodi. Mheshimiwa Mbunge nikutoe wasiwasi, Serikali kwanza imetenga maeneo maalum na imeweka masharti maalum ya maeneo ambayo wachimbaji wadogo wanaruhusiwa kuchimba pekee na maeneo hayo hayawezi kuingiliwa na wachimbaji wakubwa. Hiyo ni kwa ajili ya kuwalinda wachimbaji wadogo wasiingie kwenye *competition* na wachimbaji wakubwa katika kupata leseni hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, Serikali kupitia Wizara ya Fedha wanayo taasisi maalum ambayo inatoa dhamana ya mikopo, yaani *Credit Guarantee Scheme,* kwa ajili ya kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata fedha zenye nafuu, gharama nafuu na kodi nafuu kwa ajili ya shughuli zao za kila siku. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salome Makamba, Naibu Waziri wa Nishati, kwa niaba ya Wizara ya Madini, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, sasa ninamwita Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake. *(Makofi)*

Na. 53

Kanuni za Uvuvi kupunguza kero za Tozo nyingi kwa Wavuvi

MHE. SYLVIA F. SIGULA aliuliza:-

Je, lini Serikali itapitia tena Kanuni za Uvuvi ili kupunguza kero za tozo nyingi kwa wavuvi?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, ninaomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imefanya mapitio ya Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009 na kufanya marekebisho ya mwaka 2026 kwa lengo la kuiwezesha kuendana na mabadiliko ya kisera, kiuchumi, kimazingira na kiteknolojia ili kuimarisha usimamizi na udhibiti wa rasilimali za uvuvi. Aidha, katika mapitio hayo tozo na ada mbalimbali zimepitiwa kwa lengo la kupunguza kero na gharama kwa wadau wa uvuvi bila kuathiri utekelezaji wa wajibu wa Wizara kwa kusimamia, uhifadhi na kuendeleza rasilimali za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeandaa na kuziunganisha kanuni zote za ada na tozo ili kuwa na kanuni moja ya ada na tozo kwa sekta ya uvuvi. Aidha, kanuni hii inayojulikana kwa jina la Kanuni za Tozo na Ada ya Mwaka 2026 ipo katika ngazi mbalimbali za kukamilishwa, sambamba na uanzishwaji wa Mamlaka ya Uvuvi. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, swali la nyongeza.

MHE. SYLVIA F. SIGULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru, na ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kero ya tozo na ada kwa wavuvi ni jambo ambalo limekuwa ni la muda mrefu sana.

Wabunge wengi wamekuwa wakilalamika lakini pia wananchi wenyewe wavuvi wamekuwa wakilalamika kwa muda mrefu sana. Majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yanasema ziko kwenye hatua mbalimbali, lakini wavuvi walitamani kujua kwa sababu hatua mbalimbali hizo zimechukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini hasa hatua mbalimbali hizo zitakamilika ili wavuvi waweze kuendelea na utaratibu mzuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri, baada ya Bunge hili uko tayari kuongozana na mimi, kufanya ziara katika Mkoa wa Rukwa, kuongea na wavuvi ili uone uzito wa kero hizi wanazozipata wavuvi wenyewe. Wavuvi wa Kalambo, wavuvi wa Kasanga, wavuvi wa Wampembe, wavuvi wa Kala, wavuvi wa Kabwe? Je, uko tayari kwenda kuwasikiliza uone uzito wa kero hizi wanazopitia wavuvi? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwanza kabla ya yote nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula kwa namna anavyoendelea kuwapambania wavuvi wote wanaovua katika Ziwa Tanganyika, kwa namna ya pekee nimpongeze sana yeye na kuona kwamba wanawake wa Mkoa wa Rukwa kwa hakika wamechagua jembe na jemedari mzuri kabisa wa kuwakilisha ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema, tumekuwa na hatua mbalimbali ambazo tumezifanya katika kupitisha kanuni hizi, kama nilivyojibu katika majibu ya awali, ni kwamba kanuni hizi zinaitwa Kanuni za Tozo na Ada za Mwaka 2026. Hivyo nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba, hatua tuliyopo sasa, hatua zote za awali zimeshakamilika, hatua ya mwisho ya sasa ni kuhakikisha kwamba wenzetu wa Wizara ya Fedha wanapitia kanuni hizi kwa sababu zina *implication* za kifedha na kibajeti ili baada ya hapo Mheshimiwa Waziri aweze kuzi-*sign* zianze kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimtoe hofu ndani ya mwaka huu wa fedha mwaka 2026 kanuni hizi zitakuwa tayari na zitaanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia swali lake la pili la utayari wangu wa kuongozana naye, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya Bunge hili tuonane ili tupange ratiba nzuri ya lini hasa, tutakuwa na muda mzuri twende tukazungumze na wavuvi wa Mkoa wa Rukwa, lakini na wavuvi wote ambao wanavua katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, nitumie jukwaa hili pia kutoa rai kwa vijana wote wa Mkoa wa Rukwa na Mikoa yote inayovua Ziwa Tanganyika na Maziwa Makuu (Ziwa Nyasa na Ziwa Victoria) kuchangamkia fursa ya mikopo ambayo imetangazwa na Wizara yetu ya Mifugo na Uvuvi, ambapo tunatoa vizimba kwa ajili ya ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo vyetu ni vyepesi na vinawezekana. Ni Mtanzania mwenye umri kati ya miaka 18 na 35 ambaye ni mkazi wa eneo husika ambapo mradi unafanyika lakini ambaye hana mikopo chechefu kwenye taasisi yoyote ya fedha, aweze kuchangamkia fursa hizi ambazo mwisho wa maombi haya ni Tarehe 14 mwezi Septemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado tuna muda wa kutosha na niwaombe Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo yote ambayo yanapakana na maziwa haya ya Tanganyika, Nyasa na Victoria, kuwahamasisha vijana wetu kuomba mikopo hii ili nao waweze kunufaika. Ninakushukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunamalizia swali letu la mwisho ambalo linaelekezwa Wizara ya Viwanda na Biashara. Sasa

ninamwita Mheshimiwa Athumin Omary Mapalilo, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 55

Kuwa na Utaratibu Maalum kwenye Viwanda vya Saruji

MHE. ATHUMIN O. MAPALILO aliuliza:-

Je, lini Serikali itaweka utaratibu maalum kwenye viwanda vya saruji Mkoani Mtwara ili kupunguza bei kwa kuwa uzalishaji unafanyika Mkoani humo?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Viwanda na Biashara.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, ninaomba nijibu swali la kutoka kwa Mheshimiwa Athumin Omary Mapalilo, Mbunge wa Viti Maalum, Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoani Mtwara kuna viwanda viwili vya saruji ambavyo ni kiwanda cha Dangote na kiwanda cha Lulu. Kiwanda cha Dangote ndicho chenye uzalishaji mkubwa wa *cement* ambapo hadi kufikia tarehe 22 Agosti, 2026, bei ya saruji ya kiwandani Mkoani Mtwara ilikuwa shilingi 16,500 kwa mfuko, kwa Dar es Salaam bei ya kwenye ghala *(depot)* ilikuwa ni shilingi 18,200, na *Depot* Dodoma ilikuwa ni shilingi 20,200. Tofauti ya bei kati ya Mtwara na maeneo mengine inaakisi kwa kiasi kikubwa umbali na gharama za usafirishaji na usambazaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Dangote kimetoa masharti nafuu kwa wanunuzi wa jumla wa Mtwara ukilinganisha na maeneo mengine ya nchi. Kwa msingi huo, bei ya kiwandani Mkoani Mtwara ni nafuu kuliko maeneo mengine nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kufuatilia mnyororo wa usambazaji ili kuhakikisha kuwa manufaa ya ukaribu wa kiwanda yanaonekana pia katika bei ambayo mlaji wa mwisho analipa Mkoani Mtwara na kuzuia ongezeko la bei lisiloendana na gharama halisi za biashara. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Athumin Omary Mapalilo, swali la nyongeza.

MHE. ATHUMIN O. MAPALILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Niipongeze Wizara kwa kutoa majibu mazuri sana na kwa sababu hiyo, nitakuwa na swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mkoa wa Mtwara una rasilimali ya gesi na bandari, na kwa kuwa uwepo wa rasilimali hii husaidia sana kupunguza gharama za uzalishaji. Na kwa kuwa, bidhaa ya saruji kutoka bandarini kwenda kwa walaji ipo chini zaidi ukilinganisha na maeneo mengine. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwashauri viwanda vya Dangote na Lulu *Cement* kuhakikisha kwamba wanaendelea kupunguza bei ya saruji kwa Mkoa wa Mtwara ili kurahisisha maendeleo kwa wananchi wa Mkoa wa Mtwara? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2020/2050, imejikita kwenye uchumi wa viwanda. Pia uwekezaji mkubwa tunauweka kwenye ujenzi wa miundombinu, hasa bandari, reli na barabara, lakini pia kuhakikisha kwamba tunapeleka umeme wa uhakika na mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la uwekezaji huu mkubwa ni kushusha gharama ya uzalishaji na biashara kwa wafanyabiashara, wasambazaji na wazalishaji. Lengo la Serikali ni kuona kwamba,

punguzo la gharama hizi kwa uwekezaji huu mkubwa kwenye miundombinu linaenda ku-*reflect* kwenye bei ya mwisho ya mlaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Bandari ya Mtwara ni moja ya maeneo ya kimkakati ambayo dira yetu na Ilani ya Chama cha Mapinduzi inaelekeza kuhusiana na upanuzi mkubwa lakini ujenzi wa miundombinu rafiki, pamoja na bandari hiyo, Bandari ya Bagamoyo pamoja na Dar es Salaam inaenda kuona upanuzi mkubwa, lengo ni kurahisisha usafiri na kupunguza gharama kwa mlaji. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali imejizatiti kuwekeza katika kupunguza gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa saruji katika maeneo ya Mtwara, umetokana na kuharibika kwa mitambo kwenye Kiwanda cha Dangote na Maweni ambayo kwa pamoja wanazalisha zaidi ya 55% ya saruji. Pia, Serikali inafuatilia kwa karibu kuona kwamba sababu ni hizo ama kuna sababu nje ya hizo, kwa sababu kupungua kwa uzalishaji kumepelekea kupanda kwa bei ya saruji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi viwanda na biashara tuna jukumu siyo tu la kulinda mzalishaji kwa maana ya viwanda, tuna jukumu la ku-*stabilize* bei lakini kuhakikisha kwamba bidhaa inapatikana kwa bei ambayo ni *affordable*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imejizatiti kujua kama ni sababu hizo tu ama kuna sababu nyingine ili tuchukue hatua stahiki kuhakikisha kwamba saruji inapatikana na bei inakuwa rafiki kwa mlaji. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dennis Londo, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Ninaomba sasa niwatambulishe wageni waliopo Bungeni.

Tukianza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika, wapo wageni watano wa Mheshimiwa Balozi Khamis Mussa Omar, Waziri wa Fedha, ambao ni Wakurugenzi na Watendaji Wakuu kutoka Wizara ya Fedha; yupo Ndugu Nsubili Joshua, Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha; na Ndugu Dionisia Mjema, Kaimu Kamishna wa Idara ya Maendeleo ya Sekta ya Fedha.

Wengine ni Ndugu Mgonya Benedicto, Meneja Usimamizi wa Sera za Bajeti na Madeni ambaye anamwakilisha Gavana; Ndugu Mwantumu Sultani, Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Huduma za Sheria; na Ndugu Fred Ilomo, Kaimu Kamishna Msaidizi wa Idara ya Maendeleo ya Sekta ya Fedha. *(Makofi)*

Wapo pia wageni watano wa Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava ambao ni viongozi wa dini kutoka Kanisa la KKKT Lushoto Mkoani Tanga, wakiongozwa na Askofu Dkt. Msafiri Joseph Mbilu wa Kanisa la KKKT Dayosisi ya Kaskazini Mashariki, Lushoto. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Kaspar Kaspar Mmuya, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, pamoja na Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka, ambao ni viongozi wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Wilaya za Ruangwa, Nachingwea na Mtama Mkoani Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia yupo Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Nachingwea, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Ruangwa, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Lindi Vijijini na Katibu wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Nachingwea. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga, ambao ni rafiki zake kutoka Makete Mkoani Njombe. *(Makofi)*

Yupo pia mgeni mmoja wa Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, ambaye ni Ndugu Leith Ahmed, mtoto wake kutoka Solwa Mkoani Shinyanga. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Arif Suleiman Premji, ambao ni familia yake kutoka Mkoani Mtwara. *(Makofi)*

Wapo wageni 35 wa Mheshimiwa Mariam Madalu Saidi Nyoka, ambao ni ndugu, jamaa na marafiki kutoka Wilaya ya Ubungo, Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Naomy Duncan Mwaipopo, ambaye ni Ndugu Aria *Store,* Mfanyabiashara kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wengine ni wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 76 na walimu watano wa Shule ya Msingi Dabalo kutoka Wilaya ya Chamwino Mkoani Dodoma. *(Makofi)*

Karibuni sana wageni wote ambao mmepata fursa ya kututembelea hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwaletee matangazo. Tangazo la kwanza ni taarifa ya Bunge Bonanza, iliyofanyika Jumamosi tarehe 29 Agosti, 2026, katika Shule ya Sekondari ya John Merlini, Dodoma.

Tamasha la *NMB Bunge Bonanza*, lililofanyika Jumamosi liliwashirikisha Wabunge, Watumishi wa Ofisi ya Bunge, Maafisa wa Benki ya NMB, Wizara, Vyuo vya Elimu ya Juu, taasisi mbalimbali za umma, pamoja na *club* za *jogging* kutoka Dodoma.

Wadhamini Wakuu wa bonanza hilo lililobebwa na kauli mbiu, "Pamoja *AFCON,* Tanzania Tuko Tayari," walikuwa ni Benki ya NMB. Mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Daniel Sillo, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waheshimiwa Wabunge, matokeo yalikuwa kama ifuatavyo:-

Mpira wa miguu, Wizara ya Ardhi walishinda magoli matatu kwa *zero* dhidi ya Bunge. Mpira wa pete Bunge walishinda NMB seti

47 kwa seti 38. Mpira wa kikapu wanaume Bunge walishinda seti 38 kwa seti 35 dhidi ya NMB. *(Makofi)*

Mpira wa kikapu wanawake Bunge walishinda seti 33 kwa nne dhidi ya *UDOM*. Mpira wa wavu wanaume TAMISEMI walishinda seti nne kwa moja dhidi ya maliasili; Mpira wa kikapu wanawake ulinzi walishinda seti mbili kwa *zero* dhidi ya Bunge; kuvuta kamba wanaume Uchukuzi waliwashinda Mahakama; kuvuta kamba wanawake, Nishati iliwashinda Wizara ya Madini; kupokezana vijiti, wanaume Wizara ya Katiba na Sheria walikuwa washindi; na kupokezana vijiti, wanawake Mahakama walikuwa washindi.

Washindi wa medali. Washindi wa kwanza wa kila mchezo wa mtu mmoja mmoja walipewa medali ya dhahabu kwa upande wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni kama ifuatavyo:-

Riadha, mita 100 wanawake mshindi alikuwa Mheshimiwa Latifa Juwakali, riadha mita 100 wanaume mshindi alikuwa Mheshimiwa Abubakari Asenga. Karata wanawake mshindi alikuwa Mheshimiwa Tinnar Andrew Chenge. *(Makofi)*

Kurusha vishale, wanawake mshindi alikuwa Mheshimiwa Mwantumu Mbaraka. Kukimbiza kuku wanawake mshindi alikuwa Mheshimiwa Sara Msafiri. *Pool table* wanawake mshindi alikuwa Mheshimiwa Esther Matiko.

Waheshimiwa Wabunge, Tangazo hili limeletwa na Mheshimiwa Festo Sanga Mwenyekiti wa Bunge Bonanza. Hongereni sana Waheshimiwa Wabunge wote mliopata ushindi na medali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nilete tangazo. Tunatangaziwa kuwa kesho siku ya Jumanne tarehe 1 Septemba, 2026 kutakuwa na semina itakayoendeshwa na Soko la Hisa la Dar es Salaam kuhusu uwekezaji wa masoko na mitaji ya umma na huduma zinazotolewa. Semina hiyo itafanyika katika ukumbi wa Pius Msekwa kuanzia saa saba mchana mara baada ya kusitisha

Shughuli za Bunge. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu. Tangazo limetolewa na Katibu wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba iliyoko mbele yetu.

Katibu.

NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* - KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana ya Mali Zinazohamishika wa Mwaka 2026

(Kusomwa Mara ya Pili)

MWENYEKITI: Sasa ninamwita Mheshimiwa Waziri wa Fedha Mheshimiwa Balozi Khamis Omar.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Mikopo wa Dhamana za Mali Zinazohamishika wa Mwaka 2026 pamoja na Marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninapenda kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi kwa kuaminiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kuteuliwa kuwa Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uteuzi huu ni heshima kubwa na ni ishara ya imani ambayo Mheshimiwa Rais ameendelea kuwa nayo kwake. Ninamwombea afya njema, hekima, busara na nguvu katika kutekeleza majukumu yake mapya kwa uadilifu na kwa maslahi

mapana ya Taifa. Naamini kuwa uzoefu na uwezo wa Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, utaendelea kuwa chachu katika kuimarisha maendeleo, umoja na ustawi wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Ali Hassan King, Mbunge wa Jimbo la Jang'ombe na Wajumbe wote wa Kamati kwa kujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri kwa ajili ya kuuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Muswada umezingatia ushauri wa mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na wadau mbalimbali. Aidha, ninawashukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wataalamu wake pamoja na wataalamu wa Wizara ya Fedha kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kutunga Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali Zinazohamishika ya Mwaka 2026 ni kuweka masharti bora ya usimamizi wa mikopo inayopatikana kwa kutumia dhamana zinazohamishika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, sheria inayopendekezwa inakusudia kuongeza watumiaji wa huduma za benki na kufikia 50% ifikapo mwaka 2030 kutoka 22% ya mwaka 2023. Kuongeza uwiano wa mikopo kwa sekta binafsi kwa pato la Taifa kufikia 50% ifikapo mwaka 2030 kutoka 22.5% mwaka 2024 kuongeza ajira na kuongeza ukuaji wa sekta ya fedha na kufikia 20% mwaka 2030 kutoka 17.1% mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za hivi sasa zinazotarajiwa kutatuliwa kwa kutungwa sheria hiyo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Kutokuwepo na mfumo jumuishi wa usajili wa dhamana kwa ajili ya kusajili mali zinazohamishika zinazoweza kutumika kama

dhamana. Changamoto hii imesababisha matumizi ya dhamana moja kwa mikopo mbalimbali bila wakopeshaji wengine kuwa na taarifa, na hivyo kusababisha ongezeko la mikopo isiyolipwa, yaani chechefu katika sekta ya fedha;

(ii) Kukosekana kwa usimamizi na utaratibu wa pamoja wa mali zinazohamishika zinazoweza kutumika kama dhamana; na

(iii) Kukosekana kwa utaratibu wa utekelezaji wa haki za mkopaji na mkopeshaji wakati wa kuuza dhamana za mali zinazohamishika, ikizingatiwa kuwa dhamana hizo zinaweza kupoteza thamani ndani ya muda mfupi au kuharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umegawanyika katika sehemu 10. Sehemu ya Kwanza yenye Ibara ya kwanza hadi ya tatu, ikisomwa pamoja na jedwali la marekebisho, inahusu masharti ya utangulizi yanayojumuisha jina la kuanza kutumika kwa sheria, matumizi, pamoja na fasili ya tafsiri ya misamiati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili ya Muswada ikisomwa pamoja na Jedwali la Marekebisho Ibara ya nne, tano na sita inaanzisha masijala ndani ya Benki Kuu ya Tanzania itakayojulikana kama masijala ya dhamana na kuainisha mamlaka ya benki na ukasimishaji wa majukumu ya masijala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu ya Muswada ikisomwa pamoja na Jedwali la Marekebisho yenye Ibara ya saba hadi ya 11, inaainisha matumizi ya maslahi kwa dhamana ya mkopo mmoja au zaidi, mali zinazoweza kuwekwa dhamana ambazo ni mali zinazohamishika au zinazoshikika au zisizoshikika, zinazogawanyika au zisizogawanyika au zenye asili moja. Aidha, sehemu hii inaweka sharti kwa Gavana kushauriana na Waziri kabla ya kutangaza mali zinazoweza kutumika kama dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii vilevile inaainisha kwa maslahi katika dhamana yatajumuisha mapato yanayotambulika yanayotokana na dhamana. Sehemu ya nne ya Muswada ikisomwa

pamoja na Jedwali la Marekebisho Ibara ya 12 hadi 15 inahusu usajili wa maslahi, kipindi cha uhalali wa usajili wa maslahi, marekebisho au ufutaji wa usajili wa maslahi na upekuzi wa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tano ya Muswada ikisomwa pamoja na Jedwali la Marekebisho yenye Ibara ya 16 hadi 18 inahusu maslahi katika dhamana dhidi ya mtu wa tatu, maslahi katika mapato yanayotokana na dhamana dhidi ya mtu wa tatu na utekelezaji wa maslahi katika mali zinazohamishika zilizochanganywa dhidi ya mtu wa tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Sita ya Muswada ikisomwa pamoja na Jedwali la Marekebisho yenye Ibara ya 19 hadi ya 34 inaainisha vipaumbele katika maslahi, wakopaji tofauti, mapato na mali zinazochanganywa kwa mkusanyiko na athari za kufilisika kwa mkopaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile sehemu hii inaainisha haki za mnunuzi, mpokeaji, mkodishaji au mmiliki wa leseni za matumizi ya dhamana na kuwa mshindi wa tuzo atakuwa na haki ya kipaumbele dhidi ya maslahi katika dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Saba ya Muswada ikisomwa pamoja na Jedwali ya Marekebisho yenye Ibara 35 hadi 42 inaainisha haki ya kukagua dhamana, wajibu wa kutoa taarifa, jukumu la kutunza dhamana, haki na wajibu wa mdaiwa kuomba uthibitisho au kukataa deni au madai ya malipo yaliyofanywa na mdaiwa, unufaikaji na haki katika makusanyo tarajiwa, mali au hati za malipo zinazoziwezesha au kudhamini malipo au utekelezaji mwingine wa dhamana, utengenezaji wa maslahi katika haki ya malipo ya fedha zilizowekwa kwenye akaunti na ulinzi wa haki za mkopaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nane ikisomwa pamoja na Jedwali la Marekebisho yenye Ibara ya 43 hadi 58 inaainisha masharti ya usajili wa taarifa za utekelezaji, uondoaji wa dhamana, utumiaji wa dhamana katika kutekeleza wajibu unaotokana na

mkopo, utaratibu wa uondoaji wa dhamana, ukomo wa maslahi katika dhamana baada ya uondoaji, mgawanyo wa mapato baada ya uondoaji, pendekezo la kumiliki dhamana katika malipo ya deni la pingamizi dhidi ya pendekezo la kumiliki dhamana, uombaji wa dhamana na uhuishaji wa makubaliano ya mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, sehemu hii inaainisha ukomo wa muda wa uhifadhi wa dhamana, gharama za uhifadhi, haki ya mkopaji kuchagua sehemu mbadala ya kuhifadhi dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tisa inahusu masharti ya jumla na ukisoma pamoja Jedwali ya Marekebisho yenye Ibara ya 56 hadi 65 inaainisha utekelezaji wa haki na wajibu kwa nia njema, haki ya kudai fidia dhidi ya ukiukwaji wa wajibu, kinga, kosa la kutoa taarifa za uongo, malalamiko na mapitio ya uamuzi wa benki na rufaa, mtu ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa benki na masuala ya adhabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, sehemu hii inampa mamlaka Mheshimiwa Waziri kutengeneza kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kumi ikisomwa na Jedwali la Marekebisho yenye Ibara 66 hadi 79 zinaainisha marekebisho ya sheria mbalimbali zilizopendekezwa kurekebishwa kuwezesha utekelezaji wa Muswada huu. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania Sura ya 197, Sheria ya Sampuni Sura ya 212, Sheria ya Uhamishaji wa Mali Sura 210 na Sheria ya Vyama vya Ushirika sura ya 211.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2025, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali Zinazohamishika ya Mwaka 2026 ujadiliwe na kupitishwa katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

31 SEPTEMBA, 2026

MHESHIMIWA BALOZI KHAMIS MUSSA OMAR (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MUSWADA WA SHERIA YA MIKOPO KWA DHAMANA ZA MALI ZINAZOHAMISHIKA WA MWAKA 2026 KUSOMWA KWA MARA YA PILI - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali Zinazohamishika wa Mwaka 2026 pamoja na marekebisho yake sasa **usomwe kwa mara ya pili.**

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati **Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi** kwa kuaminiwa na **Mheshimiwa Rais wa Jamhuri Muungano wa Tanzania, Daktari Samia Suluhu Hassan** na kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uteuzi huu ni heshima kubwa na ni ishara ya imani ambayo Mheshimiwa Rais ameendelea kuwa nayo kwake. Ninamuombea afya njema, hekima, busara na nguvu katika kutekeleza majukumu yake mapya kwa uadilifu na kwa maslahi mapana ya Taifa. Ninaamini kuwa uzoefu na uwezo wa **Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi** utaendelea kuwa chachu katika kuimarisha maendeleo, umoja na ustawi wa watanzania.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake *Mhe.* **Mashimba Mashauri Ndaki,** Mbunge wa Maswa na **Makamu Mwenyekiti** *Mhe.* **Ali Hassan Omar King** Mbunge wa Jimbo la Jang'ombe kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri kwa ajili ya kuuboresha. Vilevile, nitumie nafasi hii kuwatakia wote heri ya mwaka mpya wa fedha wa Serikali 2026/2027.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba, Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo mazuri ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na wadau mbalimbali ambao kwa nyakati tofauti walitoa ushauri wao. Aidha, nitoe shukrani zangu kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali,

wataalam wake pamoja wataalam wa Wizara ya Fedha kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** lengo la kutunga Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali Zinazohamishika wa Mwaka 2026 ni kuweka masharti bora ya usimamizi wa mikopo inayopatikana kwa kutumia dhamana zinazohamishika. Kwa ujumla, Sheria inayopendekezwa inakusudia kuongeza watumiaji wa huduma za benki na kufikia asilimia 50 mwaka 2030 kutoka asilimia 22 mwaka 2023; kuongeza uwiano wa mikopo kwa sekta binafsi kwa Pato la Taifa na kufikia asilimia 50 mwaka 2030 kutoka asilimia 22.5 mwaka 2024; kuongeza ajira; na kuongeza ukuaji wa sekta ya fedha na kufikia asilimia 20 mwaka 2030 kutoka asilimia 17.1 mwaka 2024.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** changamoto zilizopo hivi sasa ni pamoja na:

(a) kutokuwepo na mfumo jumuishi wa usajili wa dhamana (centralized collateral registry) kwa ajili ya kusajili mali zinazohamishika zinazoweza kutumika kama dhamana. Changamoto hii imesababisha matumizi ya dhamana moja kwa mikopo mbalimbali bila ya wakopeshaji wengine kuwa na taarifa na hivyo kusababisha ongezeko la mikopo chechefu katika sekta ya fedha;

(b) kukosekana kwa usimamizi na uratibu wa pamoja wa mali zinazohamishika zinazoweza kutumika kama dhamana; na

(c) kukosekana kwa utaratibu wa utekelezaji wa haki za mkopaji na mkopeshaji wakati wa kuuza dhamana za mali zinazohamishika ikizingatiwa kuwa dhamana hizo zinaweza kupoteza thamani ndani ya muda mfupi au kuharibika.

MADHUMUNIYAMUSWADA

7. ***Mheshimiwa Spika,*** Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kumi (10). Sehemu ya Kwanza yenye ibara ya 1 hadi 3 ikisomwa pamoja na Jedwali la Marekebisho inahusu Masharti ya Utangulizi yanayojumuisha jina na kuanza kutumika kwa sheria, matumizi pamoja na fasili ya misamiati.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Pili ya Muswada ikisomwa pamoja na Jedwali la Marekebisho, yenye Ibara ya 4, 5 na 6 inaanzisha masijala ndani ya Benki Kuu ya Tanzania itakayojulikana kama Masijala ya Dhamana na kuainisha mamlaka ya Benki na ukasimishaji wa majukumu ya masijala.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Tatu ya Muswada ikisomwa pamoja na Jedwali la Marekebisho yenye ibara ya 7 hadi ya 11 inaainisha matumizi ya maslahi kama dhamana ya mkopo mmoja au zaidi, mali zinazoweza kuwekwa dhamana ambazo ni mali zinazoshikika au zisizoshikika, zinazogawanyika au zisizogawanyika au yenye asili moja. Aidha, sehemu hii inaweka sharti kwa Gavana kushauriana na Waziri kabla ya kutangaza mali zinazoweza kutumika kama dhamana. Sehemu hii vilevile inaainisha kuwa maslahi katika dhamana yatajumuisha mapato yanayotambulika yanayotokana na dhamana.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Nne ya Muswada ikisomwa pamoja na Jedwali la Marekebisho yenye Ibara 12 hadi 15 inahusu usajili wa maslahi, kipindi cha uhalali wa usajili wa maslahi, marekebisho au ufutaji wa usajili wa maslahi na upekuzi wa taarifa.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Tano ya Muswada ikisomwa pamoja na Jedwali la Marekebisho yenye Ibara 16 hadi 18 inahusu maslahi katika dhamana dhidi ya mtu wa tatu, maslahi katika mapato yanayotokana na dhamana dhidi ya mtu wa tatu na utekelezaji wa maslahi katika mali zinazohamishika zilizochanganywa dhidi ya mtu wa tatu.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Sita ya Muswada ikisomwa pamoja na Jedwali la Marekebisho yenye Ibara ya 19 hadi 34 inaainisha vipaumbele katika maslahi, wakopaji tofauti, mapato, na mali zilizochanganywa kwa mkusanyiko Athari za kufilisika kwa mkopaji. Vilevile, sehemu hii inaainisha haki za mnunuzi, mpokeaji, mkodishaji au mmliki wa leseni za matumizi ya dhamana na kuwa mshida tuzo atakuwa na haki ya kipaumbele dhidi ya maslahi katika dhamana.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Saba ya Muswada ikisomwa pamoja na Jedwali la Marekebisho yenye Ibara ya 35 hadi 42 inaainisha haki ya kukagua dhamana, wajibu wa kutoa taarifa, jukumu la kutunza dhamana, haki na wajibu wa ya mdaiwa kuomba uthibitisho au kukata deni, madai ya malipo yaliyofanywa na mdaiwa, unufuaikaji na haki katika makusanyo tarajiwa, mali au hati za malipo zinzowezesha au kudhamini malipo au ytekelezaji mwingine wa dhamana, utengenezaji wa masaklahi katika haki ya malipo ya fedha zilizowekwa kwenye akaunti na ulinzi wa haki za mkopaji.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Nane ikisomwa pamoja na Jedwali la Marekebisho yenye Ibara 43 hadi 58 inaainisha masharti ya usajili wa taarifa za utekelezaji, uondoshaji wa dhamana, utumiaji wa dhamana katika kutekeleza wajibu unaotokana na mkopo, utaratibu wa uondoshaji wa dhamana, ukomo wa maslahi katika dhamana baada ya uondoshaji, mgawanyo wa mapato baada ya uondoshaji, pendekezo la kumiliki dhamana kama malipo ya deni na pingamizi dhidi ya pendekezo la kumiliki dhamana, ukomboaji wa dhamana na uhuishaji wa makubaliano ya mkopo. Aidha, sehemu hii inaainisha ukomo wa muda wa uhifadhi 5 wa dhamana, gharama za uhifadhi, haki ya mkopaji kuchagua sehemu mbadala ya kuhifadhi dhamana.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Tisa ikisomwa pamoja na Jedwali la Marekebisho yenye Ibara ya 59 hadi 65 inaainisha kuwa ni kosa kutoa taarifa za uongo, malalamiko na mapitio ya uamuzi wa benki na rufaa mtu ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa benki, adhabu.

Aidha. sehemu hii inampa mamalaka waziri kutengeza kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya sheria hii. Utambuzi wa Maslahi katika Sheria ya Uhamishaji Mali Sura 210.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Kumi ikisomwa na Jedwali la Marekebisho, yenye Ibara ya 66 hadi 79 zinaainisha marekebisho ya sheria mbalimbali zinazopendekezwa kurekebishwa kuwezesha utekelezaji wa Muswada huu. Sheria hizo ni zifuatazo: Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania Sura ya 197, Sheria ya Kampuni, Sura ya 212, na Sheria ya Uhamishaji Mali, Sura ya 210, Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sura ya 211.

HITIMISHO

17. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo haya, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2025, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali Zinazohamishika ya Mwaka 2026 ujadiliwe na kupitishwa katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili.

18. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.

Khamis Omar
Waziri wa Fedha

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ninakushukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Sasa ninamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa niaba Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba

ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, ninaomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali Zinazohamishika wa Mwaka 2026 *(Secured Transaction of Movable Properties Act of 2026)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utangulizi. Kwa mujibu wa Kanuni ya 102(1)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ya Mwaka 2025 ikisoma pamoja na Kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Bajeti Sura 439, ninaomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali Zinazohamishika wa Mwaka 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge ya Mwaka 2025, Kamati ilikutana na wadau tarehe 28 na 29 Aprili, 2026 ambapo ilipokea maoni yao kuhusu Muswada. Jumla ya wadau watano walifika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao. Ninaomba kuwatambua wadau hao kama ifuatavyo:-

(i) *Tanzania Bankers Association;*
(ii) *Tanzania Association of Microfinance Institution;*
(iii) Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania;
(iv) Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania; na
(v) *Imarika Microfinance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati ilipokea maoni kupitia baruapepe kutoka kwa *Nyembe Group of entities*, wadau kutoka Jimbo la Vunjo na Mdau binafsi mmoja. Maoni hayo yaliisaidia Kamati katika uchambuzi, kuboresha na kufanya maamuzi kwa maslahi mapana ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umekuja wakati mwafaka hasa ukizingatia kuwa taasisi ya fedha nchini zilikuwa tayari zinakopesha kwa kutumia mali zinazohamishika kwa maana ya *movable asset or properties* kama dhamana kwa mikopo, lakini bila kuwa na msingi rasmi wa kisheria. Taarifa hii inatoa mrejesho wa mashauriano kati ya Kamati na Serikali kuhusiana na Muswada

unaopendekezwa kutungwa. Muswada huo umegawanyika katika sehemu kuu 10 zenye jumla ya Ibara 79.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo wa taarifa. Taarifa hii imegawanyika katika sehemu saba. Sehemu ya Kwanza ni utangulizi; Sehemu ya Pili ni chimbuko la Muswada; Sehemu ya Tatu ni hali ya sekta ya fedha nchini. Sehemu ya Nne ni uchambuzi wa ibara za Muswada; Sehemu ya Tano ni maoni ya jumla; na mwisho ni hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko la Muswada; Hali ya upatikanaji wa mikopo nchini. Maendeleo ya uchumi wa nchi yanategemea mfumo thabiti wa sekta ya fedha wenye ufanisi unaohakikisha kunakuwepo na ukwasi wa kutosha katika kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Utafiti wa soko la mikopo hapa nchini uliofanywa na *Financial Sector Deepening Africa* kwa kushirikiana na *Financial Sector Deepening Trust* ulibainisha aina za mali zinazotumiwa kama dhamana na watu wa huduma wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huo, mali zinazohamishika ndiyo aina ya dhamana inayoongoza kutumiwa na taasisi za benki ambayo ilichangia zaidi ya 46% ya dhamana zote. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa kuna fursa kubwa ya kutumia mali zinazohamishika, zinazomilikiwa na watu binafsi na kupata mikopo endapo kutakuwepo na mfumo madhubuti ya usajili wa maslahi katika mali zinazohamishika zilizotumika kama dhamana kupata mkopo kutoka kwa huduma za fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamana za mikopo zinazokubalika katika sekta ya fedha hivi sasa ni mali zisizohamishika, mfano ardhi. Utafiti wa *FINSCOP 2023* umeshakuwa asilimia tatu ya wananchi wenye hatimiliki rasmi za umiliki wa ardhi nchini. Kutokana na hali hiyo, wananchi wengi wanakosa sifa ya kukopa kwa masharti nafuu kutoka benki na taasisi za fedha. Hali hii imesababisha upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi kuwa wa kiwango cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Disemba, 2023 uwiano wa mikopo kwa sekta binafsi na pato la Taifa ni 16.3% ikilinganishwa na nchi jirani za Rwanda 22.6%, Kenya 31.8%. Aidha, kwa upande za nchi zilizoendelea, uwiano wa mikopo kwa sekta binafsi ni zaidi ya 100%. Nchi hizo ni kama vile Ufaransa 109.3%, Uingereza 120.8, Canada 124.1 na China 194.7. Takwimu hizi ni kwa mujibu wa taarifa kutoka Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inadhihirisha kuwa wananchi wengi wana mali zinazohamishika zinazoweza kutumika kama dhamana na watu wa huduma wa fedha. Hata hivyo, mfumo wa kisheria uliopo haujengi imani kwa watu wa huduma wa fedha kukopesha dhidi ya mali zinazohamishika, na hivyo wananchi wengi kushindwa kutumia mali zinazohamishika kama dhamana katika kupata mikopo yenye masharti nafuu, hali inayopelekea kuwa na ukuaji mdogo wa mikopo kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mageuzi mbalimbali ya kisera na kisheria. Kutokana na umuhimu wa sekta ya fedha katika uchumi, Serikali katika kipindi kirefu imekuwa ikifanya mageuzi mbalimbali ya kisera na kisheria ikiwa ni pamoja kuandaa sera, mipango na mikakati mbalimbali ikiwemo Sera ya Huduma Ndogo ya Fedha ya Mwaka 2017, Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya Mwaka 2003, Sera ya Taifa ya Kinga ya Jamii ya Mwaka 2023, Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wa Mwaka 2020/2021 hadi 2029/2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia uwepo wa sera, mipango na mkakati wa upatikanaji wa huduma jumuishi ya fedha wa mwaka 2023/2028, mkakati wa upatikanaji wa rasilimali fedha kwa wajasiriamali wadogo na wa kati wa mwaka 2023/2024, sheria mbalimbali pia zilitungwa ikiwemo Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania Sura 197, Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha Sura 342 Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Sura 407, Sheria ya Mikopo ya Fedha Sura 417 na Sheria ya Ufilisi Sura ya 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria nyingine ni zile zinazosimamia dhamana zinazohamishika na zilitungwa kwa malengo tofauti. Mageuzi hayo yameleta mafanikio makubwa katika sekta ya fedha ikiwa ni pamoja na kuongeza kwa mchango wa sekta ya fedha katika shughuli za kiuchumi na huduma ya jumuishi za fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwaka 2025 shughuli za huduma za fedha na bima zilikuwa 15.7% ikilinganishwa na 12.7% katika kipindi kama hicho 2024. Aidha, michango ya shughuli za huduma ya fedha na bima katika pato la Taifa ulikua kwa asilimia nne nukta tatu mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia tatu nukta tisa mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, utafiti wa *FinScope* wa 2023 umeonyesha kuongezeka kwa huduma jumuishi za fedha ambapo 76% ya nguvukazi walikuwa wanatumia huduma rasmi za kifedha katika kaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, uzoefu wa nchi nyingine. Kamati ilibaini kwamba, sheria hii siyo ya kwanza kutungwa duniani, bali kuna nchi nyingine zina sheria kama hiyo. Nchi za Afrika zilizotunga sheria hiyo ni pamoja na Ghana (2020), Zimbabwe (2017), Zambia (2016), Kenya (2017), na Nigeria (2016). Aidha, katika Bara la Asia, nchi zilizotunga sheria za usimamizi wa dhamana za mikopo kwa kutumia mali zinazohamishika ni Bangladesh (2023), China (2007) na India (2002).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hizo zilitungwa kutokana na miongozo iliyotolewa na mashirika ya Kimataifa. Mashirika hayo yalitoa miongozo mbalimbali kuhusu mageuzi na mikopo inayohusiana na mali zinazohamishika kama vile:-

(i) Sheria ya Kifani ya Usimamizi wa Dhamana za Mikopo kwa kutumia Mali Zinazohamishika ya Mwaka 1994 iliyotolewa na Benki ya Ulaya ya Maboresho na Maendeleo;

(ii) Sheria ya Kifani ya Jumuisho ya Majimbo ya Marekani *(OAS)* ya Mwaka 2002 iliyotolewa na Shirika la Majimbo ya Marekani;

(iii) Mwongozo wa Sheria ya Kamisheni ya Umoja wa Mataifa ya Sheria ya Kimataifa ya Biashara *(UNCITRAL)* ya 2007 na Sheria ya Kifani ya *UNCITRAL* kuhusu Sheria za Usimamizi wa Dhamana za Mikopo kwa Kutumia Mali Zinazohamishika ya Mwaka 2019 iliyotolewa na Kamisheni ya Umoja wa Mataifa ya Sheria za Kimataifa za Biashara; na

(iv) Zana za Shirika la Fedha Kimataifa *(IFC)* 2010 iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana katika nchi hizo yamekuwa chachu ya uandaaji wa sheria inayopendekezwa. Madhumuni ya kutungwa kwa sheria inayopendekezwa, moja, ni kutokana na changamoto za kutokuwepo kwa sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mageuzi makubwa yaliyofanyika katika sekta ya fedha nchini, moja ya changamoto katika sekta ya fedha imekuwa ni kutokuwepo kwa sheria mahsusi inayotambua haki na wajibu wa wakopeshaji na wakopaji katika miamala ya mikopo inayotumia mali zinazohamishika kama dhamana kutokana na sababu zifuatazo:-

(i) Kutokuwepo na mfumo jumuishi wa usajili wa dhamana *(centralized collateral registry)* kwa ajili ya kusajili mali zinazohamishika zinazoweza kutumika kama dhamana. Changamoto hii imepelekea matumizi ya dhamana moja kwa mikopo mbalimbali bila wakopeshaji wengine kuwa na taarifa na hivyo kusababisha ongezeko la mikopo chechefu katika sekta ya fedha;

(ii) Uwepo wa masijala mbalimbali zilizoanzishwa chini ya sheria mbalimbali. Hali hii imesababisha dhamana moja kutumika kwa mikopo mbalimbali bila wakopeshaji wengine kuwa na taarifa,

na hivyo, kusababisha ongezeko la mikopo chechefu katika sekta ya fedha;

(iii) Kukosekana kwa usimamizi na uratibu wa pamoja wa mali zinazohamishika zinazoweza kutumika kama dhamana; na

(iv) Kukosekana kwa utaratibu wa utekelezaji wa haki ya mkopaji na mkopeshaji wakati wa kuuza dhamana za mali zinazohamishika ikizingatiwa kuwa dhamana hizo zinaweza kupoteza thamani ndani ya muda mfupi au kuharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia changamoto hizo, Serikali inapendekeza kutunga sheria mahsusi ya mikopo inayotumia dhamana za mali zinazohamishika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Muswada. Muswada huu unakusudia kuweka utaratibu wa matumizi ya mali zinazohamishika katika ukopaji kwa kuwa utaratibu wa matumizi ya mali zisizohamishika kama vile ardhi, tayari mifumo ipo inayosimamia dhamana hizo. Masuala ya msingi yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni pamoja na:-

(i) Benki Kuu ya Tanzania kupewa jukumu la kusimamia masijala ya usajili wa maslahi ya dhamana ya mali zinazohamishika;

(ii) Kuweka mfumo wa usimamizi wa masijala ya usajili wa maslahi ya dhamana ya mali zinazohamishika;

(iii) Kumpa mamlaka Waziri wa Fedha kutunga kanuni zitakazotumika katika utekelezaji wa sheria inayopendekezwa;

(iv) Kuanzisha masijala ya usajili wa maslahi ya dhamana za mali zinazohamishika zilizotumika kupata mikopo kutoka kwa watoa huduma za fedha;

(v) Kuweka utaratibu wa udhibiti wa vihatarishi katika mali zinazohamishika kama vile mali kuungua moto, kuibiwa au kushuka thamani; na

(vi) Kuweka haki na wajibu wa wakopeshaji na wakopaji. Sheria zinazohusika na usajili wa maslahi ya dhamana kutoainisha haki na wajibu kwa wakopeshaji na wakopaji kama vile Sheria ya Uhamishaji Mali, Sura ya 210, Sheria ya Kampuni, Sura ya 212, Sheria ya Usajili wa Nyaraka, Sura 117, Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sura 211, Sheria ya Ufilisi, Sura ya 25 na Sheria ya Mikopo ya Fedha, Sura 417;

(vii) Kuweka hatua za kisheria zinazoweza kuchukuliwa endapo mkopaji atashindwa kulipa mkopo; na

(viii) Kuweka utaratibu wa kulinda maslahi ya dhamana za mali zinazohamishika zilizotumika kupata mkopo kutoka kwa watoa huduma za fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya kutungwa kwa sheria inayopendekezwa ni pamoja na:-

(i) Kufanya marekebisho ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197; Sheria ya Kampuni, Sura 212; Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sura 211; Sheria ya Uhamishaji Mali, Sura ya 210 ili kuwezesha sheria hizi kuendana na mashariti ya sheria inayopendekezwa;

(ii) Kuongezeka kwa watumiaji wa huduma za benki kufikia 50% mwaka 2030 kutoka 22% mwaka 2023;

(iii) Kuongezeka kwa uwiano wa mikopo kwa sekta binafsi kwa pato wa Taifa kufikia 2050 mwaka 2030 kutoka 22.5% mwaka 2024;

(iv) Kuongezeka kwa ajira;

(v) Kupungua kwa viwango vya riba; na

(vi) Kuongezeka kwa ukuaji wa sekta ya fedha kufikia 20% mwaka 2030 kutoka 17.1% mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Ibara za Muswada. Kamati ifanye uchambuzi wa Ibara za sheria zinazopendekezwa ambapo baadhi ya mapendekezo Kamati ilikubaliana nayo na maeneo mengine yalihitaji maboresho. Mapendekezo ya Kamati katika maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara zenye mapendekezo ya Kamati na ambayo Serikali ilikubali mapendekezo hayo ni Ibara ya nane ambayo inahusu mali zinazoweza kuwekwa dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara inayopendekezwa haikuwa na sharti la Gavana wa Benki Kuu kuwashirikisha wadau wa sekta ya fedha kabla ya kutangaza orodha ya mali zinazoweza kutumika kama dhamana. Hivyo, Kamati ilipendekeza Ibara ya 8(2) iboreshwe kwa kuongeza sharti ya kumtaka Gavana kufanya mashauriano na wadau wa sekta husika kabla ya kuomba ridhaa kwa Waziri na kutangaza orodha ya mali zinazoweza kutumika kama dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, sheria itakuwa imerasimisha utaratibu unaotumika katika kutangaza orodha ya mali zinazoweza kutumika kama dhamana na kuufanya kuwa shirikishi kwa wadau wote wa sekta ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Kamati ilipendekeza kuongeza ibara ndogo itakayoweka sharti za stakabadhi za ghala, mikataba ya mazao na *collateral management* kutumika kama dhamana ya mkopo. Serikali ilikubali mapendekezo yote ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara za 12, 13 na 15 kuhusu usajili wa maslahi, kipindi cha uhalali wa usajili wa maslahi, na upekuzi wa taarifa. Katika ibara hizi inakusudiwa masuala yafuatayo:-

(i) Kuweka masharti kuhusu usajili wa maslahi kwa kuzingatia utaratibu utakaoainishwa katika kanuni;

(ii) Kuainisha kipindi cha uhalali wa usajili wa masilahi kuwa ni kipindi chote kilichoainishwa katika mkataba; na

(iii) Maombi ya marekebisho au ufutaji wa usajili wa masilahi yatawasilishwa benki kwa utaratibu utakaoainishwa katika kanuni na upekuzi wa taarifa zilizoingizwa katika masijala utafanyika baada ya kuwasilisha maombi na kulipa ada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa baadhi ya utaratibu kuhusu masuala ya usajili, marekebisho au ufutaji wa usajili wa masilahi zimetajwa kwenye kanuni bila kuwa na misingi kwenye sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kamati ilipendekeza ibara hizo ziboreshwe kwa kuwa masuala ya usajili ni mahususi na ni vyema yakabainishwa katika sheria. Aidha, kwa kuwa Ibara ya 14 ilishaanza kuweka utaratibu wa marekebisho na ufutaji, ni vyema ibara ikakamilisha taratibu hizo na kuepuka kuainisha taratibu nyingine katika kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Ibara ya 12 haikuwa imeweka sharti la usajili wa dhamana kwa kuzingatia kigezo cha bima katika dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kamati ilipendekeza Ibara ya 12 iboreshwe kwa kuweka sharti la kigezo cha bima katika usajili wa dhamana ili kulinda dhamana dhidi ya vihatarishi vinavyoweza kujitokeza. Marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali ya Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 17 kuhusu masilahi katika mapato yatokanayo na dhamana dhidi ya mtu wa tatu. Ibara ya 17(2) imeweka sharti la masilahi katika dhamana yanayohusiana na

mapato ambayo hayakubainishwa wakati wa usajili, yatatekelezeka dhidi ya mtu wa tatu ndani ya siku kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa siku kumi zilizotajwa ni chache, na zinaweza kuleta changamoto katika utekelezaji hasa pale ambapo marekebisho yanapokuwa hayajafanyika. Hivyo, Kamati ilipendekeza siku hizo 10 ziongezwe kutoka siku 10 hadi siku 15 za kazi. Marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa mwenyekiti. Ibara ya 19, kipaumbele cha masilahi. Ibara ya 19(2) ilieleza kuwa utekelezaji wa kipaumbele cha masilahi katika dhamana mbili au zaidi dhidi ya mtu wa tatu kitaamuliwa kwa mpangilio bila kujali tarehe ya utengenezaji wa masilahi katika dhamana. Kamati ilipendekeza kipaumbele kiamuliwe kwa utaratibu wa tarehe kama ilivyo katika Ibara ya 19(1). Serikali ilikubaliana na mapendekezo na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 22, kipaumbele kwa mkusanyiko wa mali au bidhaa zinazoshikika zilizochanganywa. Ibara hii imeeleza kuwa thamani ya dhamana itaamuliwa kwa makubaliano ya uthamini baina ya mkopeshaji na mkopaji. Suala ambalo Kamati iliona kuwepo kwa uwezekano wa kuchochea kutokupata thamani halisi ya dhamana kwa sababu upande mmoja unaweza kuwa na nguvu ya kuamua thamani kulingana na mazingira yatakayotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, baada ya mashauriano ya kina, Serikali ilikubali kufuta Ibara ya 22(2)(b) na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 25, madai ya Serikali kupewa kipaumbele. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, maudhui ya ibara hii yanakinzana na mfumo wa kutabirika wa sheria hii katika mfumo wa vipaumbele *(predictability in priority regime)* unaosisitizwa na Tume ya Umoja wa Mataifa ya Biashara za Kimataifa *(UNCITRAL)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, baada ya mashauriano ya kina, Serikali ilikubalika kufutwa kwa ibara hii kwa kuwa kipaumbele cha masilahi cha madai ya Serikali yana kipaumbele kwa mujibu wa sheria nyingine, mfano Sheria za Kodi. Marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 28, kipaumbele dhidi ya masilahi shindani katika dhamana isiyonunuliwa. Ibara ya 28(2) ilivyokuwa awali haikuweka msisitizo kuwa kipaumbele katika dhamana isiyonunuliwa, itazingatia tarehe na muda wa usajili wa masilahi hayo ili kuepuka mgogoro unaweza kujitokeza iwapo kuna maslahi zaidi ya moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kamati ilipendekeza Ibara ibainishe kuwa itazingatia tarehe na muda wa usajili wa maslahi hayo ili kuepuka mgogoro unaoweza kujitokeza. Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 29, maslahi katika mapato ya dhamana iliyonunuliwa. Uchambuzi wa Kamati katika Ibara ya 29(2) ulibaini kuwa utekelezaji wa masharti haujazingatia usajili wa masilahi katika dhamana inayonunuliwa kwa kigezo cha tarehe na muda wa usajili wa maslahi hayo, ili kuepuka mgogoro wa wakopeshaji wakati wa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kamati ilipendekeza utekelezaji wa masharti uzingatie usajili wa maslahi katika dhamana kwa kigezo cha tarehe na muda wa usajili wa maslahi hayo ili kuepuka mgogoro unaoweza kujitokeza. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 34, uhamishaji wa dhamana. Ibara hii ilivyokuwa awali ilikuwa inabana wigo wa kuhusisha mali isiyoshikika pekee. Hivyo, Kamati ilipendekeza kuwa ni vyema ibara ikaboreshwa kwa kujumuisha mali inayoshikika katika masharti hayo.

Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na kutumia maneno "*mali inayohamishika*" badala ya maneno "*mali isiyoshikika*" katika Ibara ya 34. Marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 36, wajibu wa kutoa taarifa. Ibara hii haikuweka wazi utaratibu wa utekelezaji wa wajibu wa mkopeshaji kutoa taarifa kwa mkopaji kuhusu mwenendo wa mkopo. Aidha, ibara haikueleza, nani anaomba taarifa hiyo, Muda wa utoaji wa taarifa, na masuala yatakayokuwa kwenye taarifa ya mkopaji. Hivyo, Kamati ilipendekeza kuweka msingi wa kisheria kwa kanuni zitakazotungwa kwenye suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mashauriano, ili kuleta ufanisi, ilikubalika kuwa ni vyema masuala yote yanayohusu utaratibu yakabainishwa kwenye kanuni, kwa kuwa yanaweza kubadilika. Hivyo, Ibara ya 64(2) imeboreshwa kwa kuongeza kipengele (g) kinachohusu utaratibu wa ukaguzi wa dhamana. Marekebisho ni kama yanavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 37, jukumu la kutunza dhamana. Ibara hii haikuwa na katazo la matumizi ya dhamana pale ambapo dhamana inatunzwa na mkopeshaji. Vilevile, ibara haikuweka wazi vihatarishi vinavyoweza kuathiri dhamana na ni nani atawajibika na vihatarishi hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kamati ilipendekeza ibara hiyo kuweka katazo la matumizi ya aina yoyote ya dhamana inayoshikiliwa na mkopeshaji ili kulinda mali za wakopaji dhidi ya matumizi mabaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ibara iboreshwe kwa kuweka sharti la mkopeshaji kuwa na bima ya kutunza dhamana anazohifadhi ili kuzikinga dhidi ya vihatarishi vinavyoweza kujitokeza. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati, na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 42, ulinzi wa haki za mkopaji. Ibara inaeleza kuwa haki za mkopaji au utatuzi wa migogoro utafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu. Hata hivyo, Sheria ya Benki Kuu haina mfumo maalum wa kumlinda mkopaji dhidi ya usajili na uondoaji wa masilahi katika dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kamati ilipendekeza kuwa ni vyema sheria ikaweka sehemu mahsusi au kifungu mahsusi cha kumlinda mkopaji kama ilivyo katika Sheria Ndogo ya Fedha hususan Sehemu ya Saba Kifungu cha 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ilipendekezwa sehemu hiyo ijumuishe masharti kuhusu uwazi, usawa, wajibu wa kulinda haki ya mkopaji, namna ya kushughulikia mgogoro, taarifa kamili za mkopo, kutoa elimu kwa mkopaji na kutoa taarifa kuhusu riba, ada, tozo zinazoambatana na mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati iliitaka Serikali kuhamishia vifungu vyote vinavyohusu ulinzi wa mkopaji wakati wa usajili wa maslahi katika dhamana ya mali inayohamishika na viwekwe sehemu moja vitakavyokuwa vinaonyesha namna mkopaji na mali yake itakavyolindwa. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 45, uondoaji wa dhamana. Ibara ya 45 pamoja na mambo mengine inakusudia kuweka utaratibu wa uondoaji wa dhamana pale dhamana hiyo inapokuwa hatarini au mkopaji ameshindwa kutekeleza wajibu wake. Hata hivyo, Ibara ya tatu haikuwa imetoa tafsiri ya maneno "*dhamana kuwa hatarini*" na hivyo kuweka uwezekano wa kutumiwa vibaya. Aidha, Ibara hiyo haikuwa imeweka mazingira ambayo dhamana itatambulika kuwa hatarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kamati ilipendekeza ibara hiyo iboreshwe kwa kutafsiri maneno "*dhamana kuwa hatarini*" pamoja na kufafanua ni mazingira gani dhamana itahesabika kuwa ipo

hatarini? Kamati inaona ulinzi dhidi ya matumizi mabaya ya haki ya kuondoa dhamana ni muhimu yakabainishwa ili kumlinda mkopaji dhidi ya utashi wa mkopeshaji. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 46, utumiaji wa dhamana kutimiza wajibu wa mkopo. Pamoja na kwamba, Ibara ya 51 imeweka utaratibu wa mgawanyo wa fedha, Kamati ilibaini kuwa utaratibu huo haukidhi kikamilifu mahitaji, kwani unaweza usihusu malipo ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kamati ilipendekeza Ibara ya 46 ifafanue wazi matumizi ya fedha hizo kuwa ni fidia ya mtaji, riba iliyobaki na gharama zinazokubalika kwa mkopeshaji ili kulipa deni linalotokana na mkataba kwa kuzingatia malipo yaliyofanyika awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo hayo, Kamati ilipendekeza kufanya mabadiliko katika Ibara ya 46. Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 47, utaratibu wa uondoaji wa dhamana. Uchambuzi wa Kamati ulibaini ibara hii haikubainisha utaratibu wa kupatikana kwa bei ya thamani ya soko wakati wa uondoaji wa dhamana. Hivyo, Kamati ilipendekeza Ibara ndogo ya (2) kuboreshwa ili kutambua mifumo mingine rasmi kama vile ya mazao ya biashara na dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la mapendekezo ya Kamati ni kutoathiri mifumo hiyo katika uondoaji wa dhamana pamoja na kupata thamani ya soko. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 50, mkopeshaji kutoa taarifa ya hesabu kwa mkopaji. Ibara haikueleza kuhusu haki ya mkopaji

kuweka pingamizi dhidi ya hesabu au taarifa ya hesabu iliyotolewa na mkopeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipendekeza kuwe na haki ya pingamizi kwa mkopaji dhidi ya hesabu zilizotolewa na mkopeshaji ili kuondoa uwezekano wa mkopeshaji kutumia haki yake vibaya. Utaratibu uliopendekezwa na Kamati pia upo katika Ibara ya 14 na 53 za Muswada unaopendekezwa. Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 51, mgawanyo wa mapato baada ya uondoaji. Ibara ya 51 ilibainisha mgawanyo wa mapato mara baada ya mali inayohamishika kuuzwa ili kurejesha mkopo. Hata hivyo, ibara hiyo haikuweka mgawanyo wa mapato yatakayotokana na mali iliyouzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipendekeza ibara hii iboreshwe ili kuweka sharti la kuwasilisha bakaa au kiasi kitakachokuwa kimezidi baada ya mkopo na riba kulipwa. Aidha, endapo kutakuwa na mgogoro, kiasi hicho kiwekwe kwenye akaunti ya Mahakama ili kisubiri uamuzi utakapofanyika. Serikali ilikubaliana kufuta na kuandika upya Ibara ya 51(3) kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 54, ukomboaji wa dhamana. Ibara hii haikuwa imebainisha aina ya gharama nyingine zinazokusudiwa kurejeshwa na mkopeshaji kuhusiana na dhamana hiyo husika. Hivyo, Kamati ilipendekeza kuweka sharti kwa mkopeshaji kubainisha aina zote za gharama ili kuepusha mkopeshaji kuongeza gharama zisizohusiana na mkopo. Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 61, rufaa. Ibara hii haikueleza kuhusu haki ya kukata rufaa Mahakamani kwa mtu ambaye hajaridhika na uamuzi wa Waziri. Hivyo, Kamati ilipendekeza ibara

iboreshwe ili kubainisha endapo mtu hajaridhika na maamuzi ya Waziri, atawasilisha shauri la marejeo Mahakamani *(judicial review)*. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla. Pamoja na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwenye ibara mbalimbali za Muswada, Kamati ina maoni ya jumla yafuatayo:-

(i) Elimu ya wakopaji kabla ya kupewa mikopo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto kuu iliyowakabili wakopaji katika sekta ndogo ya fedha ni elimu duni ya mikopo na matumizi yake. Pamoja na kuwa Kifungu cha 52(e) cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha, Sura 407, kinawataka wakopeshaji wote kutoa elimu ya kina kuhusu mikopo, riba, faini, uwazi wa gharama, ulinzi wa mlaji, utunzaji wa taarifa na taratibu za kushughulikia malalamiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kwamba kifungu hicho hakitekelezwi ama kwa lengo la kutokuwapa wakopaji taarifa kamili wanayohitaji ili kukopa au kutokana na mahitaji ya fedha kwa wakopaji yanayosababisha wasizingatie takwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba wakopeshaji wote katika huduma ndogo za fedha wanatekeleza takwa hilo ili kuondoa madhila yanayowakumba wakopaji.

(ii) Wakopeshaji kutokufuata masharti ya Sheria ya Ukopaji kwa Dhamana na Mali Zinazohamishika ya Mwaka 2016;

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutungwa kwa Sheria hii pamoja na mambo mengine, kunaziba ombwe lililokuwepo la wakopeshaji kukopesha kwa kutumia mali zinazohamishika bila utaratibu. Pamoja na kwamba Kamati imehakikisha kwamba Sheria inamlinda mkopaji

dhidi ya uuzaji wa mali yake bila idhini yake au utaratibu, bado changamoto itabaki katika usimamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Wizara ya Fedha kupitia Benki Kuu, kusimamia kikamilifu masharti ya sheria hii ili kudhibiti matumizi mabaya yatakayojitokeza. Aidha, wakopeshaji wote ambao watatumia mali ambazo hazijasajiliwa, kuchukuliwa hatua kali ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa leseni zao kama sheria inavyotaka.

(iii) Uanzishaji wa klabu za masuala ya mikopo shuleni;

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba mikopo ni sehemu muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi, bado suala la mikopo halipewi kipaumbele katika mitaala yetu. Imekuwa ni kawaida kwa baadhi ya Watanzania kukopa kwa ajili ya kufanya sherehe au kutunza mtu kwenye sherehe. Matokeo yake Watanzania wengi wamekuwa wakijikuta katika matatizo makubwa ya kushindwa kurejesha mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali ilishaandaa mtaala mpya na inaweza ikawa suala gumu kufanya mabadiliko, hivyo Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu kuhakikisha wanahamasisha uanzishwaji wa klabu za masuala ya mikopo kuanzia shule ya msingi hadi sekondari. Aidha, vikao vya vijiji na mitaa viwe na ajenda ya kuwapa wananchi elimu kuhusu mikopo. Hatua hizi kwa pamoja zikitekelezwa, zitaepusha changamoto nyingi tulizonazo hivi sasa.

(iv) Changamoto za biashara kufanyika nje ya mfumo usio rasmi;

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanyika kwa biashara nje ya mfumo rasmi, kumesababisha changamoto mbalimbali kama vile kutokuwa na kumbukumbu rasmi za biashara, taarifa za mapato, uthibitisho wa umiliki wa mali na historia ya mikopo. Changamoto hizi kwa

pamoja zinaweza kusababisha wafanyabiashara wadogo washindwe kupata mikopo kutoka katika taasisi za fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo masharti yatakayowekwa kwenye kanuni kuhusu utaratibu wa uthibitishaji wa umiliki wa mali zinazohamishika yawe rahisi kwa Watanzania wote ili sheria inayopendekezwa iweze kufikia lengo la kuongeza upatikanaji wa mikopo na mitaji kwa Watanzania wanaomiliki na kuendesha biashara ndogo zilizo nje ya mfumo rasmi.

(v) Utungaji wa kanuni zinazoendana na lengo la sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto ambayo Kamati ilikutana nayo wakati wa kujadili sheria hii, ni ufafanuzi wa baadhi ya maeneo yanayopendekezwa kufanyika kupitia kanuni. Hivyo, Kamati inasisitiza, kanuni zitakazoandaliwa ziende sambamba na maudhui, malengo na madhumuni ya sheria iliyotungwa ili kurahisisha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuhitimisha kwa kumshukuru Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Spika wa Bunge la Tanzania, pamoja na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru pia Mheshimiwa Balozi Khamis Mussa Omar, Waziri wa Fedha; Mheshimiwa Hamza S. Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mheshimiwa Mhandisi Mshamu Ali Munde, Naibu Waziri wa Fedha; na Mheshimiwa Laurent Deogratius Luswetula, Naibu Waziri Fedha kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wa kuchambua Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali Zinazohamishika wa Mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninapenda kumshukuru Dkt. Natu El-maamry Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali; Ndugu Elijah Mwandumbya na Ndugu Msibiri A. K. Joshua, Naibu Makatibu Wakuu wa Wizara ya Fedha; Ndugu Emmanuel M. Tutuba, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania; na Bi.

Dionisia Mjema, Kaimu Kamishna wa Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, niwashukuru Makamishna, Wakuu wa Taasisi, na Wataalamu wote katika Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pamoja na Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati katika kipindi chote cha kuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwapongeza Wajumbe wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao wakati wote, na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Ninaomba kuwatambua Wajumbe hao kama wanavyoonekana kwenye taarifa hii ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nimshukuru Ndugu Baraka Leonard, Katibu wa Bunge kwa niaba ya watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha, na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MIKOPO KWA DHAMANA ZA MALI ZINAZOHAMISHIKA WA MWAKA 2026 *[SECURED TRANSACTION OF MOVABLE PROPERTIES ACT, 2026]* – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102(1)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025 ikisomwa pamoja na kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Bajeti Sura 439, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria

ya Mikopo kwa Dhamana za Mali Zinazohamishika wa Mwaka 2026 (Secured Transaction of Movable Properties Act, 2026).

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 100(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, Kamati ilikutana na wadau tarehe 28 na 29 Aprili, 2026 ambapo ilipokea maoni yao kuhusu Muswada. Jumla ya wadau 5 walifika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao. Naomba niwatambue wadau hao kama ifuatavyo:- Tanzania Bankers Association (TBA), Tanzania Association of Micro Finance Institutions (TAMFI), Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) na Imarika Microfinance. Aidha, Kamati ilipokea maoni kupitia barua pepe kutoka kwa Nyembe Group of Entities, Wadau kutoka Wilaya ya Vunjo na mdau binafsi mmoja. Maoni hayo yaliisaidia Kamati katika uchambuzi, kuboresha na kufanya maamuzi kwa maslahi mapana ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umekuja wakati muafaka hasa ukizingatia kuwa taasisi za fedha nchini zilikuwa tayari zinakopesha kwa kutumia mali zinazohamishika (movable assets/properties) kama dhamana kwa mikopo lakini bila ya kuwa na misingi rasmi ya **kisheria**. Taarifa hii inatoa mrejesho wa mashauriano kati ya Kamati na Serikali kuhusiana na Muswada unaopendekezwa kutungwa. Muswada huo umegawanyika katika sehemu kuu **kumi (10)** zenye jumla ya **Ibara 79**.

1.1. Muundo wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu saba (7). Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya Pili ni Chimbuko la Muswada; Sehemu ya Tatu ni Hali ya Sekta ya Fedha Nchini; Sehemu ya Nne ni Uchambuzi wa Ibara za Muswada; Sehemu ya Tano ni Maoni ya Ujumla na mwisho ni Hitimisho.

2.0. CHIMBUKO LA MUSWADA

2.1. Hali ya Upatikanaji wa Mikopo Nchini

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya uchumi wa nchi yanategemea mfumo thabiti wa sekta ya fedha wenye ufanisi unaohakikisha kunakuwepo na ukwasi wa kutosha katika kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi.

Utafiti wa Soko la Mikopo hapa nchini uliofanywa na *Financial Sector Deepening Africa* kwa kushirikiana na *Financial Sector Deepening Trust* (FSDT) ulibainisha aina za mali zinazotumiwa kama dhamana na watoa huduma wa fedha. Kwa mujibu wa matokeo ya Utafiti huo, mali zinazohamishika ndiyo aina ya dhamana inayoongoza kutumiwa na taasisi za benki ambayo ilichangia zaidi ya **asilimia 46** ya dhamana zote.

Mheshimiwa Spika, matokeo hayo ya utafiti yanaonesha kuwa kuna fursa kubwa ya kutumia mali zinazohamishika zinazomilikiwa na watu binafsi na kupata mikopo endapo kutakuwepo na mfumo madhubuti wa usajili wa maslahi katika mali zinazohamishika zilizotumika kama dhamana kupata mkopo kutoka kwa watoa huduma za fedha.

Mheshimiwa Spika, dhamana za mikopo zinazokubalika katika sekta ya fedha hivi sasa ni mali zisizohamishika mfano ardhi. Utafiti wa Finscope, 2023 umeonesha kuwa **asilimia 3** ya wananchi wana hatimiliki rasmi za umiliki wa ardhi nchini. Kutokana na hali hiyo wananchi wengi wanakosa sifa ya kupata mkopo yenye masharti nafuu kutoka benki na taasisi za fedha.

Mheshimiwa Spika, hali hii imesababisha upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi kuwa wa kiwango cha chini. Hadi Desemba 2023, uwiano wa mikopo kwa sekta binafsi na Pato la Taifa ni **asilimia 16.3** ikilinganishwa na nchi jirani za Rwanda **(asilimia 22.6)** na Kenya **(asilimia 31.8).** Aidha, kwa upande wa nchi zilizoendelea uwiano wa mikopo kwa sekta binafsi ni zaidi ya **asilimia 100**. Nchi hizo ni kama

vile Ufaransa **(asilimia 109.3)**, Uingereza **(asilimia 120.8)**, Canada **(asilimia 124.1)** na China **(asilimia 194.7)**. Takwimu hizi ni kwa mujibu wa taarifa kutoka Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, hali hii inadhihirisha kuwa wananchi wengi wana mali zinazohamishika zinazoweza kutumika kama dhamana na watoa huduma za fedha. Hata hivyo, mfumo wa kisheria uliopo haujengi imani kwa watoa huduma za fedha kukopesha dhidi ya mali zinazohamishika na hivyo wananchi wengi kushindwa kutumia mali zinazohamishika kama dhamana katika kupata mikopo yenye masharti nafuu hali inayopelekea kuwa na ukuaji mdogo wa mikopo kwa sekta binafsi.

2.2. Mageuzi mbalimbali ya Kisera na Kisheria

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa sekta ya fedha katika uchumi Serikali katika kipindi kirefu imekuwa ikifanya mageuzi mbalimbali ya kisera na kisheria ikiwa ni pamoja na kuandaa Sera, Mipango na Mikakati mbalimbali ikiwemo; Sera ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2017; Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2003; Sera ya Taifa ya Kinga ya Jamii ya mwaka 2023; Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha (2020/2021-2029/2030);

Mkakati wa Upatikanaji wa Huduma Jumuishi za Fedha 20232028; Mkakati wa Upatikanaji wa Rasilimali Fedha kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati wa 2023/24.

Mheshimiwa Spika, kufuatia uwepo wa Sera, Mipango na Mikakati hiyo Sheria mbalimbali pia zilitungwa ikiwemo Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197, Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342; Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha, Sura ya 407; Sheria ya Mikopo ya Fedha, Sura ya 417 na Sheria ya Ufilisi Sura ya 25. Sheria nyingine ni zile zinazosimamia dhamana zinazohamishika na zilitungwa kwa malengo tofauti.

Mheshimiwa Spika, mageuzi hayo yameleta mafanikio makubwa katika sekta ya fedha ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa

mchango wa Sekta ya Fedha katika shughuli za kiuchumi na huduma jumuishi za fedha. Hadi mwaka 2025 shughuli za huduma za fedha na bima zilikua kwa **asilimia 15.7** ikilinganishwa na **asilimia 12.7** katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha, mchango wa shughuli za huduma za fedha na bima katika Pato la Taifa ulikuwa **asilimia 4.3** mwaka 2025 ikilinganishwa na **asilimia 3.9** mwaka 2024. Vile vile, Utafiti wa FinScope wa 2023, umeonesha kuongezeka kwa huduma jumuishi za fedha, ambapo **asilimia 76** ya nguvukazi walikuwa wanatumia huduma rasmi za kifedha katika kaya.

2.3. Uzoefu wa Nchi Nyingine

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kwamba sheria hii si ya kwanza kutungwa duniani bali kuna nchi nyingine zina sheria kama hiyo. Nchi za Afrika zilizotunga sheria hiyo ni pamoja na: Ghana (2020), Zambia (2016), Zimbabwe (2017), Nigeria (2016) na Kenya (2017). Aidha, katika Bara la Asia, nchi zilizotunga sheria za usimamizi wa dhamana za mikopo kwa kutumia mali zinazohamishika ni China (2007), Bangladesh (2023) na India (2002).

Mheshimiwa Spika, Sheria hizo zilitungwa kutokana na miongozo iliyotolewa na Mashirika ya Kimataifa. Mashirika hayo yalitoa miongozo mbalimbali kuhusu mageuzi ya mikopo inayohusisha mali zinazohamishika kama vile:-

i. Sheria Kifani ya Usimamizi wa Dhamana za Mikopo kwa kutumia Mali Zinazohamishika ya Mwaka 1994 iliyotolewa na Benki ya Ulaya ya Maboresho na Maendeleo;

ii. Sheria Kifani ya Jumuiya ya Majimbo ya Marekani (OAS) ya Mwaka 2002 iliyotolewa na Shirika la Majimbo ya Marekani;

iii. Mwongozo wa Sheria wa Kamisheni ya Umoja wa Mataifa ya Sheria za Kimataifa za Biashara (UNCITRAL) 2007 na Sheria ya Kifani ya UNCITRAL kuhusu sheria za usimamizi wa dhamana za mikopo kwa kutumia mali zinazohamishika ya

mwaka 2019 iliyotolewa na Kamisheni ya Umoja wa Mataifa ya Sheria za Kimataifa za Biashara; na

iv. Zana za Shirika la Fedha Kimataifa (IFC), 2010 iliyotolewa na Shirika la Fedha Kimataifa na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatika katika nchi hizo ndio yamekuwa chachu ya uaandaji wa Sheria hii inayopendekezwa.

Madhumuni ya Kutungwa kwa Sheria Inayopendekezwa

2.4.1. Changamoto za kutokuwepo kwa Sheria inayopendekezwa

Mheshimiwa Spika, pamoja na mageuzi makubwa yaliyofanyika katika sekta ya fedha nchini, moja ya changamoto katika Sekta ya Fedha imekuwa ni kutokuwepo sheria mahsusi inayotambua haki na wajibu wa wakopeshaji na wakopaji katika miamala ya mikopo inayotumia mali zinazohamishika kama dhamana kutokana na sababu zifuatazo:-

i. Kutokuwepo na mfumo jumuishi ya usajili wa dhamana *(centralized collateral registry)* kwa ajili ya kusajili mali zinazohamishika zinazoweza kutumika kama dhamana.

Changamoto hii imepelekea matumizi ya dhamana moja kwa mikopo mbalimbali bila ya wakopeshaji wengine kuwa na taarifa na hivyo kusababisha ongezeko la mikopo chechefu katika sekta ya fedha;

ii. Uwepo wa masijala mbalimbali zilizoanzishwa chini ya sheria mbalimbali. Hali hii imesababisha dhamana moja kutumika kupata mikopo mbalimbali bila wakopeshaji wengine kuwa na taarifa, hivyo, kusababisha ongezeko la mikopo chechefu katika sekta ya fedha;

iii. Kukosekana kwa usimamizi na uratibu wa pamoja wa mali zinazohamishika zinazoweza kutumika kama dhamana; na

iv. Kukosekana kwa utaratibu wa utekelezaji wa haki za mkopaji na mkopeshaji wakati wa kuuza dhamana za mali zinazohamishika ikizingatiwa kuwa dhamana hizo zinaweza kupoteza thamani ndani ya muda mfupi au kuharibika.

Mheshimiwa Spika, kufuatia changamoto hizo, Serikali inapendekeza kutunga Sheria mahsusi ya mikopo inayotumia dhamana za mali zinazohamishika.

2.4.2. Madhumuni ya Muswada

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unakusudia kuweka utaratibu wa matumizi ya mali zinazohamishika katika ukopaji kwa kuwa utaratibu wa matumizi ya mali zisizohamishika kama vile ardhi tayari mifumo ipo inayosimamia dhamana hizo. Masuala ya msingi yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni pamoja na:-

i. Benki Kuu ya Tanzania kupewa jukumu la kusimamia masijala ya usajili wa maslahi ya dhamana za mali zinazohamishika;

ii. Kuweka mfumo wa usimamizi wa Masijala ya usajili wa maslahi ya dhamana za mali zinazohamishika;

iii. Kumpa mamlaka Waziri wa Fedha kutunga kanuni zitakazotumika katika utekelezaji wa sheria inayopendekezwa;

iv. Kuanzisha Masijala ya usajili wa maslahi ya dhamana za mali zinazohamishika zilizotumika kupata mkopo kutoka kwa watoa huduma za fedha;

v. Kuweka utaratibu wa udhibiti wa vihatarishi katika mali zinazohamishika kama vile mali kuungua moto, kuibiwa na kushuka thamani;

vi. Kuweka haki na wajibu wa wakopeshaji na wakopaji. Sheria zinazohusika na usajili wa maslahi ya dhamana kutoainisha haki na wajibu wa wakopeshaji na wakopaji kama vile Sheria ya Uhamishaji Mali, Sura ya 210, Sheria ya Kampuni, Sura ya 212, Sheria ya Usajili wa Nyaraka, Sura ya 117, Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sura ya 211, Sheria ya Ufilisi Sura ya 25 na Sheria ya Mikopo ya Fedha, Sura ya 417;

vii. Kuweka hatua za kisheria zinazoweza kuchukuliwa endapo mkopaji atashindwa kulipa mkopo; na

viii. Kuweka taratibu za kulinda maslahi ya dhamana za mali zinazohamishika zilizotumika kupata mkopo kutoka kwa watoa huduma za fedha.

2.4.3. Matokeo ya kutungwa kwa Sheria inayopendekezwa

Mheshimiwa Spika, matokeo ya kutungwa kwa sheria hii ni pamoja na:

i. Kufanya marekebisho ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197, Sheria ya Kampuni, Sura ya 212, Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sura ya 211, na Sheria ya Uhamishaji Mali, Sura ya 210 ili kuwezesha sheria hizi kuendana na masharti ya sheria inayopendekezwa;

ii. Kuongezeka kwa watumiaji wa huduma za benki na kufikia **asilimia 50** mwaka 2030 kutoka **asilimia 22** kwa mwaka 2023;

iii. Kuongezeka kwa uwiano wa mikopo kwa sekta binafsi kwa Pato la Taifa na kufikia **asilimia 50** kwa mwaka 2030 kutoka **asilimia 22.5** kwa mwaka 2024; iv. Kuongezeka kwa ajira;

v. Kupungua kwa viwango vya riba; na

vi. Kuongezeka kwa ukuaji wa sekta ya fedha na kufikia **asilimia 20** mwaka 2030 kutoka **asilimia 17.1** mwaka 2024.

3.0. UCHAMBUZI WA IBARA ZA MUSWADA

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa Ibara za Sheria zinazopendekezwa ambapo baadhi ya mapendekezo, Kamati ilikubaliana nayo na maeneo mengine yalihitaji maboresho. Mapendekezo ya Kamati katika maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

3.1. Ibara zenye mapendekezo ya Kamati na Serikali ilikubali mapendekezo hayo.

3.1.1. Ibara ya 3 - Fasili

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 3 ya Muswada inatoa fasili ya maneno mbalimbali yanayotumika katika sheria. Hata hivyo, maneno "Maslahi katika dhamana", "Maslahi katika dhamana inayonunuliwa" na "Maslahi katika dhamana isiyonunuliwa" hayakuwa yamepatiwa fasili fasaha. Hivyo, Kamati ilipendekeza maneno hayo yapate fasili fasaha bila kurudia neno maslahi ili kuondoa changamoto katika matumizi. Serikali ilikubali mapendekezo hayo na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho ya Serikali.

3.1.2. Ibara ya 4 - Uanzishwaji wa Masijala

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 4 inapendekeza kuanzisha masijala ndani ya Benki Kuu ya Tanzania ambayo itajulikana kama Masijala ya Dhamana na kuipa Benki Kuu ya Tanzania mamlaka ya usimamizi wa utendaji kazi wa masijala hiyo. Hata hivyo, Kamati iliona kuwa jukumu la usajili wa dhamana alilopewa Benki Kuu linaweza lisitekelezwe kwa ufanisi kutokana na majukumu makubwa ambayo Benki inayo na maeneo ambayo Benki Kuu inaweza kufika kutoa huduma hiyo. Vilevile, imeonekana kuwa kunaweza kujitokeza mgongano wa kimaslahi kwa kuwa Benki Kuu ni sehemu ya usajili na msimamizi.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Kamati ilipendekeza Ibara iboreshwe kwa kuiondoa Masijala ndani ya Benki Kuu na badala yake kuwe na taasisi maalumu ambayo itahusika na masijala ya dhamana na Ibara itamke bayana kuhusu uwepo wa nafasi ya Msajili wa Dhamana. Hata hivyo, Serikali kwa kushauriana na Kamati ilikubalika Ibara hiyo ibaki kama ilivyo kwa sababu Benki Kuu ya Tanzania, kama msimamizi wa sekta ya fedha ina uwezo na mamlaka ya kuhakikisha usimamizi uendeshaji na uadilifu wa Masijala ya Dhamana pamoja na kuwezesha ufanisi katika usajili na ufuatiliaji wa dhamana zinazotolewa kwa ajili ya kupata mikopo.

Mheshimiwa Spika, uamuzi huo wa Kamati ulizingatia kuwa Benki Kuu ina mifumo imara ya usimamizi, ikiwemo mifumo ya malipo na mifumo ya kubadilishana taarifa za wakopaji. Kwa hiyo, kupewa jukumu la kusimamia masijala ya dhamana zinazohamishika kutaimarisha ufanisi wa soko la mikopo, usalama wa taarifa, muunganiko wa mifumo, na kupunguza vihatarishi katika utoaji wa mikopo. Aidha, Serikali ilikubali suala la ukasimishaji wa majukumu ya Benki Kuu. Marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho ya Serikali.

3.1.3. Ibara ya 8 - Mali zinazoweza kuwekwa dhamana

Mheshimiwa Spika, Ibara inayopendekezwa haikuwa na sharti la Gavana wa Benki Kuu kuwashirikisha Wadau wa sekta ya fedha kabla ya kutangaza orodha ya mali zinazoweza kutumika kama dhamana. Hivyo, Kamati ilipendekeza **Ibara 8(2)** iboreshwe kwa kuongeza sharti la kumtaka Gavana kufanya mashauriano na wadau wa sekta husika kabla ya kuomba ridhaa kwa Waziri na kutangaza orodha ya mali zinazoweza kutumika kama dhamana. Kwa kufanya hivyo, sheria itakuwa imerasimisha utaratibu unaotumika katika kutangaza orodha ya mali zinazoweza kutumika kama dhamana na kuufanya kuwa shirikishi kwa wadau wote wa sekta ya fedha.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati ilipendekeza kuongeza Ibara ndogo itakayoweka sharti la stakabadhi za ghala, mikataba ya

mazao na 'collateral Management' kutumika kama dhamana ya mkopo. Serikali ilikubali mapendekeo yote ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho ya Serikali.

3.2. Ibara za 12,13 na 15 - Usajili wa Maslahi, Kipindi cha Uhalali wa Usajili wa Maslahi na Upekuzi wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, katika Ibara hizi Serikali inakusudia masuala yafuatayo:-

i. kuweka masharti kuhusu usajili wa maslahi kwa kuzingatia utaratibu utakaoainishwa katika Kanuni;

ii. kuainisha kipindi cha uhalali wa usajili wa maslahi kuwa ni kipindi chote kilichoainishwa katika Mkataba; na

iii. maombi ya marekebisho au ufutaji wa usajili wa maslahi yatawasilishwa Benki kwa utaratibu utakaoainishwa katika Kanuni na upekuzi wa taarifa zilizoingizwa katika Masijala utafanyika baada ya kuwasilisha maombi na kulipa ada.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa baadhi ya taratibu kuhusu masuala ya usajili, marekebisho au ufutaji wa usajili wa maslahi zimetajwa kwenye kanuni bila ya kuwa na misingi kwenye sheria. Hivyo, Kamati ilipendekeza ibara hizo ziboreshwe kwa kuwa masuala ya usajili ni mahsusi na ni vyema yakabainishwa katika sheria. Aidha, kwa kuwa **Ibara ya 14** ilishaanza kuweka utaratibu wa marekebisho na ufutaji ni vyema Ibara ikakamilisha taratibu hizo na kuepuka kuainisha taratibu nyingine katika kanuni.

Mheshimiwa Spika, vilevile, **Ibara ya 12** haikuwa imeweka sharti la usajili wa dhamana kwa kuzingatia kigezo cha bima katika dhamana. Hivyo, Kamati ilipendekeza **Ibara ya 12** iboreshwe kwa kuweka sharti la kigezo cha bima katika usajili wa dhamana ili kulinda dhamana dhidi ya vihatarishi vinavyoweza kujitokeza.

Marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho ya Serikali.

3.2.1. Ibara ya 17 - Maslahi katika mapato yatokanayo na dhamana dhidi ya mtu wa tatu

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 17 (2) imeweka sharti la Maslahi katika dhamana yanayohusiana na mapato ambayo hayakubainishwa wakati wa usajili, yatatekelezeka dhidi ya mtu wa tatu ndani ya siku kumi. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa siku 10 zilizotajwa ni chache na zinaweza kuleta changamoto katika utekelezaji hasa pale ambapo marekebisho ya usajili yanapokuwa hayajafanyika.

Hivyo, Kamati ilipendekeza siku hizo ziongezwe kutoka siku **10** hadi siku **15** za kazi. Marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho ya Serikali.

3.2.2. Ibara ya 19 - Kipaumbele cha maslahi

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 19 (2) inaeleza kuwa utekelezaji wa kipaumbele cha maslahi katika dhamana mbili au zaidi dhidi ya mtu wa tatu kitaamuliwa kwa mpangilio bila kujali tarehe ya utengenezaji wa maslahi katika dhamana. Kamati ilipendekeza kipaumbele kiamuliwe kwa utaratibu wa tarehe kama ilivyo katika **Ibara ya 19 (1)**. Serikali ilikubali mapendekeo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho ya Serikali.

3.2.3. Ibara ya 22 - Kipaumbele kwa mkusanyiko wa mali au bidhaa zinazoshikika zilizochanganywa

Mheshimiwa Spika, Ibara hii imeeleza kuwa thamani ya dhamana itaamuliwa kwa makubaliano ya uthamini baina ya mkopeshaji na mkopaji suala ambalo Kamati iliona kuwepo kwa uwezekano wa kuchochea kutopata thamani halisi ya dhamana kwa sababu upande mmoja unaweza kuwa na nguvu ya kuamua thamani kulingana na mazingira yatakayotokea. Hivyo, baada ya

mashaurino ya kina na Serikali ilikubalika kufutwa kwa **Ibara 22(2**)(b) na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho ya Serikali.

3.2.4. Ibara ya 25 - Madai ya Serikali kupewa kipaumbele

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa maudhui ya Ibara hii yanakinzana na mfumo wa kutabirika kwa Sheria hii katika Mfumo wa Vipaumbele (predictability in priority regime) unaosisitizwa na Tume ya Umoja wa Mataifa ya Biashara za Kimataifa (*UNICITRAL*). Hata hivyo, baada ya mashauriano ya kina na Serikali ilikubalika kufutwa kwa Ibara hii kwa kuwa kipaumbele cha maslahi cha madai ya Serikali yana kipaumbele kwa mujibu wa sheria zingine mfano Sheria za Kodi. Marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho ya Serikali.

3.2.5. Ibara ya 27 - Maslahi shindani katika dhamana inayouzwa

Mheshimiwa Spika, maneno "maslahi shindani" yaliyotumika katika Ibara hii haikuwa imetafsiriwa katika **Ibara ya 3** na hivyo kuleta mkanganyiko katika matumizi. Hivyo, Kamati ilipendekeza tafsiri ya maneno "maslahi shindani" yaliyotumika katika maudhui ya Ibara kutafsiriwa katika **Ibara ya 3** ili kuondoa mkanganyiko unaoweza kujitokeza. Serikali ilikubali mapendekeo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho ya Serikali.

3.2.6. Ibara ya 28 - Kipaumbele dhidi ya maslahi shindani katika dhamana isiyonunuliwa

Mheshimiwa Spika, **Ibara ya 28 (2)** ilivyokuwa awali haikuweka msisitizo kuwa kipaumbele katika dhamana isiyonunuliwa itazingatia tarehe na muda wa usajili wa maslahi hayo ili kuepuka mgogoro unaoweza kujitokeza iwapo kuna maslahi zaidi ya moja. Hivyo, Kamati ilipendekeza Ibara ibainishe kuwa itazingatia tarehe na muda wa usajili wa maslahi hayo ili kuepuka mgogoro unaoweza kujitokeza. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho la Serikali.

3.2.7. Ibara ya 29 - Maslahi katika mapato ya dhamana inayonunuliwa

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati katika **Ibara ya 29 (2)** ulibaini kuwa utekelezaji wa masharti haujazingatia usajili wa maslahi katika dhamana inayonunuliwa kwa kigezo cha tarehe na muda wa usajili wa maslahi hayo ili kuepuka mgogoro wa wakopeshaji wakati wa utekelezaji. Hivyo, Kamati ilipendekeza utekelezaji wa masharti uzingatie usajili wa maslahi katika dhamana kwa kigezo cha tarehe na muda wa usajili wa maslahi hayo ili kuepuka mgogoro unaoweza kujitokeza. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho ya Serikali.

3.2.8. Ibara ya 34 - Uhamishaji wa dhamana

Mheshimiwa Spika, Ibara hii ilivyokuwa awali ilikuwa inabana wigo kwa kuhusisha mali isiyoshikika pekee. Hivyo, Kamati ilipendekeza kuwa ni vyema Ibara ikaboreshwa kwa kujumuisha mali inayoshikika katika masharti hayo. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na kutumia maneno "mali inayohamishika" badala ya maneno "mali isiyoshikika" katika **Ibara ya 34**. Marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho ya Serikali.

3.2.9. Ibara ya 35 - Haki ya kukagua dhamana

Mheshimiwa Spika, Ibara hii imetoa haki kwa mkopeshaji ya kukagua dhamana hata hivyo haijafafanua namna ambavyo Mkopeshaji atatekeleza haki hiyo bila kusababisha usumbufu usio wa lazima kwa mkopaji. Kamati iliona kama Ibara hii ikiachwa jinsi ilivyo kuna uwezekano wa kuvuruga shughuli za kawaida za mkopaji. Hivyo, Kamati ilipendekeza kuweka sharti la utoaji wa notisi, muda na namna ya ukaguzi pamoja na ukomo wa utekelezaji wa haki hiyo ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima wakati wa utekelezaji wa haki hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya mashauriano ili kuleta ufanisi ilikubalika kuwa ni vyema masuala yote yanayohusu utaratibu

yakabainishwa kwenye Kanuni kwa kuwa yanaweza kubadilika. Hivyo, **Ibara ya 64(2)** imeboreshwa kwa kuongeza **kipengele (f)** kinachohusu utaratibu wa ukaguzi wa dhamana. Marekebisho ni kama yanavyoonekana kwenye Jedwali la marekebisho ya Serikali.

3.2.10. Ibara ya 36 - Wajibu wa kutoa taarifa

Mheshimiwa Spika, Ibara hii haikuweka wazi utaratibu wa utekelezaji wa wajibu kwa mkopeshaji kutoa taarifa kwa mkopaji kuhusu mwenendo wa mkopo. Aidha, Ibara haikueleza nani anaomba taarifa hiyo, muda wa utoaji wa taarifa na masuala yatakayokuwa kwenye taarifa ya mkopaji. Hivyo, Kamati ilipendekeza kuweka msingi wa kisheria kwa kanuni zitakazotungwa kwenye suala hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya mashauriano ili kuleta ufanisi ilikubalika kuwa ni vyema masuala yote yanayohusu utaratibu yakabainishwa kwenye Kanuni kwa kuwa yanaweza kubadilika. Hivyo, **Ibara ya 64(2)** imeboreshwa kwa kuongeza **kipengele (g)** kinachohusu utaratibu wa ukaguzi wa dhamana. Marekebisho ni kama yanavyoonekana kwenye Jedwali la marekebisho ya Serikali.

3.2.11. Ibara ya 37 - Jukumu la kutunza dhamana

Mheshimiwa Spika, Ibara hii haikuwa na katazo la matumizi ya dhamana pale ambapo dhamana inatunzwa na mkopeshaji. Vilevile, Ibara haikuweka wazi vihatarishi vinavyoweza kuathiri dhamana na ni nani atawajibika na vihatarishi hivyo. Hivyo, Kamati ilipendekeza ibara hiyo kuweka katazo la matumizi ya aina yoyote ya dhamana inayoshikiliwa na mkopeshaji ili kulinda mali za wakopaji dhidi ya matumizi mabaya. Aidha, Ibara iboreshwe kwa kuweka sharti kwa mkopeshaji kuwa na bima ya kutunza dhamana anazohifadhi ili kuzikinga dhidi ya vihatarishi vinavyoweza kujitokeza. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho ya Serikali.

3.2.12. Ibara ya 38 - Haki ya mdaiwa kuomba uthibitisho au kukataa deni

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa maudhui ya Ibara hii na maneno ya pembeni yalikuwa hayaendani, hivyo ilipendekezwa maneno ya pembeni yarekebishwe kuendana na maudhui ya ibara hiyo. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho ya Serikali.

3.2.13. Ibara ya 42 - Ulinzi wa haki za mkopaji

Mheshimiwa Spika, Ibara inaeleza kuwa haki za mkopaji au utatuzi wa migogoro utafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu. Hata hivyo, Sheria ya Benki Kuu haina mfumo maalumu wa kumlinda mkopaji dhidi ya usajili na uondoshaji wa maslahi katika dhamana. Hivyo, Kamati ilipendekeza kuwa ni vyema sheria ikaweka sehemu mahsusi au kifungu mahususi cha kumlinda mkopaji kama ilivyo katika Sheria ya Sekta Ndogo za Fedha hususani **Sehemu ya Saba, Kifungu cha 50**.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ilipendekezwa sehemu hiyo ijumuishe masharti kuhusu uwazi, usawa, wajibu wa kulinda haki za mkopaji, namna ya kushughulikia migogoro, taarifa kamili ya mkopo, kutoa elimu kwa mkopaji na taarifa ya wazi kuhusu riba, ada na tozo zinazoambatana na mkopo. Aidha, Kamati iliitaka Serikali kuhamishia vifungu vyote vinavyohusu ulinzi wa mkopaji wakati wa usajili wa maslahi katika dhamana ya mali inayohamishika na viwekwe sehemu moja vitakavyokuwa vinaonyesha namna mkopaji na mali yake itakavyolindwa. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho ya Serikali.

3.2.14. Ibara ya 44 - Usajili wa taarifa ya utekelezaji

Mheshimiwa Spika, Ibara hii haikuweka ukomo wa muda ambao Benki Kuu itatakiwa kutoa idhini kwa mkopeshaji kuchukua hatua

dhidi ya dhamana ili kurejesha mkopo. Hivyo, kukosekana kwa muda huo kungeleta mkanganyiko kwa mkopeshaji kuwa ni muda gani unahitajika ili aendelee ama asiendelee na utekelezaji. Kamati ilipendekeza ni vyema sheria ikaweka muda kwa Benki Kuu kutoa au kutokutoa idhini. Aidha, Ibara iongeze sharti kwa Benki Kuu kutoa sababu za uamuzi wake. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho ya Serikali.

3.2.15. Ibara ya 45 - Uondoshaji wa dhamana

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 45 pamoja na mambo mengine inakusudia kuweka utaratibu wa uondoshaji wa dhamana pale dhamana hiyo inapokuwa hatarini au mkopaji ameshindwa kutekeleza wajibu. Hata hivyo, **Ibara ya 3** haikuwa imetoa tafsiri ya maneno "dhamana kuwa hatarini" na hivyo kuwepo uwezekano wa kutumiwa vibaya. Aidha, Ibara hiyo haikuwa imeweka mazingira ambayo dhamana itatambulika kuwa hatarini.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Kamati ilipendekeza Ibara hiyo kuboreshwa kwa kutafsiri maneno "dhamana kuwa hatarini" pamoja na kufafanua ni mazingira gani dhamana itahesabika kuwa ipo hatarini. Kamati inaona ulinzi dhidi ya matumizi mabaya ya haki ya kuondosha dhamana ni muhimu yakabainishwa ili kumlinda mkopaji dhidi ya utashi wa mkopeshaji. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho ya Serikali.

3.2.16. Ibara ya 46 - Utumiaji wa dhamana kutimiza wajibu wa mkopo

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba **Ibara ya 51** imeweka utaratibu wa mgawanyo wa fedha, Kamati ilibaini kuwa utaratibu huo haukidhi kikamilifu mahitaji, kwani unaweza usihusu malipo ya awali. Hivyo, Kamati ilipendekeza **Ibara ya 46** ifafanue wazi matumizi ya fedha hizo kuwa ni kufidia mtaji, riba iliyobaki na gharama

zinazokubalika kwa mkopeshaji ili kulipa deni linalotokana na mkataba kwa kuzingatia malipo yaliyokwishafanyika awali.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia mapendekezo hayo Kamati ilipendekeza kufanya mabadiliko katika Ibara ya 46, Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho ya Serikali.

3.2.17. Ibara ya 47 - Utaratibu wa uondoshaji wa dhamana

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa Ibara hii haikubainisha utaratibu wa kupatikana kwa bei ya thamani ya soko wakati wa uondoshaji wa dhamana. Hivyo, Kamati ilipendekeza **Ibara ndogo ya (2)** kuboreshwa ili kutambua mifumo mingine rasmi kama vile ya mazao ya biashara na dhahabu. Lengo la mapendekezo ya Kamati ni kutoathiri mifumo hiyo katika uondoshaji wa dhamana pamoja na kupata thamani ya soko. Serikali ilikubali mapendekeZo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho ya Serikali.

3.2.18. Ibara ya 48 - Taarifa ya uondoshaji wa dhamana

Mheshimiwa Spika, katika Ibara hii Kamati ilipendekeza kubainishwa kwa muda wa utoaji notisi wa uondoshaji wa dhamana kuwa ni siku **30** kutoka siku **14** ili kumpa mkopaji muda wa kutosha ili kufanya marejesho. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho ya Serikali.

3.2.19. Ibara ya 50 - Mkopeshaji kutoa taarifa ya hesabu kwa mkopaji

Mheshimiwa Spika, Ibara haikueleza kuhusu haki ya mkopaji kuweka pingamizi dhidi ya hesabu au taarifa ya hesabu iliyotolewa na mkopeshaji. Kamati ilipendekeza kuweka haki ya pingamizi kwa mkopaji dhidi ya hesabu zilizotolewa na mkopeshaji ili kuondoa

uwezekano wa mkopeshaji kutumia haki yake vibaya. Utaratibu uliopendekezwa na Kamati pia upo katika **Ibara ya 14** na **53** za muswada unaopendekezwa.

Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho ya
Serikali.

3.2.20. Ibara ya 51 - Mgawanyo wa mapato baada ya uondoshaji

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 51 inabainisha mgawanyo wa mapato mara baada ya mali inayohamishika kuuzwa ili kurejesha mkopo. Hata, hivyo Ibara hiyo haikuweka mgawanyo wa mapato yatakayotokana na mali iliyouzwa. Kamati ilipendekeza ibara hii iboreshwe ili kuweka sharti la kuwasilisha bakaa au kiasi kitakachokuwa kimezidi baada ya Mkopo na riba kulipwa. Aidha, endapo kutakuwa na mgogoro kiasi hicho kiwekwe kwenye akaunti ya mahakama ili kusubiri uamuzi utakapofanyika. Serikali ilikubali kufuta na kuandika upya **Ibara ya 51(3)** kama inavyoonekana kwenye jedwali la Marekebisho la Serikali.

3.2.21. Ibara ya 54 - Ukomboaji wa dhamana

Mheshimiwa Spika, Ibara hii haikuwa imebainisha aina ya gharama nyingine zinazokusudiwa kurejeshwa na mkopeshaji kuhusiana na dhamana husika. Hivyo, Kamati ilipendekeza kuweka sharti kwa mkopeshaji kubainisha aina zote za gharama ili kuepusha mkopeshaji kuongeza gharama zisizohusiana na mkopo. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho la Serikali.

3.2.22. Ibara ya 57 - Ukiukwaji wa wajibu

Mheshimiwa Spika, Ibara hii haikubainisha ni mamlaka gani itahusika kwenye utatuzi wa migogoro ya kudai fidia ya hasara au uharibifu wowote uliotokea kutokana na kushindwa kutekeleza jukumu au wajibu wa sheria hii.

Hivyo, Kamati ilipendekeza maboresho ya Ibara ili kubainisha mamlaka itakayoshughulika na mgogoro wa fidia ya hasara au uharibifu uliopatikana. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho ya Serikali.

3.2.23. Ibara ya 60 – Mapitio

Mheshimiwa Spika, Ibara hii ilikuwa inamtaka mtu ambae hajaridhishwa na maamuzi ya Benki Kuu kuomba marejeo ya uamuzi huo kwa Benki Kuu. Hatua hii ilikuwa inamnyima haki mtu ambae hajaridhishwa na Benki Kuu kutendewa haki na mamlaka nyingine tofauti na Benki Kuu ambayo inakuwa ndiyo iliyotoa uamuzi wa awali. Aidha, Ibara hiyo haikuwa imeweka ukomo wa idadi ya siku ambazo Benki Kuu itatakiwa kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Kamati ilipendekeza Ibara hii iboreshwe ili kuruhusu mtu ambaye hajaridhika na maamuzi ya Benki Kuu ya Tanzania kuweza kukata rufaa moja kwa moja kwa Waziri na kuweka muda ambao Benki kuu itatakiwa kufanya maamuzi. Serikali ilikubali mapendekeo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho ya Serikali.

3.2.24. Ibara ya 61 – Rufaa

Mheshimiwa Spika, Ibara hii haikueleza kuhusu haki ya kukata rufaa Mahakamani kwa mtu ambaye hajaridhika na uamuzi wa Waziri. Hivyo, Kamati ilipendekeza Ibara iboreshwe ili kubainisha endapo mtu hataridhika na maamuzi ya Waziri atawasilisha Shauri la marejeo Mahakamani *(Judicial Review)*. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho la Serikali.

4.0. MAONI YA UJUMLA

Mheshimiwa Spika, pamoja na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwenye Ibara mbalimbali za Muswada, Kamati ina maoni ya ujumla yafuatayo:-

4.1. Elimu kwa wakopaji kabla ya kutoa mikopo

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto kuu inayowakabili wakopaji katika sekta ndogo ya Fedha ni elimu duni ya mikopo na matumizi yake. Pamoja na kwamba **Kifungu cha 50(2)(e) cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Sura 407** kinawataka wakopeshaji wote kutoa elimu ya kina kuhusu mkopo, riba, faini, uwazi wa gharama, ulinzi wa mlaji, utunzaji wa taarifa na taratibu za kushughulikia malalamiko.

Kamati imebaini kwamba kifungu hicho hakitekelezwi ama kwa lengo la kutowapa wakopaji Taarifa kamili wanayohitaji ili kukopa au kutokana na mahitaji ya fedha kwa wakopaji yanayosababisha wasizingatie takwa hilo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba wakopeshaji wote katika huduma ndogo ya Fedha wanatekeleza takwa hilo ili kuondoa madhira yanayowakumba wakopaji.

4.2. Wakopeshaji kutokufuata Masharti ya Sheria ya Ukopaji kwa Dhamana na Mali Zinazohamishika ya Mwaka 2026

Mheshimiwa Spika, kutungwa kwa sheria hii pamoja na mambo mengine kunaziba ombwe lililokuwepo la wakopeshaji kukopesha kwa kutumia mali zinazohamishika bila utaratibu. Pamoja na kwamba Kamati imehakikisha kwamba Sheria hii inamlinda mkopaji dhidi ya uuzaji wa mali yake bila idhini yake au utaratibu, bado changamoto itabaki katika usimamizi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Wizara ya Fedha kupitia Benki Kuu kusimamia kikamilifu masharti ya Sheria hii ili kudhibiti matumizi

mabaya yatakayojitokeza. Aidha wakopeshaji wote ambao watatumia mali ambazo hazijasajiliwa kuchukuliwa hatua kali ikiwa ni pamoja na kunyag'anywa leseni zao kama sheria inavyotaka.

4.3. Uanzishwaji wa Klabu za Masuala ya Mikopo Shuleni

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba mikopo ni sehemu muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi bado suala la mikopo halipewi kipaumbele katika mitaala yetu. Imekuwa ni kawaida kwa baadhi ya Watanzania kukopa kwa ajili kufanya sherehe au kutunza mtu kwenye sherehe. Matokeo yake Watanzania wengi wamekuwa wakijikuta katika matatizo makubwa ya kushindwa kurejesha mikopo.

Mheshimiwa Spika, Kwakuwa Serikali ilikwisha andaa mtaala mpya na inaweza kuwa suala gumu kufanya mabadiliko. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu kuhakikisha wanahamasisha uanzishaji wa klabu za masuala ya mikopo kuanzia Shule za Msingi hadi Sekondari. Aidha, vikao vya Vijiji na mitaa viwe na agenda ya kuwapa wananchi elimu kuhusu mikopo. Hatua hizi kwa pamoja zikitekelezwa zitaepusha changamoto nyingi tulizonazo hivi sasa.

4.4. Changamoto za biashara kufanyika nje ya mifumo isiyo rasmi

Mheshimiwa Spika, kufanyika kwa biashara nje ya mifumo rasmi kumesababisha changamoto mbalimbali kama vile kutokuwa na kumbukumbu rasmi za biashara, taarifa za mapato, uthibitisho wa umiliki wa mali na historia ya mikopo. Changamoto hizi kwa pamoja zinaweza kusababisha wafanya biashara wadogo washindwe kupata mikopo kutoka taasisi rasmi za fedha.

Mheshimiwa Spika, Hivyo, masharti yatakayowekwa kwenye Kanuni kuhusu utaratibu wa uthibitishaji wa umiliki wa mali zinazohamishika yawe rahisi kwa Watanzania wote ili Sheria inayopendekezwa iweze kufikia lengo la kuongeza upatikanaji wa mikopo na mitaji kwa Watanzania wanaomiliki na kuendesha biashara ndogo zilizo nje ya mifumo rasmi.

4.5. Utungaji wa Kanuni zinazoendana na Lengo la Sheria

Mheshimiwa Spika, Moja ya changamoto ambayo Kamati ilikutana nayo wakati wa kujadili Sheria hii ni ufafanuzi wa baadhi ya maeneo kupendekezwa kufanyika kupitia Kanuni. Hivyo, Kamati inasisitiza Kanuni zitakazoandaliwa ziendane sambamba na maudhui, malengo na madhumuni ya Sheria ilivyotungwa ili kurahisisha utekelezaji wake.

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha kwa kukushukuru wewe binafsi Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb Spika wa Bunge la Tanzania pamoja na Mhe. Daniel Baran Sillo, Mb Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza vema Bunge lako Tukufu. Nawashukuru pia Mhe. Bal. Khamis Mussa Omar Mb, Waziri wa Fedha, Mhe. Hamza S. Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Mhandisi Mshamu Ali Munde, Mb Naibu Waziri wa Fedha na Mhe. Laurent Deogratius Luswetula, Mb Naibu Waziri wa Fedha, kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wa kuchambua Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali Zinazohamishika wa Mwaka 2026.

Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda kumshukuru Dkt. Natu ElMaamry Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Ndg. Elijah Mwandumbya na Ndg. Nsubili Akomeligwe Kajela Joshua, Manaibu Katibu Wakuu Wizara ya Fedha, Ndg. Emmanuel M. Tutuba, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania na Bi. Dionisia Mjema Kaimu Kamishna wa Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha. Pia niwashukuru Makamishna, Wakuu wa Taasisi na Wataalam wote kutoka Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha kuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza wajumbe wa

Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb Mwenyekiti
2. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Bal. Dkt. Pindi Hazara Chana, Mb Mjumbe
4. Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb Mjumbe
5. Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, Mb Mjumbe
6. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb Mjumbe
7. Mhe. Amina Idd Mabrouk, Mb Mjumbe
8. Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb Mjumbe
9. Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb Mjumbe
10. Mhe. Bahati Kenneth Ndingo, Mb Mjumbe
11. Mhe. Ally Yahya Mhata, Mb Mjumbe
12. Mhe. Kakulu Buchard Kakulu, Mb Mjumbe
13. Mhe. Dkt. Catherine Canute Joachim, Mb Mjumbe
14. Mhe. Moses Charles Bujaga, Mb Mjumbe
15. Mhe. Asma Ali Mwinyi, Mb Mjumbe
16. Mhe. Haran Nyakisa Sanga, Mb Mjumbe
17. Mhe. Devotha Daniel Mburarugaba, Mb Mjumbe
18. Mhe. Thomas Mgonto Kitima, Mb Mjumbe
19. Mhe. Enock Zadock Koola, Mb Mjumbe
20. Mhe. Nancy Hassan Nyalusi, Mb Mjumbe

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, nimshukuru Ndg. Baraka I. Leonard, Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mashimba Mashauri Ndaki, Mb
MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI
31 Agosti, 2026

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Esther Matiko kwa uwasilishaji wa taarifa ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia kwenye uchangiaji. Ninamwita Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, ajiandae Mheshimiwa Devotha Daniel, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata uhai na afya na pia nikushukuru wewe kwa kuniona na kunipa nafasi hii ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakumbuka kwamba Januari 15, 2026, katika Bunge hili la Kumi na Tatu, Mkutano wa Pili, huu Muswada ndiyo uliletwa kusomwa kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu tuliujadili katika Kamati, katika Bunge lote la Bajeti na pia katika Mkutano huu wa Nne ambapo pia tumejadili tena na hatimaye leo umekuja hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri msomaji wa Kamati ya Bajeti katika taarifa aliyosoma, amefafanua kila kitu na bora alivyochukua muda ili watu waelewe kitu gani kimo katika hii sheria. Yale marekebisho ambayo ameyasema ni marekebisho ambayo Kamati imeyapendekeza kwa Serikali na Serikali imeyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru sana Serikali kwa kuwa sikivu na kuweza kufanya marekebisho katika maeneo hayo. Marekebisho hayo yamelenga zaidi katika kuangalia haki na wajibu wa mkopaji na mkopeshaji, pamoja na dhamana iliyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuwa na Sheria hii, ilikuwa watu wanakopeshana na mali zinawekwa dhamana, lakini palikuwa hapana sheria. Kwa maana hiyo, ilikuwa kila mmoja anatumia uwezo na nguvu au anaweza akatumia ule ukweli, huruma yake,

lakini ilikuwa hakuna sheria. Kwa kuja sheria hii sasa, imekuja kuponya makundi yote mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma, mtu alikuwa anaweza akachukua dhamana akaiweka, lakini akachukua mikopo inafika mitatu kwa dhamana ile ile moja. Akaenda kwa A, akachukua mkopo akaweka dhamana hiyo hiyo; akaenda kwa B, akaenda na kwa C, akachukua mikopo ile ikalundikana na baadaye dhamana yake thamani yake ikawa ni ndogo na asiweze kurudisha ule mkopo na ikasababisha hiyo mikopo ikaitwa mikopo chechefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine inawezekana ikawa mkopeshaji anaweza kwenda kuchukua dhamana kwa nguvu ambayo ina thamani kubwa kuliko mkopo alioutoa na badala yake akachukua, lakini sheria hii ilivyokuja imesema hivyo vitu vyote ambavyo vitafanyika kwa mujibu wa sheria na kila mmoja amelindwa katika haki na wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mfano mmoja tu. Kule kwetu alikuwepo mtu mmoja anaitwa nguvu mdomo. Huyu nguvu mdomo, utakapokwenda wewe kumdai, wewe ndio unaodai lakini utarudi wewe unalia. Ni kwa sababu ya nguvu mdomo. Utapata maneno, utapata kashfa na pengine kupigwa utapigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sheria hii, dhamana imesajiliwa, dhamana imewekwa, inajulikana thamani yake na tayari taasisi ziko zinazoshughulikia. Kwa hiyo, zitakwenda kutukomboa, na hii sheria inalenga zaidi katika uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zote mbili; taarifa ya Waziri na taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti imesema mambo haya hapa yafuatayo: kwamba huduma za fedha kufikia 50% itakapofika 2030, kutoka 22%; lengo lingine ni kuongeza uwiano wa mikopo kwa sekta binafsi kwa pato la Taifa kufikia 50% itakapofika 2030 kutoka 22.5% na pia kuongeza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndiyo kidogo ninataka niwashawishi Wabunge wenzangu tuipitishe hii sheria haraka sana kwa sababu inakwenda kututatulia matatizo ya kiuchumi. Moja, nitaanza labda katika sekta hizi binafsi. Tunakwenda kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kitu kimoja, wasanii wana kitu wanaita hakimiliki kwa nyimbo zao. Sasa zitakuwa zina hakimiliki. Leo sheria hii inakuja kufungua fursa kwamba kumbe kama una kitu ambacho kinakupatia mapato, ambao wanapata mrabaha, kumbe unaweza ukakopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tuna fungu la kukopesha wasanii. Ninakumbuka tulikuwa na Mwana FA hapa tukawahangaikia baadhi yao, lakini wengine hawakupata kwa sababu fedha zilikuwa kidogo, lakini sasa benki zitakuwa tayari kuwakopesha hawa watu na kuweza kufanya shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, wanapata mrabaha, lakini pia kuna *blank tape levy* ambayo wale wanaorudufu zile kazi zao, wanaweza wakazitumia. Kwa hiyo, msanii anaweza akapeleka *catalogue* yake ya nyimbo zake akakopeshwa kwa kuweka dhamana kwa sababu zile nyimbo zina mapato yanatarajiwa, pia ni umiliki wa kwake yule. Kwa hiyo, hili litakwenda kututatulia tatizo hilo la kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kihistoria, hapa kwetu Tanzania wakina mama wengi hawamiliki mali zisizohamishika, lakini wengi wana uwezo wa kumiliki mali zinazoweza kuhamishika. Kwa hiyo, kwa ujio wa sheria hii, tunakwenda kuiponya nchi yetu katika kutanua uchumi katika sekta ndogo binafsi, katika sekta ndogo ya fedha na sekta binafsi, kwa sababu atapata fursa hiyo ya kwenda kukopa na kufanya mambo yao ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie mambo mawili, moja kwa Serikali, na moja kwa wananchi wa Tanzania ambao

wanatusikiliza. Serikali; kama alivyozungumza Mwenyekiti wa Kamati katika taarifa ya Kamati, ni kwamba kanuni zitakapokuja kutungwa ziendane. Hapa wakati mwingine kwenye jambo zuri tunaweza tukaja tukatofautiana katika kanuni. Zinaweza zikawepo kanuni ambazo zikakwamisha utekelezaji wa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuiombe Serikali ije na kanuni nzuri kwa wananchi na kwa Serikali pia, ipatikane elimu. Ili tunapokwenda kukopa kwa kuweka dhamana zetu, tusiende kucheza hizi ngoma za mitaani wala tusiende kufanya mambo ambayo hutaweza kurejesha, kwa maana hiyo utasababisha wewe mwenyewe ufilisike. Kwa hiyo, niwaombe wananchi, wakakope kwa shughuli za kiuchumi. Ukikopa kwa shughuli za kiuchumi, haya malengo aliyoyasema Mheshimiwa Waziri na haya malengo iliyosema Kamati, kufikia 2030, yanaweza yakafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa upande wangu, niwaombe Wabunge kwamba Kamati imefanya kazi nzuri na ndiyo maana taarifa ilikuwa ndefu, waiamini Kamati. Hii Sheria ni nzuri, kwa hiyo, tuipitisheni sote kwa nguvu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Devotha Daniel, ajiandae Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga.

MHE. DEVOTHA D. MBURARUGABA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikushukuru kwa kunipa nafasi, na pia nichukue fursa hii kuwapongeza sana Wizara ya Fedha na wadau wote ambao wameshiriki kwenye Muswada huu, pia na Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakwenda moja kwa moja kuunga mkono Muswada huu, kwa sababu, tukiangalia Dira ya 2050 tunaona kwamba Muswada huu unakwenda moja kwa moja kuinua uchumi wa Watanzania. Ninasema haya kwa sababu tunajua

kabisa Watanzania wana mali nyingi, lakini wengi wao wana mali ambazo zilikuwa ziko tofauti na ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kabisa Tanzania hii wamiliki wa ardhi ni asilimia tatu. Kwa hiyo, tunaona kuna Watanzania wana magari, wana mashine, wana mazao, wana vitu mbalimbali ambavyo wanaweza kuvitumia kwa ajili ya kukopa. Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, huu ni wakati wa kwenda na Muswada huu, kwa sababu tunakwenda kuhakikisha maisha ya Watanzania yanaenda kuinuliwa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninasema hayo? Kwa sababu Muswada huu umetaja *very clear*, tutakwenda kuwa na usajili wa hizi mali. Tutakwenda kuzisajili kwa ajili ya kuzitambua, na hili litatusaidia. Watanzania wataweza kusajili mali zao, na tutaweza kupunguza *default of loans* ambayo ilikuwa inatokea, kwa sababu Watanzania wengi walikuwa wanaweza kutumia mali hiyo hiyo moja kukopa taasisi mbalimbali ambapo mwisho wa siku ilikuwa inasababisha migogoro mikubwa sana kwenye familia zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiongelea akina mama, *just imagine* mwanaume amekwenda kazini, wanakuja wale watu wa kausha damu, wanakusanya vitanda, wanachukua redio, wanachukua vitu mbalimbali kwenye nyumba. Mwanaume anaporudi migogoro inakuwa mikubwa sana kwa sababu sheria zilikuwa hazipo zinazoweza kuwakalisha chini wote wakakubaliana kwamba tupeleke mali gani kwa ajili ya kukopea? Kwa hiyo, Muswada huu ni muhimu sana kwa Watanzania na umekuja kwa wakati mwafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tunaona Muswada huu unakwenda kuinua pato la Taifa, kwa sababu tunafahamu zilikuwepo taasisi ambazo zilikuwa zinawakopesha Watanzania, lakini taasisi hizo zilikuwa zinazingatia ardhi, nyumba, na vitu vingine ambavyo vilikuwa viko katika *documentation*. Leo hii tunakwenda kuzialika taasisi nyingi ambazo zitakwenda kufungua ofisi kwa ajili ya kukopesha wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii italeta nini kwenye uchumi wa Tanzania? Ina maana riba za mikopo zinakwenda kushuka, na Watanzania wengi wakiwemo wakina mama, vijana, wakulima na wafugaji, wataweza kukopa kwa kutumia mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tukiongelea wakulima waliopo ndani ya Mkoa wa Kagera wataweza kukopa kwa kutumia stakabadhi za ghala, ambapo tunaona kabisa tunakwenda kuinua uchumi wa Watanzania ambao wana maisha ya chini. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, huu ni wakati mwafaka wa kuhakikisha Muswada huu tunaupitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni muhimu sana kwenye Muswada huu, tumeona kabisa hizi mali ambazo zitawekwa kwenye dhamana na tutakwenda kutengeneza *transparency*. Kwa maana kwamba kwa mtu atakayekuwa anakopa na yule atakayekuwa anakopeshwa kutakuwa kuna uwazi mkubwa sana kiasi kwamba atakayekuwa anakopeshwa atajua sheria zote za kukopa, na mkopeshwaji pia ataelewa, atapewa elimu, lakini moja kwa moja tutaweza kutambua umuhimu wa kukopa wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu Watanzania tulikuwa na desturi ya kukopa. Tukipewa mikataba, tunasaini *very fast*. Mwisho wa siku tunakuta kuna sheria ambazo tulikuwa hatuzitambui, lakini Muswada huu umesema *very clear* nini ambacho kitakwenda kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nitoe ushauri mdogo tu kwa huu Muswada. Tunafahamu kwamba Watanzania wengi watakaokwenda kukopa watakuwa ni Watanzania wenye maisha ya chini wakiwemo akina mama, na wafanyabiashara wadogo wadogo. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iweze kuweka gharama nafuu kwenye huu utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kuna kusajili mali, na kuna kukata bima. Huu utaratibu wote ukiwa na gharama ndogo, ndiyo

tutakwenda kuwafikia Watanzania wa chini. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali yetu iweze kuhakikisha gharama hizi zinakuwa ndogo sana ili hata wale wananchi wenye kipato cha chini waweze kukopa na gharama hizi ambazo zitakuwa zinatumika kwa ajili ya kupata hii mikopo ziweze kuwa ni gharama nafuu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ninaiomba Serikali yetu, tuweze kuzingatia utoaji wa elimu kwa wananchi kuhusiana na hii mikopo ambayo inakwenda kutolewa. Tumeona wananchi wengi hasa hasa hata kwenye ile mikopo ya 10%, tunaona ni jinsi gani wananchi wetu wanahitaji kupata hii elimu. Ningeomba kupendekeza angalau hizi elimu zifanyike kuanzia kwenye elimu ya shule huko ili tuweze kujua elimu ya mikopo, tuitambue. Hata tukifika kwenye ngazi za chini, tuweze kuhamasisha viongozi walioko kwenye Serikali za Mitaa, Wenyeviti pamoja na watu wengine, tuweze kuhamasisha kujua elimu hizi kabla hawajaenda kukopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, ajiandae.

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nami niungane na Wabunge waliotangulia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na wenzetu wa Serikali kwa kuleta Muswada huu. Taarifa ya Kamati imeeleza hapa kwamba zaidi ya 46% ya mikopo inayotolewa sasa inatolewa kwa dhamana ya mali zinazohamishika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ni wazi kwamba sheria hii ambayo tunaitunga tayari kule mtaani utekelezaji wake ulishaanza, ila utekelezaji huu ulikuwa unafanyika bila mwongozo maalum wa kisheria. Benki na taasisi mbalimbali za fedha tayari walikuwa wanakopesha kwa mali ambazo zinahamishika. Kama ambavyo

Kamati imesema, utafiti uliofanywa na taasisi inayoitwa *Financial Sector Deepening Africa* kwa kushirikiana na *Financial Sector Deepening Trust*, hii ndiyo inaonesha 46% ya dhamana zote ambazo zinatumika ni za mali ambazo tayari zinahamishika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa nini? Ni kwa sababu utafiti pia umeonesha kwamba Watanzania ambao wana hati hawazidi asilimia tatu. Kwa hiyo, ni eneo dogo sana. Watanzania wengi ambao walikuwa na sifa za kupata mikopo, wana uwezo wa kufanya kazi na hawana mitaji, walikuwa wanashindwa kupata dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kutunga sheria hii maana yake Serikali inakwenda sasa kuweka utaratibu mzuri ambao utazingatia vitu kama upatikanaji rahisi wa mitaji kwa wananchi. Tukiangalia Dira ya Maendeleo ya Taifa inazungumzia kukuza viwanda na biashara. Sasa vitu kama hivi vinahitaji sana mitaji. Wananchi wetu waweze kuwa na mitaji ili waweze kufanya biashara na hasa akina mama, vijana, wahitimu wa vyuo vikuu na wasanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumzia lengo kuu la hii sheria; kwanza kabisa ni kurahisisha mfumo wa dhamana; pili, ni kuweka mambo ya uwazi; na vilevile kuhakikisha kunakuwa na usalama. Kwa sababu Benki Kuu ndiyo imepewa dhamana ya kuwa msajili, hapa kinachotakiwa sasa kama ambavyo wazungumzaji wenzangu wamesema; Benki Kuu iko makao makuu labda na kwenye kanda, lakini changamoto za wananchi wanaokosa mitaji zipo kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Benki Kuu ijitahidi sana kuangalia eneo hili ili kuwafikia wananchi walio wengi hasa wa maeneo ya vijijini. Kwa hiyo, watatumia njia gani? Wanaweza hata kuweka mawakala kwa sababu benki hata pale kwangu Ludewa kuna benki, kuna *NMB,* kuna *CRDB* kwa sababu nao ni taasisi au waje na mfumo wowote ambao unaweza kuwafikia wananchi kirahisi zaidi kuliko mwananchi akiwa na changamoto aanze kuhangaika kwenda mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua vilevile kwamba mfumo huu wa usajili utakuwa wa kidijitali na hapo ndipo tunapozungumzia uwazi; kwamba kila mtu anaweza akaona. Hata benki kabla ya kumkopesha mtu watakuwa wanaangalia kama amechukua mkopo sehemu nyingine kwa mfumo huu wa kielektroniki. Kwa hiyo, ni muhimu sana kwenda kisasa, kutumia mifumo hii ya kielektroniki (mifumo ya kidijitali) katika usajili na hivi vitu viwe wazi mtu yeyote aweze kuona. Hii itasaidia sana kuepusha migogoro na ukiusoma huu Muswada kwa kiasi kikubwa umezingatia haya ninayosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia pia hata Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi mbali na dira, Ilani ya 2025 – 2030 nayo imesisitiza sana kwamba kutakuwa na mfumo ambao ni rahisi kwa wananchi kuweza kupata mitaji na mifumo hii ambayo haitamwacha yeyote pembeni. Kutakuwa na hiyo *financial inclusion*. Kwa hiyo, watu wote waweze kupata mitaji kwa sababu kila mtu ana haki ya kufanya kazi kwa mujibu wa Katiba ya nchi. Kwa hiyo, sasa wapewe fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani vilevile inazungumzia kutengeneza ajira 8,000,000. Sasa hizi ajira zote haziwezi kuwa za kuajiriwa na Serikali au kwenye utumishi wa umma au mashirika. Kwa hiyo, kama kutakuwa na njia rahisi na mfumo mwepesi wa wananchi kuweza kupata mitaji, yaani mtu ana mazao yake, ana vifaa vyake vya biashara, ana mifugo yake kama ng'ombe au mbuzi nayo ikubalike kama dhamana. Ila tu kama ambavyo sheria imeeleza kutakuwa na utaratibu ambao ile mifugo inaweza ikawa imekatiwa bima kwa ajili ya usalama. Kwa hiyo, hizo taratibu zote zimezingatiwa na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunavyozungumzia ajira 8,000,000 tunahitaji wananchi wengi zaidi waweze kuwa na fursa ya kupata mitaji kirahisi ili waweze kujiajiri kwenye biashara mbalimbali na kuajiri Watanzania wengine. Hizi biashara zikikua sasa ndiyo dira pia inasema kwamba Serikali haiwezi kugharamia utekelezaji wa dira hii. 70% ya mtaji unatakiwa utoke kwenye sekta binafsi, kwa hiyo, ni lazima tuhakikishe kwamba kwenye sekta binafsi kunakuwa

na ukwasi wa kutosha. Taasisi za fedha zinapata ukwasi wa kutosha na kuna mifumo rahisi ambayo wananchi wanaweza wakapata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mtu labda ana vifaa vyake vya biashara, taasisi ya fedha inaweza kwenda kuviangalia, kuviona na kuvitumia kama dhamana kuliko kusubiri tu kila mwananchi aweze kuwa na hatimiliki. Hatusemi kwamba watu wa ardhi wasiendelee kupima na kutoa hatimiliki, hayo yaendelee lakini tunaangalia wepesi kwa Watanzania wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu hawa wanaoendesha bodaboda, ile bodaboda anaweza akaenda sehemu akakopa na yenyewe ikawa kama dhamana akalipa taratibu. Kwa hiyo, tunaona jinsi gani sheria hii itakwenda kusaidia vijana wengi wa Kitanzania kupata ajira. Wapo wafanyabiashara wa vyombo vya usafiri, magari na malori, nao wanaweza wakatumia hivyo vikawa kama dhamana kwa ajili ya kupata mikopo kirahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja na ninawashawishi Wabunge wote waweze kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga; Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe, Mheshimiwa Mwanahamisi Athumani Munkunda na Mheshimiwa Pindi Hazara Chana wajiandae.

MHE. HARAN N. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwanza, kwa kutoa pendekezo la jina la Makamu wa Rais, lakini hatimaye Kamati Kuu, Halmashauri Kuu na Bunge kutoa kura za kishindo kwa kuonesha imani kwa kijana mwenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusema tu kwamba Rais wetu amekuwa na imani kubwa sana kwa sisi vijana na kutuamini

katika shughuli mbalimbali. Ni dhahiri kabisa sisi sote tunaona namna ambavyo vijana wamekuwa wakitekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa, kwa umakini na kwa weledi mkubwa. Niendelee kusema vijana tuchape kazi ili kuendeleza imani hiyo, lakini pia misingi, miiko na maadili ya uongozi kwa ajili ya kujenga Nchi yetu ya Tanzania maana hatuna Nchi nyingine zaidi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii pia kumpongeza sana Mkuu wetu wa Mkoa wa Dar es Salaam, *Comrade* Albert Chalamila; kwa kufanya *operation* ya kupunguza foleni ya malori pale mjini. Ninaomba niseme wananchi wangu wa Kigamboni wanampongeza sana kwa sababu walikuwa wanachelewa kurudi nyumbani, lakini sasa barabara ni nyeupe wanaenda kwa ufanisi mzuri na wanafanya kazi vizuri kabisa. Hivyo, ninaomba nitumie jukwaa hili kumpongeza sana. Ninamshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kumwacha katika mkoa wetu wa Dar es Salaam ili aendelee kutekeleza majukumu yake kama anavyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu wa mali zinazohamishika ni kitu ambacho leo kama Bunge tunaenda kujenga historia kwa Watanzania. Maana Muswada huu unaenda kuwa nyenzo ya kukuza uchumi kuelekea Dira ya 2050. Muswada huu una mafungu 10 ambayo yamebainishwa na Kamati ya Bajeti, lakini pia mafungu haya yamebainishwa na Wizara. Ukiyasoma ndiyo ambayo yamekuwa *guideline* kubwa ya ku-*formalize* Muswada huu ambao utaenda kuwasaidia wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumpongeze Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuona vilio vingi vya Watanzania hasa ambao walikuwa wanakopa mikopo, wanachukuliwa mali zao, lakini kunakuwa hakuna *fairness* katika *repayment processes* za ku-*cover* huo mkopo. Wamekuja na hii sheria ambayo sasa itakuwa ni *guideline* ya kuwasaidia Watanzania kwa sababu ina masharti ya pande zote mbili za mkopaji pamoja na mkopeshaji. Hii yote ni

katika hatua ya kulinda maslahi ya wakopaji au wananchi wa Tanzania ambao wataenda ku-*enjoy* kutokana na Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe na ninawashawishi sana Waheshimiwa Wabunge, tuunge mkono Muswada huu kwa 100% kwa sababu unaenda kutusaidia hata sisi Wabunge. Zile za kuombwa shilingi 100,000 au shilingi 2,000,000 kwa wananchi wetu zitakuwa zimepungua kwa kiasi kikubwa sana kwa sababu hawa wananchi watakuwa na uwezo sasa wa kutumia mali zao na vitu vyao walivyonavyo mathalan kama baiskeli, ng'ombe, kuku, kondoo na gari. Hivi vyote ni mali zinazohamishika zilizoainishwa katika hii mikopo ili ziweze kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania hawa wakipata mikopo wataweza kufanya biashara. Ukiangalia Dira yetu ya 2050 tunazungumzia 70% *private sector* na 30% Serikali. Hii itaenda kusaidia sana kuinua uchumi wa *private sector* na kuongeza *tax base* ya nchi yetu katika kuongeza mapato na hasa katika kutoa huduma mbalimbali za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niende kwenye usajili wa maslahi ya dhamana. Kipengele hiki kimekuwa ni muhimu, kipengele ambacho kimezingatia kwamba mali zote ambazo zitakuwa zinatakiwa kukopeshwa au kukopea zitatakiwa zisajiliwe kwa thamani ambayo itakuwa imeainishwa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Muda wako umekwisha.

MHE. HARAN N. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. Nilimtaja Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe, ajiandae Mheshimiwa Mwanahamisi Athumani Munkunda.

MHE. LUCY EDWARD MWAKYEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Muswada huu ambao umefika hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ajili ya asubuhi hii, lakini pia ninatoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambazo anazifanya na anaendelea kuzifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru pia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona sasa umekuwa ni wakati sahihi wa kufanya marekebisho ya Muswada kwa ajili ya kupeleka tumaini na furaha kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza vilevile Serikali kupitia Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Balozi Dkt. Khamis Mussa pamoja na wasaidizi wake kwa kuleta Muswada huu siku ya leo ili tuupitishe kwa ajili ya dhamana hii ya mikopo ya mali zinazohamishika kwa ajili ya kuwanufaisha wananchi wa Tanzania. Ninapenda pia kuipongeza Kamati ya Bajeti ambayo inafanya kazi kubwa katika kupitia bajeti za Serikali kwa ajili ya Taifa, lakini pia imefanya uchambuzi mkubwa hasa kupitia kwenye Muswada huu ambao umewasilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nizungumzie suala la umuhimu wa mkopo. Muswada huu umeenda kuwakomboa wanawake, vijana, watu wenye ulemavu na wananchi wote kwa ujumla. Hapa tunakwenda kuwapatia ajira, kuwapatia mitaji na kuinua maisha ya wananchi na kuinua pia vipato vyao. Pia, kuna wale ambao wanatamani na wao kuchangia pato la Taifa lakini inakuwa ni vigumu, kwa hiyo, sasa ni wakati mwafaka kwa wao kuweza kuchangia pato la Taifa na kuinua uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze tena Serikali kwenye upande wa dhamana ya mikopo ambayo imewekwa kwa ajili ya wanawake. Tumeona wanawake wengi walikuwa wanapata shida

katika kuweka dhamana ya mikopo kwa sababu wakati huo ilikuwa inatakiwa dhamana ya mali zisizohamishika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wengi walikuwa hawawezi kumiliki hati kwa ajili ya kuomba mikopo hiyo, lakini sasa umefika wakati wanawake na wao wamekombolewa na baadhi ya wananchi pia wamekombolewa kwa ajili ya kuomba mikopo hiyo kwa kutumia mali ambazo zinahamishika kama vile magari, fedha ambazo ziko benki, samani na hata mauzo ya biashara zao pia umekuwa ni msaada mkubwa kwa ajili ya kuweza kuchukua mikopo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea tena kuipongeza Serikali kwa ajili ya dhamana ya mikopo hii ya mali zinazohamishika. Pia, kuna umuhimu mkubwa wa kulipa mikopo hii kwa wananchi. Sasa wananchi wanatakiwa waweze kuwa na kipato kikubwa na pia mkopo huu wanapouchukua wapate matumaini ya kuongeza kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaiomba Serikali, waangalie hata kwenye upande wa zile riba ambazo zinawekwa. Tunaona Serikali ina lengo zuri la kuweka riba na tunaona riba mwanzo wake waliionesha kuwa asilimia 3.5, lakini sasa riba zinawekwa kubwa zinafika mpaka 12%, kidogo kinakuwa kilio kwa wananchi. Tunaomba hapo Serikali waangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuchangia kuhusu gharama kwa ujumla za mikopo; mwananchi mpaka anapotaka kukopa ingawaje kasharahisishiwa kwenye upande wa mkopo basi apate kujua gharama halisi siyo anakwenda kukopa lakini baadaye gharama zinageuka kuwa kubwa kwake. Apewe elimu ya kuelewa gharama halisi za mkopo zinakuwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali pia iangalie, wakati ambapo wananchi hawa wamekopa hususan wanawake isifikie wakati ambapo mwananchi anashindwa kulipa, bila ya wao kukaa pamoja kujua kwa nini ameshindwa, ananyang'anywa mali zake,

hapa haitakuwa vizuri. Tumempa furaha ya kumpa mkopo, basi isifike wakati wa kumnyang'anya mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, ninawaomba wanawake wote, vijana na watu wenye ulemavu pamoja na wananchi wote; hii ni fursa kwa ajili ya kuchukua mikopo ili kuongeza tija, kuongeza vipato katika familia na kufanya maisha kuwa mazuri kwa ajili ya familia. Kwa hiyo, ninawaomba sana tuichangamkie, lakini tunapochangamkia fursa hii, tunapopewa mikopo hii, hususan wanawake basi tuhakikishe tunailipa, tusibaki na madeni na baadaye kugeuka kuwa wanawake ni wadaiwa sugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Mwanahamisi Athumani Munkunda; wajiandae Mheshimiwa Pindi Hazara Chana na Mheshimiwa Josephine Kapoma. Tutamalizia na Mheshimiwa Thomas Kitima.

MHE. MWANAHAMISI A. MUNKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa Muswada huu mzuri, lakini pia ninawapongeza sana Kamati ya Bajeti kwa mapendekezo na ushauri ambao wameutoa kwenye Muswada huu. Kwa kweli ninayaunga mkono mapendekezo yote na ibara zote walizozipendekeza kufanyiwa maboresho zikifanyiwa hivyo, tutakuwa tumerahisisha utekelezaji mzuri wa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu kwa maana rahisi unakwenda kutafsiri utekelezaji wa Dira ya 2050 na unakwenda kuongeza wigo wa dhamana ambazo zilikuwa hazitambuliki na zilikuwa zikitumika bila kuwa na utaratibu wa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sasa tukipitisha Sheria hii, itakwenda kurasimisha zile mali na dhamana ambazo zilikuwa zikitumika na *microfinances* ambazo kwa wakati mwingine zilikuwa

zikiwaumiza wakopaji, wakati ambao wakopeshaji walijua kwamba hakuna sheria au taratibu ambazo zilikuwa zinasimamia dhamana hizi. Sasa uwepo wa sheria hii utakwenda kusaidia kuokoa haki za wakopaji na hasa kwenye zile *microfinances* ambazo kwa kiasi kikubwa walikuwa wanakwenda wajasiriamali wadogo kuchukua mikopo; na ambayo wakati mwingine kwa sababu ilikuwa hakuna sheria na utaratibu ambao ulikuwa unasimamia, dhamana hizi walikuwa wakipangiwa *interest* kulingana na mkopeshaji anavyoona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbuka mikopo hii kwenye *microfinances,* lengo lake lilikuwa ni kutengeneza mitaji lakini ilikuwa haitengenezi mitaji badala yake ilikuwa inakwenda kuwafilisi hawa wajasiriamali. Akipeleka dhamana yake inayohamishika, kwa mfano gari, anakwenda kufanyiwa uthaminishaji ule ambao mkopeshaji anaona yeye unamfaa kwenye biashara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, unapeleka gari ya shilingi 40,000,000, *market value* ya gari hiyo, lakini anaweza akaambiwa gari hili lina thamani ya shilingi 10,000,000, kwa hiyo utapata mkopo wa shilingi 5,000,000. Ataacha kadi ya gari na ataacha hiyo dhamana yenyewe hapohapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mkopeshaji alikuwa na uwezo wa kutumia dhamana ile vile anavyotaka yeye na mwisho wa siku matumizi mabaya ya dhamana yanaweza ikapelekea hata mtu huyu dhamana yake isiweze kurudi hata pale anapokuwa amekopeshwa. Kwa hiyo uwepo wa Sheria hii na uanzishwaji wa ukataji wa rufaa itamlinda mkopaji na pia itamlinda mkopeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, kwa sababu riba inakuwa *determined* na soko, tunapoongeza wigo wa *collateral*, tunapoongeza dhamana, hasa dhamana hizi ambazo zinahamishika, ni matumaini yetu pia kwenye kanuni sasa tutakwenda pia ku-*leverage,* kupunguza *interest* kwenye maeneo mbalimbali ya mikopo kwa sababu mikopo hii ilikuwa imefungwa kwenye mali zisizohamishika peke yake. Sasa, tunapoongeza wigo

wa *collateral,* ni mategemeo yetu kwamba wananchi watakwenda kufanyiwa wepesi kwenye upatikanaji wa mikopo hii, lakini pia ku-*leverage interest* kwenye maeneo haya wanayokopa kwa kutumia bidhaa hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, kwa sababu dira inatuambia sekta binafsi wanapaswa kuchangia shilingi 1,000,000,000,000, kwa hiyo Serikali kuja na Muswada huu ni dhahiri kwamba sasa tunakwenda kuongeza *tax base* kubwa na tuweze kufikia sasa hitaji hili la shilingi 1,000,000,000,000 kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme, kwa uwepo wa Sheria hii, itakapoanza utekelezaji wake, maana yake sekta binafsi na hasa wajasiriamali wadogo, kwa mfano hapa ukipiga tu hii 1,000,000,000,000, kama tuna idadi ya wajasiriamali labda 1,000,000, maana yake kila mjasiriamali mmoja anaweza akachangia tu shilingi 1,000,000 kwa mwaka ndiyo ukafikisha shilingi 1,000,000,000,000. Kwa hiyo maana yake tunaweza kuongeza mapato na tunaweza tukaongeza makusanyo ya Serikali kupitia utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji, hasa sekta binafsi na hasa wajasiriamali wadogo ambao walikuwa wanategemea mikopo aidha kutoka kwenye halmashauri tu, sasa itakwenda kuongeza wigo wa ukopaji. Maana yake sasa tunategemea riba pamoja na zile changamoto ambazo zilikuwa zikiwakabili wajasiriamali wadogo kwenye upatikanaji wa fedha, zitakuwa zimetatuliwa. Maana yake ni kuwa itasaidia kuongeza ajira hasa kwa makundi yale ambayo yalikuwa hayahitaji ajira rasmi, kama wajasiriamali na vijana kwenye uchangiaji wa pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, kupitisha sheria hii ili tuweze kuongeza utekelezaji na wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Pindi Hazara Chana na ajiandae Mheshimiwa Josephine Kapoma.

MHE. DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote, ninaomba kuunga mkono hoja Muswada huu ulioko mbele yetu leo, ni Muswada muhimu sana. Niipongeze sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan chini ya uongozi wake bora na imara, tunapata Muswada huu ambao unakwenda kuleta tabasamu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muswada huu, awali tulikuwa na Miswada mbalimbali ambayo ilikuwa inaruhusu mikopo kwa kutumia mali zisizohamishika *(fixed asset);* lakini sasa tunakwenda kufanya *reforms* ndiyo zile *4Rs – Reform, Rebuilding, Reconciliation* na lazima tuwe *Resilience*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa zile *4Rs* leo hii Serikali; chini ya uongozi mzuri pia wa Mheshimiwa Waziri na timu yake, wanasema sasa wataruhusu mikopo kwa mali zinazohamishika. Mali zinazohamishika ni pamoja na magari, mashine (iwe ni mashine za kusaga), bajaji na bodaboda. Nimeshuhudia benki wanawakopesha vijana wa bajaji na bodaboda kama *CRDB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama wanaweza kuwakopesha watu waendeshe, maana yake siku nyingine hawa vijana wetu wa bodaboda wanapokuwa wanakosa pesa, wawe na uwezo pia wa kurudisha bodaboda na kusema wanaomba fedha. Kwa hiyo Muswada huu ni muhimu sana, utaleta maboresho ya kiuchumi ya hali ya juu kama walivyosema waliotangulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba sana; tumekubaliana kwamba kutakuwa na *registry* (masijala). Hizi mali ambazo zinakwenda kukopeshwa zinazohamishika, kutakuwa na masijala maalum zinasajiliwa kama ni gari, hii gari kweli ipo? Namba ngapi? Au imeuzwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii masijala katika mjadala na Kamati tulisema iwe ni masijala inayojitegemea. Baadaye tukawa na muafaka mpaka kwamba, masijala hii iwe chini ya *BOT* – Benki Kuu. Kwa hiyo Benki Kuu wakumbuke kwamba tunayo mikoa isiyopungua 26, wilaya zisizopungua takribani 180. Kwa hiyo ni lazima *BOT* ifikike wanapohitaji kujua taarifa za masijala za benki mbalimbali, basi *BOT* iwe *accessible*, ifikike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati tumeshauri kwamba, wakati wa kutangaza kwenye Gazeti la Serikali *(Government Notice)* hizi mali, ni muhimu *BOT* washirikishe wadau. Kama ni gari, maana yake watu wanasajili *TRA*, *TRA* inashirikishwa na wadau mbalimbali. Kwa hiyo hii *registry* ni sawa ikiwa *BOT*, inaweza ikawa pengine kama *BRELA* au wapi, lakini kama ni *BOT*, lazima ifikike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mali hizi ambazo zinakwenda kuwekwa kama dhamana, ni muhimu ziwe na bima. Hapa kuna bima za aina kadhaa. Wakati wananchi wanachukua mikopo benki huwa zinasema zinakata asilimia moja au mbili kwa ajili ya bima. Vivyo hivyo, hizi mali zinazohamishika ni muhimu na zenyewe zikawa na bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewahi kufuatwa na wananchi, wakaniambia kuwa wamechukua mkopo, wameambiwa kuna bima, lakini benki haiwapi *insurance cover*. Wamesema wamekata asilimia moja ya bima. Sasa, bima ni haki ya *customer* kuwa na *insurance cover, insurance note*, hawakuwapa. Hii ni bima ya aina gani ambayo wewe uliyekuwa *insured* hupewi *cover*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuweke vitu vizuri, kuwe na *transparent*, mwananchi afurahi, maana tunapeleka tabasamu. Kama ni gari, mashine, nazo ziwe zina bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, chini ya uongozi wake. Wanawake Tanzania wapo zaidi ya 50%, kuna mikopo ya 10%, kuna

mikopo ya Mfuko wa Pembejeo, kuna mikopo ya kilimo, yaani kila kona ni mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, hizi benki *(Financial Institutions)* sasa wafanye kazi ya kuwezesha ku-*facilitate* na wasiwe kikwazo. Wananchi hao wanataka mikopo, benki isaidie. Kwa wananchi wetu huko vijijini tulikotoka, hizo nyaraka nani wanawasaidia, lete hiki polepole, lete *NIDA*, usiseme tu hapa hajakidhi, arudi, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sauti hii ya Bunge isikike, benki wawe *facilitative role* kwa wananchi wetu. Wawaelekeze wananchi namna ya kurejesha mikopo polepole. Isiwe tu siku imefika, wanapiga *auction*, mama mjane, ana watoto, *shock, panic, then stress*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, benki tunaomba isikie sauti ya Bunge. Tunasema iwe na *facilitative*, twende na wananchi polepole, tuwasikilize changamoto, tuwahudumie kwa furaha maana tunataka tupeleke tabasamu kwa wananchi ambao walitupa ridhaa ya kuingia humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Muswada huu kwa kweli ni mzuri na ninaomba Bunge tuunge mkono. Umekuja wakati muafaka tunaposema sasa tunakwenda kwenye *Vision 2050*, tunataka kipato cha Mtanzania kiongezeke, kipato cha Taifa kiongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu haya machache, ninaendelea kuunga mkono hoja na maelezo mengine nita-*submit in writing*. Ninakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Josephine Kapoma, atafuata Mheshimiwa Thomas Kitima na mtoa hoja ajiandae.

MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninapenda kuunga mkono hoja hii na ninaomba Waheshimiwa

Wabunge tuupitishe Muswada huu kwa 100%. Ninaomba nijielekeze moja kwa moja; ukiipitia ripoti ambayo imewasilishwa na Kamati ya Bajeti utaona kabisa kwamba kuna fursa kubwa sana kwa kutumia mali zinazohamishika huko nje. Hizi fursa hata sisi ambao tunakutana na wananchi huko chini, wamekuwa mara nyingi wanashauri jinsi gani Serikali itawasaidia kiasi gani waweze kukopesheka kwa kutumia mali zinazohamishika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hususani ukiangalia wanawake walio wengi, kama wachangiaji wengine waliotangulia kuongea, kwamba mikopo mingi inataka mali ambazo hazihamishiki. Sisi wanawake tulio wengi tunajitahidi kufanya biashara ndogondogo na hatuna zile mali ambazo hazihamishiki. Kwa mfano, nyumba na ardhi; na hata ukikuta tunazo mara nyingi unakuta ni mali ya bibi na bwana, lakini kwa biashara zetu hizi, tungeweza kupata hii fursa ya kukopa kwa kutumia mali zinazohamishika, ninadhani wigo wetu wa biashara ungetanuka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukulia mfano, sasa hivi wanawake wengi wanajishughulisha na biashara ndogondogo. Kwa mfano kama biashara za upishi *(catering),* unakuta mwanamke ana biashara kubwa, ana vifaa vya kutumia vya *catering serving dishes* na vifaa vingine, lakini unakuta hana mali isiyohamishika. Serikali inaweza ikazitumia mali hizi ambazo anazo, ikazi-*convert* kama mali ambayo inaweza ikampatia mkopo kwa kutumia mali hizi ili aweze kutanua wigo wake wa biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mengi ya vijijini tuna wanawake wengi na vijana wengi wanaojihusisha na kilimo na ufugaji, lakini kutokana na sheria ambazo zilikuwepo awali, hawa watu hawawezi kukopesheka kwa sababu hawawezi kutumia mazao, wala hawawezi kutumia mifugo. Sasa kwa Sheria hii ambayo tunataka kuipitisha, tunaenda kuongeza wigo mpana sana kwa wafugaji na wakulima. Hii itasaidia, kwa sababu ninatolea mfano, ninatoka Mkoa wa Morogoro, Mkoa wa Morogoro tuna wanawake wengi na vijana wengi wanaojishughulisha na kilimo. Sasa hivi tuna mazao ambayo yanaingia stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kilimo tunajishughulisha na kilimo na katika kipindi cha kawaida tunafanya biashara nyingine. Hata hivyo, kutokana na kwamba hatuwezi kukopesheka kwa sababu hatuna mali zinazohamishika, inapelekea kuna kipindi lazima tuuze mazao yetu kwa bei ndogo ili tuweze kukidhi biashara zetu nyingine ndogondogo. Tukitumia mazao yetu, ambayo yako ghalani, kwa stakabadhi kutatuwezesha sisi tusiuze mazao yetu kwa presha ili kupata pesa kwa ajili ya kufanya biashara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, kuna watu wanafanya ufugaji. Sasa kuna sheria ambayo hairuhusu kukopesheka kama una mifugo. Kinachoshangaza, unaweza ukakuta mtu ana mali ambayo haihamishiki, ya shilingi 2,000,000, yuko *entitled* kukopesheka. Unamkuta mtu ana mifugo ya zaidi hata ya shilingi 200,000,000, lakini hawezi kukopesheka. Kwa ndugu zetu wanaofanya utafiti, ninadhani ni muda sasa wa kuangalia ni kiasi gani tunazisajili hizi mali zikawa katika mfumo rasmi ili waweze kukopesheka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie elimu; kikubwa ambacho sasa hivi wafanyabiashara wadogowadogo wengi wanachoki-*face*, ni kupata elimu ya matumizi sahihi ya mikopo na fedha. Kwa hiyo ninadhani, tukipanua wigo wa elimu kwa watu hawa ambao hawana mali zinazohamishika, ili waweze kuelewa mantiki kubwa ya kurejesha hii mikopo, ninajua tutaenda kuongeza wigo mkubwa. Si tu kuongeza wigo mkubwa, ukiangalia kwa asilimia kubwa sana huko chini, tuna watu wengi ambao hawakopesheki na wana uwezo wa kupanua biashara zao. Tukiweza kuwasaidia kwa kuwakopesha, maana yake tutaenda kuongeza wigo mkubwa wa walipaji kodi, kwa sababu walipaji kodi tunaowafikia, ni wale matajiri na watu ambao ni wachache na watu wengi wanakosekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaungana na waliotangulia kuchangia na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa ajili ya kwenda kuweka tabasamu kwa wananchi wetu, tuupitishe huu Muswada kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Thomas Kitima.

MHE. THOMAS M. KITIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia huu Muswada wa Sheria za Mali Zinazohamishika ambao Wizara ya Fedha imeuleta kwa ajili ya kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nilipongeze Bunge lako Tukufu kwa kumpitisha Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa kura nyingi, kura za kishindo. Tumeonesha kwamba Bungeni hapa tuna upendo mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii Sheria ambayo imekuja mbele yetu, ni sheria nzuri sana kwa sababu sasa wigo mpana wa wananchi wetu kuhusiana na mikopo unakwenda kupanuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanahitaji mikopo, lakini wamekuwa wakipata shida kuipata hii mikopo kwa sababu ya vigezo vingi ambavyo vimewekwa, ambavyo vinafanya wanashindwa kupata hizo huduma katika taasisi zetu mbalimbali zikiwemo za benki na hata hizi *microfinance* pamoja na hizi *SACCOS* ambazo zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, Muswada huu ama Sheria hii ambayo iko hapa, inaenda kuwasaidia. Niseme tu wazi, tulichelewa sana kupata hii Sheria kwa sababu tumekuwa tukishindwa kupata hizo haki za msingi za wananchi wetu ili kuweza kujiletea maendeleo. Kwa hiyo niipongeze Wizara ya Fedha kwa kuona kwamba kweli wananchi sasa ifike wakati waweze kupata huduma za kifedha kwa asilimia nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hayo, tunaweza kuona kwamba mikopo hii inaenda kutolewa kwa mali mbalimbali

zikiwemo amana, wananchi wanaenda kupata mikopo kupitia amana, hati fungani, vyombo vya moto ambapo wananchi ndiyo wengi kule. Bodaboda wako kule, wanaomiliki magari, matrekta na malori haya, wananchi wetu wako wengi kule. Sasa kupitia dhamana hii, wanaenda na kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wetu kupitia stakabadhi ghalani nao wameguswa na sheria hii, wanakwenda kupata mikopo yao. Vilevile watu mbalimbali waliowekeza, wenye mashine na wenye mitambo mbalimbali, kwa maana wenye viwanda, nao wanakwenda kupata mikopo kupitia sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wenye vito vya thamani, hatimiliki, pia wananchi ambao wanamiliki mifugo nao sasa wanaenda kuguswa na hii sheria. Mifugo inaenda kutumika kama dhamana ili waweze kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa wigo huu ulivyo mpana, kwa namna Serikali ilivyofungua njia za wananchi kuweza kupata huduma hizi za kifedha, ni dhahiri kweli kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ana mapenzi ya dhati na wananchi wa Taifa hili katika kuhakikisha anaweza kuwasaidia ili waweze kuinua vipato vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye kuchangia moja kwa moja. Niishauri Wizara, katika kufanya usajili wa mali hizi, tuhakikishe tunaondoa ule mlolongo mrefu wa mtu kusajiliwa mali yake kwa sababu tunaweza tukapitisha sheria vizuri, lakini bado kukawa na mlolongo mrefu wa mtu kupata usajili wa mali yake; kwa maana huenda akaambiwa vigezo pengine vikoje au akaanza kutafuta wapi pa kuanzia na wapi pa kuishia pasipo kupata huduma kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu tuna mikopo hii ya halmashauri na tunafahamu jinsi wananchi wanavyopata shida sana kuipata mikopo hii, japokuwa ni haki yao ya msingi. Sasa kupitia Wizara hii, ninaamini sasa Sheria hii itawaweka vizuri

waondoe ule urasimu wa wananchi kusajiliwa mali zao kwanza, halafu mikopo hii iweze kupatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tayari kuna mikopo ambayo imeshatolewa pamoja na kwamba Sheria hii ilikuwa bado haijapita, lakini tayari kuna watu wameshakopea vyombo vya moto, kuna watu wameshakopea mali zao ambazo zinahamishika; nao pia hizo mali kupitia Sheria hii itakapoanza kutekelezwa, basi zihuishwe ili huduma ambayo au kinga inayopatikana kutokana na Sheria hii iwe *covered* pia kwa watu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kama wataachwa ina maana wanaweza kupoteza kutokana na kutokuwepo kwa Sheria kama hii. Yule *valuer* ambaye anakwenda kuthamini kama wengine walivyoshauri, pia na yeye awe *sharp* kuwafikia wananchi kwa wakati ili waweze kusajiliwa mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kwa kuwa mikopo hii imetungiwa sheria na kwa kuwa mikopo hii ina usajili rasmi na kuna masijala ya usajili, basi tuombe Wizara ihakikishe kupitia kanuni, riba za mikopo hii ziwe nafuu ili kumsaidia mwananchi wetu. Kwa sababu lengo ni kumwinua mwananchi kiuchumi ili kuweza kufikia maono makubwa ya Mheshimiwa Rais katika kutimiza Dira ambayo tuko nayo mkononi ya mwaka 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mikopo hii ina bima ama inaenda kuwekewa bima, basi hii mikopo iko *secured almost* 100%, basi tusione shaka kwenye kanuni zetu ambazo zinakuja, basi iwe na riba iliyo nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha mwisho kabisa, niiombe Wizara iweze kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi wetu kwa sababu mali hizi ndiyo kwanza tunaenda kuziingiza kwenye sheria ili wapate wakati mzuri wa kusajili mali zao na waelewe nini wanaenda kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, wananchi wetu wanaofuga na wanaolima, basi wafahamu kwamba sasa na wao wako kwenye wigo huo wa kuweza kukopeshwa katika hii Sheria ya Mali Zinazohamishika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo machache ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hoja iliyoletwa na Serikali. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mtoa Hoja, Waziri wa Fedha.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Sambamba na shukrani zangu hizi kwako, ninaomba vilevile nitoe shukrani za dhati kabisa kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao kwenye mapendekezo yaliyowasilishwa na Serikali kupitia Muswada huu wa Sheria ya Mali Zinazohamishika wa Mwaka 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishashukuru sana Kamati yako ya Bajeti na kwa wasilisho lililofanywa na mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati ile, ninaamini Bunge lako limeelewa kwa nini niliishukuru sana Kamati? Ni wasilisho la kina, taarifa ya Kamati ya Bajeti imeonesha kazi kubwa ambayo Kamati iliifanya kwenye uchambuzi wa Muswada huu na mapendekezo ambayo hatimaye tulikubaliana kwa kiasi kikubwa upande wa Serikali na upande wa Kamati ya Bajeti. Kwa hiyo, kwenye hili ninaishukuru sana Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninaomba vilevile niwashukuru sana Wajumbe ambao wamesimama leo kuchangia kuanzia Mheshimiwa Ali Hassan King mpaka Mheshimiwa Thomas Kitima na wote kwa kuunga mkono Muswada huu. Vilevile, wengi wao wamenasibisha na mwelekeo wetu wa Dira ya Mwaka 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kinachopendekezwa katika Muswada huu kwa kiasi kikubwa kinalenga kwenda kutekeleza kwa vitendo malengo yetu tuliyonayo

katika Dira ya Mwaka 2050 ikiwemo kukuza uchumi wetu, lakini vilevile kuongeza kukuza kipato cha watu wetu na kubadilisha hali za wananchi na Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliosimama kuchangia wameeleza faida kubwa zilizoambatana na Muswada huu ikiwemo la kwanza kwenye kukuza mitaji ya wananchi hasa wenzetu wanaofanya biashara na ni kweli kwamba eneo hili ni eneo muhimu sana kwa ajili ya mustakabali wa kiuchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi sekta binafsi imekuwa ikilalamikia katika mambo matatu makubwa. Moja; kukosekana kwa soko *(access to market),* la pili ni changamoto iliyopo kwenye upatikanaji wa teknolojia za kujiimarisha katika shughuli zao kwa maana *access to technology* na la tatu ambalo ni kubwa ni ukosefu wa mitaji *(access to finance)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili ni kweli kwamba sehemu kubwa ya sekta yetu ya fedha ilikuwa imejengwa kwa kulitambua kundi moja kubwa, kundi ambalo lina mali zisizohamishika. Kwa hiyo, lilikuwa ni sharti kwa sehemu kubwa mteja anapohitaji mkopo, lazima aweke dhamana kutokana na mali zisizohamishika. Hii kwa upande mmoja imedumaza ukuaji wa sekta binafsi na kwa hivyo moja ya lengo la Sheria hii lilikuwa ni kuongeza *access to finance,* upatikanaji wa mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo imetajwa hapa kwamba sasa Sheria hii itakapopitishwa na Bunge lako hili Tukufu itakwenda kusaidia kufungua zaidi fursa ya upatikanaji wa mitaji kwa wenzetu ambao wanahitaji mitaji hiyo hasa kwa ajili ya uwekezaji wa ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia orodha ya mali ambazo zimeanza kutajwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliosimama na kwenye jedwali zimeanza kuwekwa nitaje baadhi yake. Kwa mfano, ninajua kuna Wabunge wengi wamechukua,

wamekuwa washiriki kwenye soko letu la hisa hasa upande wa hatifungani na wamekuwa wakinunua hatifungani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachopendekezwa hatifungani ni mali ambayo inahamishika. Kwa hiyo, miongoni mwa mali ambazo zinaweza zikatumika kupata mkopo sasa hivi mojawapo itakuwa ni hatifungani, lakini Watanzania walio wengi wana mali ambazo zinahamishika, lakini hazikuwa zikiwasaidia kufikia kupatikana mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, upande wa mifugo imetajwa hapa kwamba sasa wale wenzetu, ndugu zetu, Watanzania wenzetu wenye mifugo, pengine jamii ya wale ambao wanafuga, wote inawezekana wako Mikoa ya Arusha, Singida, Kanda ya Ziwa na maeneo mengine yote ambayo kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitegemea mifugo, sasa hivi mifugo mara itakapopitishwa Sheria hii ni moja ya mali ambayo itakuwa inawasaidia katika kupata mikopo na hivyo kujiendeleza zaidi katika shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliomiliki vyombo vya moto kwa sababu ilikuwa ni mali ambazo zinahamishika haikuchukuliwa kama ni moja ya dhamana ambayo ingeweza ikamsaidia mtu kupata fedha kupitia njia ya mikopo. Nayo sasa hivi ndugu zetu wenye bodaboda aliyenunua gari yake moja na vyombo vingine navyo, itawezekana kupata mkopo, lakini kinachopendekezwa kingine ni vito vya thamani na madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imebarikiwa kuwa na maeneo mengi ambayo kunapatikana madini. Tuna wachimbaji wadogo wadogo na wengine wakubwa, lakini wachimbaji wadogo wadogo katika maeneo ya Geita huko, Musoma, Mkoa wa Mara, Chunya kule, Kusini mwa Tanzania na maeneo mengine Tunduru na kwingine katika Mkoa wa Ruvuma. Hao wote hawakuwa wanaingia katika wigo wa kupata mikopo, lakini kupitishwa kwa sheria itakwenda kuwafungulia fursa ya kupatikana kwa mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Waheshimiwa Wabunge ambao wamesema Sheria hii inatoa fursa ya uwezeshaji kiuchumi na ni kweli vilevile kwamba sasa itakapopatikana mtaji tutaweza kuwawezesha wananchi kwa vitendo kuelekea kupatikana uwezeshaji kwa upande wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana na maoni ambayo yametolewa na Mheshimiwa Kitima na wengine kwamba wakati tunaelekea kurasimisha tutazame na upande wa pili ambao unaweka vikwazo hasa kwenye upande wa urasimu. Kwa hiyo, tunarasimisha, lakini urasimu uondoke katika urasimishaji ule; hili nalo tumelichukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mapendekezo ambayo yamejitokeza vilevile kwa Waheshimiwa kadhaa waliochangia, ni suala la kutolewa elimu. Sasa itakapopitishwa sheria, elimu ifike kwa walengwa ili wayajue haya yaliyomo, utaratibu wake, mali gani zinaweza zikatumika kwa ajili ya kupatikana kwa dhamana hiyo, lakini vilevile na utaratibu wote ambao watapaswa wafuate ili hatimaye wanufaike na sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili tumelichukua, tunajua tumekuwa tukitoa elimu ya masuala ya fedha. Kwa hiyo, eneo hili nalo sheria hii mpya itakuwa ni sehemu moja muhimu katika utoaji wa elimu ya fedha *(financial literacy)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumezungumzwa sana masuala ya kanuni hasa katika pande mbili; moja imetolewa rai hapa kwamba kanuni ambazo zitakwenda kutungwa kutokana na Muswada huu utakapokuwa sheria, ziendane na sheria yenyewe ili tuondoe uwezekano wa kutokea migongano isiyo ya lazima katika upande wa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa pili, kanuni zisaidie kushusha viwango vya riba ambavyo vinatumika katika soko kwa sasa hivi. Kwenye hayo yote mawili tukubaliane nayo kwamba tutajitahidi kwa kadri inavyowezekana na kwa vyovyote vile

itawezekana kwamba kanuni zetu ziendane na mawanda yaliyomo katika sheria yenyewe na tutajitahidi tuzitunge haraka ili Watanzania ambao walilengwa kutumia sheria hii waweze kunufaika kwa haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kupunguza riba tunatarajia sasa kwa kufungua eneo hili kubwa hata kwa kupitia nguvu ya soko kwa sababu kutakuwa na watu wengi ambao wanahitaji, sasa hivi tunategemea na riba nazo zitashuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumetolewa mchango kwa upande wa Benki Kuu hasa kwa sababu Benki Kuu ndiyo itakuwa anasimamia masijala ya mali hizi, Benki Kuu ijipange kuwafikia walengwa. Hili tunakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba ni kweli mtandao wa Benki Kuu ni mdogo ukilinganisha na mtandao wa walengwa wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo rai iliyotolewa pamoja na kwamba Benki Kuu ndiyo itakuwa inasimamia masijala, lakini inawezekana ikahitaji kutumia mtandao wa benki za biashara ili iwe ni rahisi kuwafikia walengwa ili na wao waweze kunufaika; hili nalo tumelichukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo nilitaka niliguse kidogo ni mwelekeo sasa wa kusaidia ukuzaji wa sekta binafsi *(private sector development)* kwa kutumia Sheria hii. Kutokana na manufaa yake pale ambapo tutakuwa tumeweza kuikuza sekta binafsi kama ambavyo imezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wako ni kwamba tunakoelekea ni kule ambako tulishazungumza awali. Tunataka Taifa letu lijitegemee kimapato na Sheria hii itatusaidia kwenye kutanua wigo wa mapato yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ambapo watu wengi watanufaika na mikopo itakayotokana na Muswada huu wa Sheria wakaweza kuwekeza, wakapata faida, wakaleta ajira kwa vijana na wengine wakajiajiri wenyewe; huku ni kweli tunatanua wigo wetu

wa mapato na kwa sababu hiyo itatusaidia vilevile kukuza mapato yetu ya ndani na kulielekeza Taifa letu kwenye kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa ujumla nimesimama kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa mchango wao na kwa kuunga mkono, wale ambao wamechangia na walioamua kuchangia kwa kukaa kimya vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ninakushukuru Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa ninaomba niwatambulishe wageni walioko Bungeni ambao ni wageni wa Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo ambao ni wanafunzi 144 pamoja na walimu 16 kutoka Shule ya Msingi Al-Bayaan ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Katibu.

NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI: Kamati ya Bunge Zima.

MWENYEKITI: Kamati ya Bunge Zima.

KAMATI YA BUNGE ZIMA

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae.

Katibu.

NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali Zinazohamishika wa Mwaka 2026

Ibara ya 1
Ibara ya 2

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Ibara ya 3

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Ibara ya 4

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Ibara Mpya ya 5
Ibara Mpya ya 6

(Ibara mpya zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Ibara ya 8

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Ibara ya 12

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Ibara ya 17

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Ibara ya 18

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Ibara ya 19

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Ibara ya 20
Ibara ya 21

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Ibara ya 22

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Ibara ya 23
Ibara ya 24

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Ibara ya 25

(Ibara iliyotajwa hapo ilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)

Ibara ya 26
Ibara ya 27

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Ibara ya 28
Ibara ya 29

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Ibara ya 34

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Ibara ya 35
Ibara ya 36

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Ibara ya 37
Ibara ya 38

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Ibara ya 39
Ibara ya 40
Ibara ya 41

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Ibara ya 42

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Kichwa cha habari cha sehemu ndogo (A) mara baada ya kichwa cha habari cha Sehemu ya Nane.

(Kichwa cha habari kilichotajwa hapo juu kinachopendekezwa na Serikali kuongezwa kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)

Ibara ya 43
Ibara ya 44

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47
Ibara ya 48

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Ibara ya 49

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Ibara ya 50
Ibara ya 51

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Ibara ya 52
Ibara ya 53

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Ibara ya 54

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Ibara ya 55

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaongeza muda mpaka shughuli iliyoko mbele yetu itakapokamilika.

NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:

Kichwa cha habari cha sehemu ndogo (B)

(Kichwa cha habari kilichotajwa hapo juu kinachopendekezwa na Serikali kuongezwa kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)

Ibara Mpya ya 56
Ibara Mpya ya 57
Ibara Mpya ya 58

(Ibara Mpya zilizotajwa hapo juu zilizopendekezwa na Serikali kuongezwa zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)

Ibara ya 56

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Ibara ya 57
Ibara ya 58
Ibara ya 59

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Ibara ya 60

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Ibara ya 61
Ibara ya 62
Ibara ya 63

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Ibara ya 64

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Ibara ya 65
Ibara ya 66
Ibara ya 67
Ibara ya 68
Ibara ya 69
Ibara ya 70
Ibara ya 71
Ibara ya 72
Ibara ya 73
Ibara ya 74
Ibara ya 75
Ibara ya 76
Ibara ya 77
Ibara ya 78
Ibara ya 79

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Mabadiliko ya mpangilio wa Ibara ya 5 – 79 kuwa Ibara ya 6 – 82

(Mabadiliko ya mpangilio wa Ibara yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)

NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Hapa Bunge Lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae. Mheshimiwa Waziri, taarifa.

T A A R I F A

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali Zinazohamishika wa Mwaka 2026, Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwahoji kuhusu Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali Zinazohamishika wa Mwaka 2026.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali Zinazohamishika wa Mwaka 2026 Ulipitishwa na Bunge)

Waheshimiwa Wabunge, walioafiki, wameshinda. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sasa ninatamka rasmi kwamba Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali Zinazohamishika wa Mwaka 2026 umepitishwa na Bunge.

Katibu.

NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:

MUSWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kuweka Masharti ya Usimamizi wa Maslahi katika Dhamana za Mikopo za Mali Zinazohamishika, Kuanzisha Masijala ya Usajili wa Maslahi katika Mali Zilizotumika kama Dhamana, Kuainisha Masharti ya Utengenezaji wa Vipaumbele na Utekelezaji wa Maslahi katika Dhamana, Kuainisha Haki na Wajibu wa Wahusika wa Maslahi katika Dhamana na Masuala Mengine yanayohusiana na hayo.

(Kusomwa Mara ya Tatu)

MWENYEKITI: Muswada umesomwa kwa mara ya tatu. Waheshimiwa Wabunge kama Bunge tumehitimisha hatua zote za upitishwaji wa Muswada huu na sasa Muswada huu utaendelea katika hatua zingine za kuthibitishwa na Mamlaka.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema haya nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri pamoja na timu yako yote ya Wizara kwa kazi kubwa mliyofanya ya

kuhakikisha Muswada huu unafika Bungeni. Pia niipongeze Kamati yetu ya Bajeti kwa kuuchambua, kutoa maoni, kufanya maboresho na hatimaye sasa Bunge limeupitisha rasmi. Tunawatakia utekelezaji mwema. *(Makofi)*

Kubwa ambalo Wabunge wamesisitiza ni kutoa elimu ili watu wetu wajue, kufahamu na hatimaye waweze kutumia fursa zilizopo kukopa kwa mujibu wa Sheria hii. Tunawatakia kila la kheri.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema haya ninaomba niahirishe Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 7.06 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 1 Septemba, 2026 Saa Tatu Asubuhi)